# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

Kikao cha Tano – Tarehe 25 Aprili, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Hati za Kuwasilisha Mezani.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:**

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2015. *(The Annual Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of the Local Governments for the Year Ended 30 Juni, 2015).*

Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Selikali kwa Hesabu za Selikali za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia 30 Juni, 2015.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mchakato wa Tathmini ya Athari ya Mazingira katika Miradi ya Maendeleo *(Performance Audit Report on the Management of the Environmental Impact Assessment Process in Development Projects).*

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Mazingira katika Shughuli za Utafutaji wa Petroli Tanzania *(Performance Audit Report on the Compliance, Monitoring and Enforcement of Environmental Policies, Laws and Regulations as Regards to Petroleum Exploration Activities in Tanzania)*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2015 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Central Government for the Year Ended 30th June, 2015)*.

Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa Kipindi Kinachoishia tarehe 31 Machi, 2016 *(A General Report of the Controller and Auditor General on Performance and Specialized Audit for the Period Ending 31st March, 2016)*.

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia tarehe 30 Juni, 2015 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Development Projects for the Year Ended 30th June, 2015)*.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2015 *(The Annual General Reportof the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Public Authorities for the Year Ended 30th June, 2015)*.

Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi Katika Taarifa Sita za Ukaguzi wa Ufanisi zilizotolewa na Kusomwa Bungeni Kuanzia Mwaka 2009 hadi 2012 *(The Follow-Up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for the Six Performance Audit Reports Issued and tabled to Parliament between 2009 and 2012)*.

Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 *(Volume I* na *Volume II)*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi na Mchakato wa Utoaji wa Leseni na Mikataba ya Ufuatiliaji na Uendeshaji wa Shughuli za Mafuta na Gesi Asilia *(Performance of Audit Report on the Management of Process of Awarding Exploration and Development Contracts and Licenses for Oil and Natural Gas in Tanzania)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Menejimenti ya Taarifa za Kijiofizikia na Kijiolojia katika Sekta za Mafuta na Gesi Asilia Nchini Tanzania *(Performance Audit Report on the Management of Geophysical and Geological Data for Natural Gas in Tanzania)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali Watu katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia Tanzania *(Performance Audit Report on the Management of Human Capital Development for Engaging in Natural Gas Industry in Tanzania)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Utekelezaji wa Masharti ya Ushirikishwaji wa Watanzania na Uhakiki wa Urejeshwaji wa Gharama za Uwekezaji kwenye Mikataba ya Mgawanyo wa Mapato ya Uzalishaji *(Performance Audit Report on the Implementation of Local Content Provisions and Verifications of Revocable Costs in the Production Sharing Agreements)*.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Udhibiti wa Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mazao ya Kilimo Tanzania *(Performance Audit Report on the Implementation of Strategies for Managing Agricultural Crop Pests and Diseases Outbreaks in Tanzania)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Udhibiti wa Usafi katika Mchakato wa Uzalishaji Nyama *(Performance Audit Report on the Hygiene Control in Meat Production)*.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha unaoanzia 2010/2011 hadi Mwaka 2013/2014 *(Performance Audit Report on the Construction Contract Management of Urban Water Project at the Ministry of Water and Irrigation for the Financial Year 2010/2011 to Financial Year 2013/2014)*.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Mifumo ya Udhibiti wa Ubora wa Elimu Nchini Tanzania *(Performance Audit Report on the System for Quality Control of Education Programs in Tanzania)*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatua itakayofuata ni Kamati husika kuchambua Taarifa hizo na kutoa taarifa Bungeni kwa wakati utakaopangwa. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mheshimiwa Emmanuel John Papian, Mbunge wa Kiteto sasa aulize swali lake.

Na. 41

### Hitaji la Gari la Wagonjwa na Mafuta - Kiteto

**MHE. EMMANUEL P. JOHN** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza gari la wagonjwa na mafuta ili kufanya huduma za kliniki katika maeneo hayo pamoja na huduma nyingine kuwaokoa kina mama na watoto?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto inayo magari mawili ambayo yamekuwa yakitumika kubeba wagonjwa waliopewa rufaa ya matibabu. Magari haya pia hutumika katika huduma ya mkoba za kliniki za Afya ya Uzazi na Mtoto *(RCH)* kwa lengo la kuwaokoa akina mama na watoto. Katika Mpango wa Bajeti ya mwaka 2016/2017, Halmashauri haikuweka kipaumbele cha ununuzi wa gari la wagonjwa kutokana na ukomo wa bajeti. Tunaishauri Halmashauri iendelee kutumia magari mawili yaliyopo huku

ikijipanga kuweka kipaumbele cha ununuzi wa gari kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2015/2016, Halmashauri hiyo ilitengewa shilingi 43,283,040 kwa ajili ya mafuta ya gari na hadi sasa fedha zote zimeshapelekwa. Changamoto ya kijiografia ndiyo inaonekana kuwa tatizo linalosababisha bajeti iliyotengwa kutokidhi mahitaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya Kiteto yanajulikana, tunayo maeneo makubwa sana ambayo Kata za Makame kwa wafugaji, Kata za Rolela na Kata ya Kijungu, mazingira haya akina mama wamekuwa hawawezi kupata kliniki kwa sababu ya mafuta yanapokuwa yamekwisha hawawezi kupata zile kliniki ambazo gari zetu zina-*rotate Monthly* na hizi gari zinapoharibika wanashindwa kupata…

**NAIBU SPIKA:** Naomba uulize swali Mheshimiwa John.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN**: Naomba kuuliza ni lini tunaweza kupata fedha za nyongeza kwa ajili ya mafuta ili watu hawa waweze kupata huduma ya kliniki kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilisema katika jibu langu la msingi kwamba, ni kweli Halmashauri ya Kiteto ina changamoto kubwa sana kijiografia na hili tunakiri wazi na ndiyo maana hata bajeti ukiipeleka wakati mwingine inakutana na changomoto kubwa sana! Kwa hiyo, maelekezo yetu kama Ofisi ya Rais TAMISEMI ni kwamba niwashauru wananchi wa Kiteto hasa ndugu zetu wa Halmashauri Wakurugenzi na timu yake wahakikishe kwamba wanaweka mkazo wa kutosha katika kipindi hiki cha mpito kabla hatuaanza mwaka mpya wa bajeti. Wafanye udhibiti wa kutosha katika *own source* ili wakikusanya mapato ya ndani, japo kipindi hiki kilichobakia cha kumaliza mwaka wahakikishe kwamba wanakusanya fedha nyingi ili gari muda wote ziweze kufanya kazi na akina mama waweze kupata huduma. Lakini nikiri ni kweli Halmashauri ya Kiteto ni moja ya Halmashauri ambazo tunatakiwa tuziangaliye karibu. Ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Mlalo ndiyo kituo pekee kinachofanya huduma ya upasuaji katika Jimbo la Mlalo.

Je, ni lini Serikali itakipatia kituo hiki gari la wagonjwa ili pale ambapo upasuaji unakwama waweze kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Lushoto? Ahsante!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshmiwa Naibu Spika, ni kweli Kituo cha Afya cha Mlalo kina changamoto ya gari. Lakini wiki iliyopita nilizungumza kwamba wakati mwingine hizi changamoto ni kweli, naomba ikiwezekana tuweke *priority* katika mchakato wa bajeti. Mheshimiwa Shangazi kwa sababu najua ni mfuatiliaji sana katika maeneo yako haya, tukiri kwamba mwaka huu Mlalo hawajapanga hii bajeti kwa ajili ya ununuzi wa gari, lakini naomba niwasisitize kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI itakuwa nanyi kwa karibu kuhakikisha katika bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja Mlalo inapewa kipaumbele au tukipata fursa yoyote ya upatikanaji wa gari basi Mlalo iwe kipaumbele kwa sababu eneo lake na jiografia yake mpaka kuja huku Mjini changamoto yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tulichukue hilo kama Ofisi ya Rais TAMISEMI tukishirikiana nanyi kwa pamoja kuhakikisha watu wa Mlalo baadaye wapate gari la wagonjwa ili akina mama na watoto waweze kupata huduma ya kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea naomba kuwakumbusha Kanuni ya 42(2), wale wanaouliza swali wanaelekezwa hapo jinsi ya kuuliza maswali. Muuliza swali anapaswa aseme hivi; "Naomba swali langu, ataje namba ya hilo swali halafu aseme sasa lijibiwe," ndiyo Kanuni inavyosema. Kwa hiyo tuangalie Kanuni zetu 42(2) ndivyo swali linapaswa kuulizwa.

Tunaendelea, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 42

**Hitaji la Ofisi na Nyumba za Watumishi –**
**Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Wilaya ya Itilima ni moja kati ya Wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwezesha kujenga ofisi na nyumba za watumishi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima eneo la Itilima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa ujenzi wa nyumba za watumishi na viongozi katika Wilaya mpya ya Itilima umeshaanza na uko katika hatua ya ujenzi wa nguzo za jamvi. Fedha zilizopokelewa kwa kazi hiyo ni shilingi milioni 100 kati ya shilingi 500 zilizotengwa mwaka 2014/2015. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017 zimetengwa tena shilingi milioni 500 ili kuendelea na ujenzi wa nyumba na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima imesaini Mkataba na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kwa ajili ya ujenzi wa nyumba saba za watumishi kwa gharama ya shilingi milioni 450 na fedha hizo zipo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 47 zimetumika kuwalipia fidia wananchi waliohamishwa kupisha ujenzi huo. Vilevile katika bajeti ya mwaka 2016/2017 zimetengwa shilingi milioni 500 ili kuendelea na ujenzi wa nyumba na ofisi ya Halmashauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Lukago Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa, watumishi wetu hawa inawalazimu kuishi Wilaya nyingine ya Bariadi ambapo kuna umbali wa Kilometa 100 kwenda na kurudi kila siku.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuharakisha makazi haya ili watumishi hawa waishi katika maeneo husika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inaona hilo, ndiyo maana hata Halmashauri yenyewe ya Itilima katika mkataba wao waliosaini na *National Housing,* bahati mbaya mkataba ule ulikuwa haujahusisha Ofisi ya Rais - TAMISEMI wala Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pale katika Ofisi ya *RAS* na ndiyo maana

Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliona kwamba licha ya mapungufu yaliyokuwepo lakini ofisi iweze kutoa kile kibali kwa mkataba ule. Hivi sasa Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeshatoa kibali, na kwa sababu fedha tayari ninazo na kibali kimeshapatikana, imani yangu ni kwamba ujenzi kupitia Shirika la Nyumba utakamilika haraka iwezekanavyo ili kuondoa kero ya watumishi ambao wanapata taabu kutoka katika Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Bukoba Vijijini wanategemea Wilaya yao iliyoko Bukoba Mjini na ina umbali mkubwa sana, kata zake ziko mbali sana kuja kufika Bukoba Mjini, ni lini Serikali itaona umuhimu wa watu wa Bukoba Vijijini kupata Wilaya yao karibu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika hili tumelichukua, lakini mchakato wa Wilaya, mchakato wa Halmashauri upo na una taratibu zake. Mimi naomba niwahimize ndugu zangu wa Bukoba na Mheshimiwa Mbunge hapa nadhani katika hili atakuwa amejipnga vyema, tufuate ule mchakato wa kawaida, tupitishe katika Halmashauri zetu, tupitishe katika vikao vya *DCC, RCC*, mwisho wa siku ikifika katika Ofisi ya Rais -TAMISEMI jukumu letu kubwa ni kuweza kuangalia matakwa ya jamii na kuangalia mahitaji ya msingi yakiwa yamekamilika basi tutamalizia hilo zoezi. Ahsante sana.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ilipata kuwa hadhi ya Wilaya toka mwaka 2002 lakini majengo mengi katika Wilaya bado hayajakamilika, kama Hospitali ya Wilaya bado wanatumia Hopitali ya *Mission*, Makao Makuu ya Polisi bado hayajajengwa kwenye Wilaya yake na vilevile Mahakama bado hakuna…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba uulize swali!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, huwa vigezo gani vinatumika katika kuweka mipango kujenga hizi Wilaya? Kwa sababu Wilaya za zamani bado hazijatimiziwa majengo yote na zinaanzishwa Wilaya mpya, nilitaka nijue vigezo gani vinatumika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba miundombinu ya Wilaya ya Kilolo bado haijakamilika, siyo Wilaya ya Kilolo peke yake isipokuwa ni Wilaya mbalimbali, vipaumbele vinavyotumika kwanza mazoezi yote yanaanza katika mchakato wa bajeti, na ndiyo maana mwaka huu ukiangalia tuna karibu Wilaya zipatazo 44, hizi ni Halmashauri na Wilaya mpya mbalimbali ambazo tumezipa fedha.

Hali kadhalika tunaangalia upungufu katika maeneo mbalimbali. Imani yangu kubwa ni kwamba suala la Kilolo limesikika na kwa sababu tuna Wilaya mpya na Halmashauri nyingine tunaendelea katika ujenzi wa miundombinu, tukifika katika mafungu yetu ya Mikoa utakuja kubainisha kwamba jinsi gani kila Mkoa katika mafungu yake yameweza kuelekezwa. Ile sehemu ambapo miundombinu haijakamilika lakini Wilaya ambazo ni mpya tunaanza kuziasisi tena upya, jinsi gani tume-*allocate funds* katika mwaka huu wa fedha ili tuweke hali halisi ya kuhakikisha kwamba wafanyakazi katika maeneo hayo waweze kufanyakazi katika mazingira rafiki.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini sasa aulize swali lake.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru…

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Maftaha, naomba ukae Waziri anataka kuongezea.

Mheshimiwa Waziri TAMISEMI!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA(MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Naibu Waziri Jafo, nilitaka tuelewane kwenye jambo hili la uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni gumu na sote hapa tunafahamu kwamba maombi haya ya kuanzisha haya maeneo yanatokana na mahitaji ya wananchi. Lakini ni sisi wenyewe kwenye maeneo yetu ndiyo huwa tunaanzisha haya. Kwa kuwa maombi haya yanakuja mengi na wakati mwingine Serikali siyo rahisi sana kupata fedha kwa mara moja kujenga mahitaji yote ya Makao Makuu ya Halmashauri au Wilaya ni lazima tuvumiliane. Ni lazima tuvumiliane twende kidogo kidogo na ndiyo maana Serikali imekuwa ikitenga milioni 500, tunaamini tukifanya hivyo kwa miaka mitano, miaka minne, tunaweza tukakamilisha majengo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuvumiliane kwa sababu Wabunge wengi wanakuja kuniona wakiwa na maombi mapya ya maeneo mengine ya utawala, sasa tukianza kuulizwa maswali kama kwa nini tunakuwa hatujajipanga na tunayaanzisha, kuna wengine hapa mmeahidi huko mlikotoka kwamba sisi tutahakikisha hapa panakuwa Mji Mdogo, sisi tutahakikisha tunakuwa na Halmashauri, sisi tutahakikisha tunakuwa na Wilaya.

Sasa tuvumiliane na tuende pamoja na tuamini kwamba kadri Serikali itakapopata uwezo tutakuwa tunafanya, lakini jambo hili ni gumu. *(Makofi)*

Na. 43

**Kuboresha Miundombinu ya Barabara - Mtwara Mjini**

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA** aliuliza:-

Mafuriko yanayotokea Mtwara Mjini kila mwaka hasa katika Kata ya Shangani, Cuono, Magomeni na Ufukoni yanasababishwa namiundombinu mibovu ambayo imejengwa chini ya kiwango katika maeneo mengi ya Mji wa Mtwara:-

(a) Je, Serikali iko tayari sasa kujenga upya mitaro, madaraja pamoja na miundombinu mingine ili maji yaweze kusafiri kuelekea baharini wakati wa masika?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara ya Mikindani - Lwelu ufukweni mwa bahari kwa kiwango cha lami ikizingatiwa kuwa barabara hiyo iko ndani ya Manispaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016 imetenga Dola za Kimarekani 540,000 kupitia mradi wa *Tanzania Strategic Cities Project (TSCP)* kwa ajili ya upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi wa mradi wa barabara ambao utahusisha ujenzi wa mitaro na madaraja ambao utahusisha uboreshaji wa miundombinu iliyoharibika na mvua. Utekelezaji wake upo katika kukamilisha hadidu rejea ili utaratibu wa manunuzi ya kupata Mkandarasi Mshauri ziweze kufikika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza matengenezo ya barabara ya Mikindani- Mchuchu- Lwelu kwa kiwango cha lami, ambapo katika mwaka wa fedha 2013/14 kilometa moja ilitengenezwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika wakati wote, Serikali katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 imetenga shilingi 89,000,000 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo. Azma ya Serikali ni kuijenga barabara hiyo yote ya kilometa 11 zilizobaki kwa kiwango cha lami kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nachuma, swali la nyongeza!

**MHE ABDALLAH N. MAFTAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mtwara Mjini kila kipindi cha masika maji huwa yanajaa na mafuriko yanatokea na Serikali inatoa kilo 16 za unga, je, Serikali iko tayari hivi sasa kusema tarehe ngapi itaanza ujenzi wa miundombinu Mtwara Mjini?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri kadanganywa katika jibu lake nililiouliza kwamba Barabara ya Mikindani- Lwelu itajengwa lini kwa kiwango cha lami, yuko tayari hivi sasa kufuatana na mimi kama Mbunge ili aweze kujionea mwenyewe kwamba kadanganywa? Ahsante *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la lini barabara hii itajengwa nadhani katika jibu langu la msingi nimesema. Katika Mradi ule wa *Strategic City* ambapo lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tuna maeneo mbalimbali ya miji ambayo imejengwa miradi hii, hata ukiangalia pale Tanga, ukiangalia Mbeya ukiangalia Arusha, huu ndiyo mpango mkakati, hivi sasa tunakwenda hata katika Jiji la Dar es Salaam. Eneo hili nimesema kwamba mchakato wake sasa uko katika hali ya manunuzi, lengo ni kwamba bajeti hii sasa mchakato utakapokamilika maana yake miundombinu inakwenda kujengwa. Lakini kusema kwamba nimedanganywa au vipi nitafika kule Mtwara, naomba nikwambie Mheshimiwa Mbunge, siyo Mtwara peke yake, nitahakikisha maeneo yote, ikiwemo na Mtwara niende nikakague maeneo ya *field,* hii ndiyo kazi kubwa tumekuwa tukiifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuweza kufika kila maeneo kubaini changamoto mbalimbali na hasa katika kipindi hiki mvua inanyesha, maeneo mengi sasa hivi yameharibika. Taarifa ya habari pale ukiangalia jana Kyela, ukiangalia Morogoro na maeneo mbalimbali yameharibika. Kwa hiyo, ni jukumu la Ofisi hii, kufika kila mahali kubaini uhalisia wa eneo lile wananchi waweze kupata huduma inayokusudiwa na Serikali yao.

Na. 44

**Tatizo la Maji Kigoma Kaskazini**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Maji ni tatizo kubwa kwenye Jimbo la Kigoma Kaskazini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishaanza utatuzi wa tatizo la maji katika Jimbo la Kigoma Kaskazini kupitia miradi ya maji inayotekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Utekelezaji wa miradi hiyo umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mradi wa Maji wa Nyarubanda, Kagongo na Nkungwe inayohudumia wananchi wapatao 13,757 imekamilika. Taratibu za kumpata Mkandarasi atakayejenga mradi wa maji wa Kalinzi zimekamilika. Fedha zikipatikana Mkataba utasainiwa ili mkandarasi aanze kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Serikali inaendelea kutatua kero ya maji katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, Halmashauri ya Kigoma imepanga kutekeleza miradi mbalimbali katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017. Vijiji vilivyowekwa kwenye mpango huo ni Mwandiga, Kibingo, Kiganza, Kaseke, Nyamoli, Mkigo, Matendo, Pamila, Matyazo, Mkabogo, Kiziba, Kidahwe, Kigalye, Kalinzi, Kalalangabo, Mtanga, Bugamba, Nyamhoza, Kizenga, Mgaraganza, Mahembe, Samwa, Bubango, Chankele, Kagunga, Zashe, Bitale, Mwamgongo, Machazo na Mkongoro.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majawabu mazuri ya Naibu Waziri wa Maji, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Mradi wa Kalinzi huu ni mwaka wa tatu mfululizo zinawekwa fedha kwenye bajeti hazijawahi kuja, naomba leo Waziri alieleze Bunge lako, sasa fedha zilizotengwa mwaka huu zitakuja ili mradi huu uweze kutekelezwa?

Swali la pili, tunalo tatizo kubwa sana la mazingira, vijiji vyote alivyovitaja vinategemea kupata maji kwenye mito na ikifika kiangazi karibu yote inakauka, kwa hiyo tatizo linarudi kuwa palepale. Sasa, Serikali haioni imefika wakati kutumia maji ya *Lake Tanganyika* ili yaweze kuchukuliwa ili kupeleka maji kwenye vijiji vyote hivi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inatenga fedha kila mwaka kama alivyosema, lakini kutokana na matatizo ya upatikanaji wa fedha, na sisi sote ni mashahidi, uchumi

umekumba dunia yote, kwa hiyo hali ya upatikanaji wa fedha ulikuwa kidogo mgumu. Lakini kwa sasa baada ya kuanza Serikali ya Awamu ya Tano ambayo inakusanya fedha vizuri nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa fedha itapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na pili kwenye Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Maji ambayo tunashirikiana na wadau, mwezi Januari mwaka huu tayari tumeanza Programu ya Pili na tuna ahadi za kutosha za kupatiwa fedha kutoka kwa wadau tunaoshirikiana nao.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huo sasa utatekelezwa na utafiti umeshakamilika kama nilivyojibu kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili ni kweli kwamba kipindi cha kiangazi maeneo mengi ya Jimbo lako, mito ile inayotiririsha maji inakauka. Lakini pia wewe mwenyewe ni shahidi kwamba sasa hivi kuna mradi mkubwa wa maji ambao tunajenga Mji wa Kigoma na tunachukua maji kutoka Ziwa Tanganyika  na mpango huo kwa sasa Wizara ya Maji inataka kutumia vyanzo vyote vya maji ambavyo viko karibu na miji ambayo imepata bahati ya kuwa karibu na vyanzo vizuri vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tumeanza mradi wa maji Mjini Kigoma, na kadri jinsi tutakavyokuwa tunakwenda, yale maeneo ambayo hayatakuwa na chanzo kizuri cha maji tutaendelea kutumia maji ya *Lake* Tanganyika kufika mpaka kwenye maeneo yenu. *(Makofi)*

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali fupi la nyongeza.

Wilaya ya Ilemela ilikuwa ina mradi ambao ulikuwa unatakiwa kukamilika mwaka 2014, mradi huu ambao ulitakiwa kuwanufaisha Kata za Wilaya ya Ilemela ikiwepo Kata ya Kayenze, Sangabuye, Shibula, Monze na Buswelu ambayo ni Kata Mama ya Wilaya ya Ilemela.

Je, ni lini mradi wa tenki hili la kutoa maji Wilaya ya Ilemela utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi umekuwepo Wilaya ya Ilemela na ulishindwa kukamilika. Tulipata matatizo kidogo baada ya kuanza Programu ya Sekta ya Maji Awamu ya Kwanza iliyoanza mwaka 2007, programu ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, lakini kwa sababu fedha nyingi tulikuwa tunapata za wafadhili, ule mchakato wa manunuzi, kwa mfano mwaka 2007 ndiyo programu ilianza, lakini kuja kupata *no objection* ya kuanza kusanifu tuliipata Disemba mwaka

2009, utekelezaji wa miradi ukaanza mwaka 2012. Kwa hiyo, hicho ndiyo kitu ambacho kilifanya miradi mingi isikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunatoa ahadi kwamba miradi yote ambayo haikukamilika tunaanza nayo tukamilishe ndiyo tunaingia kwenye miradi mipya. Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba Kata zako zote za Wilaya ya Ilemela katika Programu ya Pili ya Mpango wa Maji itafikiwa na itakamilika.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa sababu matatizo ya maji katika jimbo langu yanafanana sana na Jimbo la Kigoma Kaskazini, ninapenda nimuulize Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali hii itakamilisha Mradi wa maji katika Mji wa Tunduma kwa sababu imekuwa inaahidi mara nyingi kwamba itatengeneza maji na hata wakati Mheshimiwa Rais anaomba kura kwa wananchi pia alisema kwamba ataweza kuwaletea maji haraka iwezekanavyo ndani ya mwaka mmoja mradi utaanza kutekelezwa. Leo hii kuna kampuni ambayo tayari imekubali kujenga…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, swali si umeshauliza? Nadhani swali umeshauliza, kwamba huo mradi utakamilika lini?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nikumbushe kidogo kwa sababu kuna kampuni leo imekuja hapa na mradi ule umeshapitishwa na Wizara lakini tunashangaa Wizara ya Fedha hawataki kukubali mradi ule uanze kujengwa haraka. Kwa sababu mradi ule ulitakiwa uanze kujengwa mwanzoni mwa mwaka huu lakini mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea. Tunataka kupata majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuwapatia wananchi wote maji safi na salama kwa kiwango cha asilimia 85 ifikapo mwaka 2020. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie, hayo unayoyazungumza ni historia, Serikali inakwenda kutekeleza Mradi wa Maji Tunduma ambao nina uhakika na tuwashauri wananchi wa Tunduma waiamini Serikali ya Awamu ya Tano. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 45

**Viwanda vilivyobinafsishwa - Moshi na Mafao ya Watumishi Waliostaafishwa**

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL** aliuliza:-

Viwanda vingi vya Moshi vilibinafsishwa havifanyi kazi, badala yake vimegeuzwa kuwa maghala ya kuhifadhia bidhaa mbalimbali na vimechakaa sana; aidha mafao ya wafanyakazi waliostaafishwa katika Kiwanda cha Magunia na *Kilimanjaro Timber Utilization* hayakulipwa inavyostahili na hivyo kuwepo kwa malalamiko ya muda mrefu ya madai yao bila mafanikio:-

(a) Je, kwa nini Serikali isivikabidhi viwanda hivyo kwa kampuni nyingine zenye uwezo wa kuviendeleza na hivyo kupunguza tatizo la ajira katika Mji wa Moshi?

(b) Je, ni lini madai ya mafao ya wafanyakazi waliostaafishwa katika viwanda hivyo yatalipwa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na zoezi la kufanya Ufuatilliaji na tathmini katika viwanda na mashirika ya umma yaliyobinafsishwa ili kubaini kama masharti ya vipengele vya Mikataba ya mauzo iliyoingiwa kati ya Serikali na wawekezaji yametekelezwa ili kuchukua hatua stahiki. Katika utekelezaji wa zoezi hilo, pamoja na mambo mengine mikataba yote ya mauzo inapitiwa na endapo itagundulika kuwa masharti ya mikataba husika yamekiukwa, hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwemo Serikali kuvirejesha viwanda hivyo. Pia wawekezaji mahiri wenye nia ya kuwekeza nchini watatafutwa. Vilevile viwanda ambavyo vitaonekana wamiliki wana nia na uwezo wa kuvifufua, makubaliano mapya yatafikiwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wote katika viwanda vilivyotajwa walilipwa stahiki zao. Hata hivyo, baada ya malipo hayo kutolewa wafanyakazi waliendelea kudai zaidi madai yanayotokana na Mikataba ya Hiari. Serikali ilishatolea ufafanuzi suala hili kuwa madai yanayotokana na Mkataba wa Hiari yanapaswa kulipwa kutokana na hali ya uzalishaji wa kiwanda au kampuni kwani yanalenga kugawana ziada ambayo kiwanda

kama cha Magunia *(Tanzania Bag Corporation –TBCL)* hakikuwa nayo, wakati kile cha *Kilimanjaro Timber Utilization* kiliuzwa kwa ufilisi.

Aidha, wakati zoezi la ubinafsishaji linatekelezwa, kiwanda cha Magunia cha Moshi kilikuwa na malimbikizo ya mishahara ya Wafanyakazi wake kwa zaidi ya miezi 18 hivyo hakikuwa hata na uwezo wa kulipa malipo ya kisheria, hivyo madai ya nyongeza hayakuwa na msingi. Serikali haiwajibiki kulipa mafao yoyote kwa wafanyakazi waliokuwa katika viwanda vya Magunia na *Kilimanjaro Timber Utilization*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raphael Japhary Michael swali la nyongeza.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majibu ya namna hiyo kuhusu viwanda vya Moshi yamekuwa yakitolewa mara kwa mara katika Bunge lako Tukufu bila utekelezaji; na kwa kuwa ilikuwa ni moja wapo ya ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba kwa muda mfupi sana viwanda vile vingetwaliwa kwa waliovitumia bila utaratibu.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kutoa muda halisi kwa maana ya *time frame* ya lini viwanda hivyo vitatwaliwa kwa watu ambao wameshindwa kuvifanyia kazi katika malengo halisi yaliyokuwa yametarajiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa majibu ya Serikali hayaakisi ukweli ulivyo kuhusu wafanyakazi, kwa sababu madai yao ni ya msingi na fedha wanazodai siyo za mikataba ya hiari na wamekuwa wakidai fedha hizo tangu mwaka 1998, na kwa kuwa Serikali haijataka kuwa karibu nao…

**NAIBU SPIKA**: Naomba uulize swali tafadhali!

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Je, ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuanza kufuatilia ukweli wa madai hayo na kuwa karibu na hao wafanyakazi ili waweze kutoa ufafanuzi unaoridhisha wafanyakazi hao kuondoa manung'uniko yao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na (b) suala la maslahi ya wafanyakazi ni lako wewe, ni langu mimi. Wewe kama Mwakilishi wao na mimi kama Kiongozi wa Serikali, mimi na wewe tuwasiliane tutakwenda wote mpaka Moshi tuwaone hao watu tuzungumze nao tutakwenda kwa Msajili wa Hazina, tutaweza kujua mbichi na mbivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali (a) Mheshimiwa Rais amezungumza bayana, na mimi nimekuwa nikizungumza mara nyingi kuhusu viwanda ambavyo havifanyi kazi. Jambo moja ambalo tunapaswa kulielewa kuna suala la kisheria kuhusu hivi viwanda vilivyobinafsishwa, kwa hiyo, tunajitahidi kufuata hizo sheria kusudi tuvitwae kisheria kusiwepo migongano. Nia yetu nikuona hivyo viwanda vinafanya kazi haraka sana, hatutaki kwenda mahakamani. Kwa hiyo, viwanda hivyo vitatwaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za kuvitwaa tunawafuata wale watu ni Watanzania wenzetu tunawauliza kitu gani kilichowasibu? Sababu nyingine zina mantiki na kuna baadhi ya viwanda vimeshaleta *proposal* namna gani vitaweza kufufuliwa. Tumewapa wataalam watu, wataalam wa Wizara yangu wawasaidie hao waliovichukua, hasa wale Watanzania wazawa tuweze kuona wanatoa bidhaa tulizotegemea.

Moja ya sababu ni kwamba soko tulilokuwemo lilikuwa linaleta bidhaa ambazo lilikuwa linafanya viwanda vyetu nchini visiwe *competitive* hilo suala ni historia Mheshimiwa Rais na Waziri wa Fedha wamelisulihisha bidhaa zinaingia kwa kulipa kodi na bidhaa *standard*. Kwa hiyo, viwanda vya Watanzania waliopewa vitafanyakazi na hiyo ni kazi yangu tulishughulikie mnisaidie Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana pia kuniruhusu na mimi niulize swali la pili la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri wa viwanda na Biashara amejibu majibu mazuri sana, kwa ujumla lakini ningependa na mimi kujua kwamba suala la viwanda vilivyobinafsishwa limekikumba kiwanda chetu cha Nyuzi cha Tabora. Ningependa Mheshimiwa Waziri aniambie ana mkakati gani hasa wa Kiwanda cha Nyuzi Tabora ambacho kilikuwa kinasaidia wakulima wote wa Pamba katika Kanda ya Ziwa Magharibi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha Nyuzi Tabora mmiliki wa Kiwanda hicho ameshaitika wito kwa Msajili wa Hazina, madai yake yeye anasema nyuzi zake hazina soko.

Kwa hiyo, tunashirikiana naye ili tuweze kupata soko la nyuzi zake lakini tuweze kuona kiwanda kile kinafanya kazi. Nyuzi zake zilikuwa zinakosa soko, mtu anakuambia kiwanda hiki nyuzi hazina soko na hayo niliyowaeleza bidhaa kutoka nje ndiyo mojawapo ya mambo yaliyokuwa yanatuumiza. Kwa hiyo, tuko nae bega kwa bega, wataalam wanafanyia kazi, na nitakuja kuleta mrejesho kwa watu wa Tabora ili kusudi kiwanda chenu kiweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anthony.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa swali la Mheshimiwa Raphael Japhary linafanana na hali ilivyo Moshi Vijijini, kuna kiwanda kilifunguliwa mwaka 1975 na Mwalimu Nyerere na kiwanda kile ni cha ngozi hakikupata mwekezaji mpaka leo, na kimepangishwa kwa shilingi 20,000 kwa mwezi. Naomba Waziri aniambie ni lini atakuwa tayari kwenda kuona hiyo hali nakuchukua hiyo hatua zinazoyostahiki? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antony Komu, Waziri Kivuli wa Viwanda Biashara na Uwekezaji kuhusu kiwanda chake cha mwaka 1975 Moshi ambacho hakukitaja jina. Kwa kweli nitakudanganya nikisema ninakijua kwa sababu hukukitaja jina, niko tayari wewe unipeleke unionyeshe kiwanda tukitafutie majawabu. *(Makofi)*

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mwanza tuna Kiwanda cha *Tanneries* ambacho sasa kimegeuzwa kuwa chuo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukirudisha hicho kiwanda ili kiweze kufanya kazi iliyokusudiwa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mwanza kuhusu kiwanda cha Mwanza *TANNERIES*, ambacho kimegeuzwa kuwa chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu anayeshughulikia Biashara na Uwekezaji Profesa Mkenda, alikuwa Mwanza wiki iliyopita, kile kiwanda kitaendelea kuwa Chuo na tunalenga kuwafundisha wananchi namna ya kutengeneza nguo, ni *Technical School* ni *VETA* ambayo itasaidia watu wa nguo, lakini kando na eneo hilo, kuna Kiwanda cha Ngozi, hicho ndicho tatizo mtu aliyepewa amekigeuza hifadhi ya makatapila na matrekta tunataka kifanyekazi. Kwa hiyo, chuo kitaendelea kufanyakazi tunawafundisha vijana, wanakwenda kwenye viwanda vyao vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni huyo mtu ambaye kiwanda cha Ngozi cha Mwanza amekigeuza hifadhi na kuja Mwanza tarehe 30 na nitakwenda kushughulikia, tarehe 30 mwezi huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, sasa aulize swali lake.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijaruhusu swali langu kujibiwa naomba marekebisho madogo kwenye majina yangu yaliyo kwenye majibu ya Waziri. Jina langu Samson halina (iil kule mwisho na jina langu Bilago halina N katikati halisomeki Bilango linasomeka Bilago.

Na. 46

**Mafao ya Wastaafu**

**MHE. KASUKU S. BILAGO** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wastaafu kutolipwa mafao yao baada ya kustaafu:-

(a) Je, kuanzia Januari hadi Disemba, 2015 ni watumishi wangapi wa umma wamestaafu utumishi?

(b) Je, kati ya hao ni wangapi wamelipwa mafao yao?

(c) Kama kuna ambao hawajalipwa, je, ni kwa sababu gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Idadi ya watumishi wa umma waliostaafu, kati ya Januari, 2015 na Disemba, 2015 ni 7,055

(b) Kati ya watumishi 7,055 waliostaafu, watumishi 5,057 wamelipwa mafao yao.

(c) Jumla ya watumishi waliostaafu 1,998 hawajalipwa mafao yao kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Upungufu wa baadhi ya nyaraka muhimu katika majadala ya wastaafu.

(ii) Waajiri kuchelewa kuwasilisha nyaraka muhimu zinazotakiwa kuthibitisha uhalali wa utumishi wa wahusika kabla ya mfuko kuanzishwa Julai, 1999.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu yaliyotolewa na Wizara ambayo hayakidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wastaafu zaidi ya idadi iliyotolewa na hasa walimu, hata Jimboni kwangu Buyungu idadi kubwa ya walimu waliostaafu inaweza ikaakisi idadi ya watumishi walistaafu katika nchi hii. Sababu zilizotolewa za wastaafu hao kutolipwa moja kubwa ni kukosa fedha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo Serikali haijataja.

Swali la kwanza, naomba Serikali ikiri ni lini italipa wastaafu wote kwa kupeleka fedha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili wasiendelee kuteseka sambamba na kuwarudisha nyumbani kwao mara baada ya kustaafu? *(Makofi)*

Swali la pili, wapo wastaafu wa aina mbili, wapo wanaolipwa pensheni na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na wapo wanaolipwa pensheni na Hazina. Wale wa Mifuko wa Hifadhi ya Jamii wanapata *monthly pension* wale wahazina wanalipwa kwa miezi mitatu *(quaterly pension)* hali hii inawasumbua na kuwatesa wastaafu wetu. Naomba wastaafu wote walipwe *monthly pension* kama ilivyo kwenye mkataba wa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naomba uulize swali, naona unaleta ombi.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Swali la pili dogo, ni lini Serikali itaanza kuwalipa wastaafu wote pensheni ya kila mwezi badala ya miezi mitatu? Ahsante! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumhakikishia *data* nilizompatia ni za kweli na za uhakika, kwa hiyo naomba aamini hao ndiyo wastaafu ambao tunajua wamestaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili sababu nilizozitaja ndizo zinazosababisha wastaafu hao wachelewe kulipwa siyo upelekaji wa fedha. Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwenye Mifuko hii ili waweze kulipwa wastaafu hawa na hizi sababu nilizozileta ndizo ambazo tunazifahamu kama Serikali na Mifuko yote imeendelea kupokea fedha kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, wastaafu wanaolipwa Hazina kulipwa kwa miezi mitatu mitatu. Naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba uamuzi wa Serikali kuelekea kulipa miezi mitatu mitatu lilifikiwa baada ya maombi ya wastaafu hawa kuomba walipwe miezi mitatu mitatu. Kama itaonekana sasa wataomba tena walipwe mwezi moja moja, Serikali haioni ugumu wowote kurejea kule tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru!*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nalazimika kusimama kuwakumbusha kwa sababu imekuwa ni kama kawaida kwa Wabunge kusema kwamba majibu ya Mawaziri, aidha hayawaridhishi au ni majibu ambayo hayatoshelezi swali lao.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni tulizo nazo anayetakiwa kusema kama swali haliridhishi, Mbunge labda awasiliane na Kiti hapa ndicho kiseme; kwa sababu Kanuni ya 45 inaagiza hivyo kwamba Spika, ndiye anayetakiwa kuridhishwa na majibu ya swali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba wakati tukitoa majibu tuzingatie hii Kanuni ya 45 na kwa sababu hizi nakala Waheshimiwa Wabunge wote tuligawiwa naomba tuwe tunaangalia kwa makini.

Tunaendelea, swali la nyongeza, Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona, nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastaafu ambao wanapitia Mfuko *PSPF* hivi karibuni Serikali iliongeza kiwango, lakini wastaafu hawa wanakuwa hawalipwi kwa wakati na kwa kiwango ambacho Serikali ilitangaza**.**

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kuwalipa wastaafu hawa kwa kiwango sahihi na kwa wakati muafaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu tatizo hili lilkuwepo *PSPF*, lakini kuanzia Disemba 2015 mpaka leo wastaafu hao wamekuwa wakilipwa pesa zao inavyostahili. Kuanzia Disemba hiyo tumeanza kulipa hao wastaafu shilingi 100,000/= kama ambavyo Serikali iliongeza kiwango hiki kupitia Mfuko wa *PSPF* na *arrears* zao mpaka kufikia mwisho wa mwezi huu wa nne wote watakuwa wamelipwa zile *arrears* za kutoka Julai hadi Disemba.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshmiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa na tabia tata ya kuchukua fedha kwenye Mashirika ya Umma kama *NSSF, LAPF* na Mashirika mengine na kutokuzirudisha kwa wakati, ama kuwekeza katika miradi mfu kama mradi wa *Machinga Complex* na miradi mingine ambayo imekuwa haina tija Serikalini. *(Makofi)*

Ni lini Serikali itakoma mchezo huu wa kuchukua fedha ambazo zinawaathiri wachangiaji? *(Mkaofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imekuwa ikichukua fedha na hii ikifuata taratibu zote na Mifuko hii kuingia katika Mikataba ili Mifuko hii iweze kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itasitisha utaratibu huu, siamini sana kwamba ni sahihi sana Serikali kusitisha, kama Mifuko inaweza kuwekeza na wakaingia katika mikataba ambayo tunaita ni *Win Win Situation* kati ya Serikali na Mifuko naamini ni sehemu nzuri ya uwekezaji kwa mifuko yetu hii. Kwa hiyo, naomba tuendele kufanya hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni sasa aulize swali lake.

Na. 47

**Ukokotoaji wa Kodi katika Forodha**

**MHE. JAMAL KASSIM ALI** aliuliza:-

Je, ni utaratibu gani unaotumika kukokotoa kodi katika forodha zetu zinazopokea bidhaa na vitu mbalimbali vinavyotokea Zanzibar, wakati vitu vilevile vinavyozalishwa Zanzibar ni vilevile vinavyotoka nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini na ukokotoaji wa ushuru au kodi ya bidhaa mbalimbali kutoka nje, ikiwa ni pamoja na bidhaa zinazopitia Zanzibar kuja Bara, unafanywa kwa kutumia mfumo ujulikanao kama *Import Export Commodity Database*. Mfumo huu unatunza kumbukumbu ya bei ya bidhaa mbalimbali zilizoingizwa nchini kutoka nje na kutumiwa na Mamlaka ya Mapato kama kielelezo na rejea wakati wa kufanya tathmini na ukokotoaji wa kodi au ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyaraka za bidhaa zinapowasilishwa *Central Data Processing Office*, ikiwa ni pamoja na bidhaa zinazotoka nje ya nchi kupitia Zanzibar, bei au thamani ya bidhaa husika huingizwa kwenye

mfumo wa *Import Export Commodity Database,* ili kuhakiki uhalali wa bidhaa na bei husika na kukokota kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa mteja. Endapo bei au thamani ya bidhaa iliyopo kwenye nyaraka itakuwa chini ya ile iliyopo kwenye mfumo wa wetu, mfumo utachukua bei iliyopo kwenye *database* na kukokotoa kiwango halali cha kodi. Hata hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na kusafirishwa kuja Tanzania Bara hazilipiwi kodi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, swali la nyongeza.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:

(a) Kwa vile Naibu Waziri ameeleza kwamba kuna *database* maalum ambayo *TRA* wanayo na kule Zanzibar inatumika, je, huu mfumo una tatizo gani, kwa sababu mizigo yote ambayo inapitia Zanzibar kuja Bara asilimia 100 ya mizigo ile inatozwa kodi inapoingia Tanzania Bara, wakati sheria inayotumika ni hiyo moja, na mamlaka ambayo inasimamia kodi na Kamishna ni huyo huyo mmoja?

(b) Mheshimiwa Naibu Waziri, alieleza katika jibu lake kwamba endapo vitu vinatoka Zanzibar kuja Bara wanaagalia tozo la awali ambalo lilitozwa Zanzibar na kuangalia ile tofauti ambayo kwa mujibu wa *database* zao wanam-*charge* yule mtu. Sasa je, kwa mtu ambaye ana *tv* moja anapopita bandarini pale kutokea Zanzibar hana *entry*…

**NAIBU SPIKA:** Naomba uulize swali Mheshimiwa Jamal,

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Ahsante Mheshimiwa NAibu Spika, je, mtu ambaye kwa vitu ambavyo ni *item* moja moja kama *tv*na *redio* anapotoka Zanzibar kuja Bara wanatumia mfumo gani wa kukokotoa hiyo kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEHDA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kodi inazotozwa kwa bidhaa zinazotika Zanzibar kuja huku kwetu, kwanza naomba nisahihishe, mfumo huu wa *Import Export Commodity Database* unaotumika Tanzania Bara kule Zanzibar hautumiki. Ndiyo maana inaonekana kule ambako hawatumii mfumo huu, bidhaa kule tathmini inapofanyika mara nyingi huonekana ipo chini ya thamani ya kiwango ambacho kinatakiwa kulipiwa kodi inapokuja Tanzania Bara.

Hivyo ndiyo maana bidhaa zinazotoka Zanzibar kuja huku zinatozwa tena kodi. Siyo kodi mara mbili lakini ni kuangalia utofauti wa kodi wa thamani, zilizothaminiwa kutoka Zanzibar na ambazo zimethaminiwa huku Tanzania Bara. Hivyo, tunaomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waweze kufanya haraka

kujiunga na mfumo huu, ili kwa pamoja hili tatizo wanalopata wafanyabiashara wetu wasiweze kulipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bidhaa hiyo moja moja, mfumo ni huohuo mmoja, inapofika kama haikuzalishwa Zanzibar, inapofika Forodhani inatakiwa ichajiwe utofauti ule wa kodi ambao utaonekana ilichajiwa Zanzibar na huku Tanzania Bara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Ugonjwa Ulioshambulia Mikorosho**

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA** aliuliza:-

Je Serikali imejipangaje kuwafidia au kuwapa kifuta machozi wananchi wa Kata za Magawa na Msonga katika vijiji vya Makumbaya, Magewa na Msonga ambao mikorosho kwenye mashamba yapatayo ekari 1000 imeangamia kutokana na ugonjwa wa ajabu na kuwaacha wananchi hawana kitu na hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya maeneo wananchi wanaopatwa na majanga kama haya wamekuwa wakilipwa fidia au hata kifuta machozi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, KILIMO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niamba ya Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida Serikali haina utaratibu wa kulipa fidia ya athari za maafa, ila ina wajibu wa kuwahudumia wananchi wake wanapokumbwa na majanga. Wizara yangu ilipata taarifa za kuwepo kwa ugonjwa huo na kuelekeza wataalam kufanya utafiti ili kubaini sababu, namna ya kuzui pamoja na tiba. Baada ya utafiti huo, iligundulika kuwa na ugonjwa huo unasababishwa na kuvu *(fungus)* aina ya *Fussarium wilt*. Hivi sasa Taasisi yetu ya Utafiti ya Naliendele inaendelea na majaribio ya viuatilifu vitakavyoweza kutibu ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango uliopo wa kuwasaidia wakulima kama ilivyo utaratibu wa Serikali ni kusambaza miche mipya ya korosho inayohimili ugonjwa katika maeneo yanayoathirika baada ya kupata mahitaji halisi kutoka Halmashauri. Aidha, namshauri Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Mkuranga kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kufanya tathmini ya

kina ili kuona kama athari za ugonjwa huo zina tishio la watu kufa njaa, ili utaratibu wa kuomba chakula cha msaada ufanyike mara moja kuokoa maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, taarifa za tahadhari zimeanza kutolewa kupitia vyombo vya habari kwa wakulima ambapo pamoja na mambo mengine, wakulima wameaswa kuteketeza mikorosho iliyoathirika na ugonjwa huo na kuepuka kuhamasisha udongo kutoka kwenye naeneo yaliyoathirika kwenda kwenye maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Hamis, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH HAMISI ULEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu haya mazuri ya Serikali naomba sasa niulize majibu ya maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kwenda Jimboni Mkuranga katika vijiji hivi vya Magawa, Msonga Makumbeya na vinginevyo pata athari hii ili aweze kujionea yeye mwenyewe na kuona namna iliyobora zaidi ya kutusaidia?

(b) Ningeomba niulize Serikali sasa ipo tayari kuhakikisha kwamba viuatilifu kwa maana ya *sulfur,* iweze kupatikana kwa wingi na kwa wakati katika Jimbo letu la Mkuranga ili kuepusha madhara haya ya ugonjwa wa mikorosho na kuhakikisha uzalishaji mkubwa zaidi ili kuwaondolea wananchi wangu umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lake la kutaka tuongozane naye kwenda Jimboni tumelipokea na ninamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia hili suala tayari tulishapanga kufika Mkuranga na kipindi cha bajeti kitakapoisha mimi binafsi nitaongozana naye kwenda Mkuranga ili kujionea hali halisi na kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kweli kwamba kumekuwepo na changamoto ya upatikanaji wa viwatilifu kwa wakati hasa *sulfur* na huko nyuma tayari kumeshatokea matatizo kwa sababu hiyo, kama nakumbuka mwaka 2011 kulikuwa na changamoto wakatia wa matumizi ya kiatilifu cha aina *eugenol 880,* lakini kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba viwatilivu hivyo na hasa *sulfur* zinapatikana kwa wingi na kwa wakati. Hivyo, ninamuahidi kwamba changamoto hii imeshafanyiwa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalumu. Sasa aombe swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Saddiq.

Na. 49

**Migogoro ya Wakulima na Wafugaji Mkoani Morogoro**

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ (K.n.y. MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA)** aliuliza:-

Amani na utulivu ni muhimu sana katika maisha ya binadamu.

Je, ni lini mgogoro wa wakulima na wafugaji katika Wilaya za Mvomero na Kilosa, Mkoani Morogoro utaisha lini ili wananchi waweze kuishi kwa amani na utulivu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara katika Wilaya za Mvomero na Kilosa ambayo imesababisha uvunjifu wa amani na upotevu wa mali na maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa Mkoa wa Morogoro umechukua hatua mbalimbali ili kutatua migogoro sugu. Hatua hizo ni pamoja na kupima na kuhakiki upya maeneo ya Kijiji cha Mabwegere, Wilaya ya Kilosa na vijiji vinavyozunguka Bonde la Mto Mgongola ikiwemo Kijiji cha Kambala Wilaya ya Mvomero. Kutokana na upimaji upya wa vijiji hivyo, kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi, kazi ya kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi inaendelea. Lengo ni kupima vijiji vyote na kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji ambapo maeneo ya ufugaji yatasajiliwa. Vilevile uongozi wa Mkoa uliunda Kamati ya Usuluhisi wa Mgogoro wa Mabwegere na Kamati hiyo imekamilisha kazi, ripoti iliwasilishwa kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya ardhi ni makubwa katika Mkoa wa Morogoro kutokana na hali ya hewa na rutuba, hali hii ndiyo inasababisha watu kutoka Mikoa mingine kuhamia Mkoa huo kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Kutokana na msukumo wa mahitaji makubwa ya ardhi na kuwepo kwa migogoro Mkoa uliamua kufanya tathmini katika Wilaya ya Mvomero na

kugundua kuwepo kwa mashamba yasiyoendelezwa. Mkoa ulimwomba Mheshimiwa Rais, afute hati za umiliki wa mashamba hayo na hadi sasa mashamba sita yeye jumla ya hekta 1,880.6 yamefutiwa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa una mpango wa kugawa mashamba hayo kwa wakulima na wafugaji ili kupunguza migogoro baina ya jamii hizo. Mashamba hayo hapo katika vijiji vya Wami Luhindo, katika maana ya shamba lililokuwa la Bwana Karim B. Walji lenye hekta 500, shamba la Bwana Lusingo Kibasisi lenye hekta 200, shamba la Bwana Nicolaus Anthony la hekta 52.3, shamba la Joseph R. Hall lenye hekta 166 na shamba la *D. H. Kato Farms* lenye hekta 247. Vilevile katika kijiji cha Nguru ya Ndege ambapo kuna shamba la Badrun na Karim Dharamishi lenye hekta 392.6 na katika Kijiji cha *Wami Valley* ambapo kuna shamba la Emmanuel J. Gereta lenye hekta 545.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Ni kweli kuna juhudi mbalimbali zinazoendelea kufanyika katika Wilaya ya Mvomero kuondoa tatizo la wakulima na wafugaji, na kwa kweli Serikali imefanya kazi kubwa kupitia Waziri Lukuvi, Mheshimiwa Simbachawene pamoja na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, tunawashukuru Mawaziri hawa, wamefanya ziara mbalimbali. *(Makofi)*

Swali la kwanza, kwa kuwa juhudi ambazo tunaendelea kuzifanya kama Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero zinahitaji bajeti, na kwa kuwa tayari Mawaziri hawa tumeshawapa bajeti zetu ili tuondoe mgogoro huu na wakulima na wafugaji wawe na maeneo yao. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ambazo tuliziomba na fedha zile ziko kwenye bajeti?

Swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna mashamba sita yamerudishwa, na mashamba mengine zaidi ya 29 bado hayajarudishwa.

Je, lini Waziri mhusika pamoja na Mheshimiwa Rais, watayafuta yale mashamba yaliyobaki ili tuwagawie wananchi maeneo ya wakulima na wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la bajeti, Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwenye bajeti yake imetenga fedha pamoja na mambo mengine kwa

ajili ya matumizi bora ya ardhi, vilevile kwa ajili ya kuweka miundombinu ya huduma za mifugo, kwa ajili ya Wilaya ya Mvomero.

Kuhusu swali la pili, tayari mashamba mengine yameshapelekwa Wizara ya Ardhi ili yaweze kufutiwa hati. Wilayani Kilosa mashamba 73 yenye ukubwa wa ekari 429,625.3 tayari yameshabainishwa na kupelekwa ili yaweze kufutwa. Vilevile Wilayani Mvomero mashamba 84 yenye ukubwa wa ekari 119,382.6 nayo yameshapelekwa Wizara ya Ardhi ili kufanyiwa kazi. Lengo ni kwamba haya mashamba yote yakiweza kufutiwa hati baada ya hapo utaratibu utakaofuata ni kuwagawia Wafugaji na Wakulima ili kuweza kuondoa tatizo kubwa lililopo la ardhi na hatimaye kupunguza migogoro hiyo ya ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Hitaji la Nyumba kwa Askari wa JWTZ**

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA** aliuliza:-

Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ) limekuwa tegemeo kwa nchi hususan katika masuala ya kiulinzi nchini:-

Je, ni lini Serikali itawapatia nyumba bora za makazi askari wa Jeshi hilo, hasa ikizingatiwa nyumba zilizopo hazitoshi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia ya kuliboresha Jeshi kwa vifaa, zana na miundombinu ikiwa ni pamoja na nyumba za makazi ya wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imechukua hatua ya kupunguza mahitaji makubwa ya nyumba kwa wanajeshi kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000.

Awamu ya kwanza ambayo utekelezaji wake umeshaanza, zinajengwa nyumba 6,064 katika kambi mbalimbali nchini. Katika awamu ya pili tunatarajia kujenga nyumba 3,034 kwa ajili ya askari wa ngazi ya kati na Maafisa. Pamoja na mradi huu, Serikali itaendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa nyumba zilizopo ili kupunguza uhaba wa makazi kwa wanajeshi.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri nina swali moja la nyongeza.

Je, nyumba hizo zilizojengwa ziko wapi na Mkoa gani unaendelea kujengwa hizo nyumba? Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba hizi ziko katika Mikoa mingi ya nchi yetu, kwa upande wa Zanzibar, nyumba wameanza kujenga upande wa Pemba, bado Unguja wataingia katika awamu ya pili. Kwa hiyo, orodha ya Mikoa ni mingi siwezi kuorodhesha yote hapa, lakini nitakuwa tayari kumpatia Mheshimiwa Mbunge kwa maandishi endapo atahitaji.

**NAIBU SPIKA:** Tuendelee Waheshimiwa Wabunge, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Kauli za Mawaziri.

## KAULI ZA MAWAZIRI

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa kauli ya Serikali kuhusu Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini, tarehe 20 Aprili wakati tunamaliza kipindi cha asubuhi, cha Kikao cha Pili cha Mkutano wa Tatu wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Mheshimiwa Juma Nkamia, Mbunge, ulifuatia jibu la ziada nililotoa kwa jibu lililotolewa na Mheshimiwa William Tate Olenasha Mbunge, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki Mbunge kutokana na jibu la msingi Na. 17. Aidha, katika Mwongozo huo Mheshimiwa Mbunge alihoji maelezo ya mradi wa muihogo niliyotolea mfano wakati nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hassan Masala kufuatia swali la msingi Na.19 la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Nkamia alitaka kujua kama ujenzi wa uchumi wa viwanda unaendana na ushushaji wa bei ya mazao ya wakulima na kama hiyo kauli ilikuwa ya Charles Mwijage binafsi au ni kauli rasmi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama Taifa tumeamua kujenga uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Tunajenga viwanda ili tuzalishe bidhaa zenye ubora tukilenga mahitaji ya soko la ndani na soko la nje. Viwanda tulivyonavyo na vingi vitakavyojengwa vinalenga kutumia malighafi ambazo zinapatikana nchini kwetu kwa wingi hususani sekta ya kilimo kwa ujumla wake.

Tanzania ni sehemu ya soko kubwa la dunia, wakati viwanda vyetu vinazalisha bidhaa kwa ajili ya masoko ya nje na Mataifa mengine viwanda vyao navyo vinazalisha kwa ajili ya masoko mengine ikiwemo nchi yetu. Hali hii ambayo hatuwezi kuiepuka inaviweka viwanda vyetu katika ushindani wa Kimataifa, zipo njia mbili kuu za kuweza kuhimili hali hii na kujenga sekta ya viwanda endelevu.

Moja, ni kulenga maeneo ambayo shughuli nzima ya viwanda tuna faida ya kiulinganisho dhidi ya washindani wetu *(comparative advantage),* na pili ni kuendesha shughuli ya viwanda kwa tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwekeza kwenye maeneo ambayo tuna faida ya kiulinganisho, tumeandaa orodha ya viwanda ambayo tutaelekeza nguvu zetu. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kuendesha shughuli ya viwanda kwa tija mkakati wa ujenzi wa viwanda unahimiza ufanisi na tija katika pingili za mnyororo wa uongezaji thamani ya bidhaa yoyote kuanzia malighafi, usindikaji bidhaa mpaka inapofikia mikononi mwa mlaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali nimeeleza kuwa viwanda vyetu vingi vitatumia mazao ya kilimo, mifugo au uvuvi kwa malighafi yake. Hivyo basi, kuweza kuzalisha bidhaa inayohimili ushindani ni lazima malighafi inayotumika izalishwe kwa tija kubwa. Malighafi iliyozalishwa kwa tija humpatia mzalishaji, mkulima kipato kikubwa, ina ubora wa hali ya juu na huwa ya gharama nafuu kwa mwenye kiwanda. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ambavyo vinategemea malighafi kutoka sekta ya kilimo unakwenda pamoja na mageuzi katika sekta ya kilimo. Mageuzi katika sekta ya kilimo ni pamoja na kulima au kufuga kwa tija, mkulima aneyelima kwa kuzingatia tija anapata mavuno mengi kwa eneo dogo hali inayomuwezesha kupunguza bei anapokabiliwa na ushindani na bado akapata pato linalomuwezesha kurejesha gharama alizowekeza na faida ya kuendesha maisha na shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfano wa zao la muhogo lililomsukuma Mheshimiwa Juma Nkamia kuomba mwongozo, dhana ya tija inajieleza vizuri. Bei ya tani moja ya muhogo ni dola za Kimarekani ni 150 sawa na shilingi 330 kwa kilo. Kwa mtazamo wa kawaida kiasi hiki ni kidogo na kinampunja mkulima, lakini andiko la mradi linaeleza kuwa kwa sasa Tanzania tunapata wastani wa tani tatu kwa hekari za muhogo, wakati mradi utaboresha kilimo chetu tupate wastani wa tani 30 kwa hekari. Kwa bei ya shilingi 330,000 kwa tani mkulima

atapata shilingi 990,000 kwa kilimo cha sasa, wakati ukulima unaolenga tija utampatika milioni 9.9 hata kama ukulima wa kisasa utagharimu asilimia 60 ya pato hilo anabakiza kiasi kingi cha fedha. Hoja hapa ni kuwa inapotokea ushindani mkulima anaweza kupunguza bei na akabaki na faida nzuri tu, lakini upande wa kiwanda kitakachopokea muhogo huo kwa bei nafuu bidhaa ya mwisho itakayozalishwa itakuwa shindani sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa muhogo tunalenga uanzie Mkoa wa Lindi na kiwanda kitajengwa huko. Tunayo *order* tayari ya tani milioni mbili kwa bei ya dola za Kimarekani 150 kwa tani, biashara inayolenga kupatia Taifa pato la dola milioni 300 ikilinganishwa na pato la kahawa dola za kimarekani 171,121,500 kwa miaka ya 2013 na 2014 mtawalia. Nchi ya Nigeria inauza tani arobaini na nne milioni kwa mwaka na mmoja wa wakulima wakubwa wa muhogo katika nchi hiyo ya Nigeria ni Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki katika swali lake Na. 16 linatambua kabisa umuhimu wa ufugaji wa tija na ndiyo maana anahimiza Serikali iwawezeshe wakulima na wafugaji kupata mitamba inayotoa maziwa mengi. Jibu langu la ziada na maelezo ninayaongezea sasa ni kuwa badala ya kuweka bei elekezi itakayoweka bei ya maziwa kwa lita isiyoshuka au kupanda, sekta ya maziwa itaendeshwa kwa tija. Uendeshaji wa sekta ya maziwa kwa tija ni pamoja na kuwa na ng'ombe wa maziwa wanaokamuliwa maziwa mengi, malisho bora, mtandao wa kukusanya na kusindika maziwa. Ng'ombe anayefugwa kisasa na kukamuliwa lita 30 na mfugaji akapata uhakikia wa soko hata lita moja ikiuzwa shilingi 700 yupo vizuri kuliko mfugaji ambaye ng'ombe wake anakamuliwa lita tatu kwa siku hata kama lita moja itauzwa kwa shilingi 1,000. Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda maziwa na bidhaa za maziwa ni eneo ambalo nitalishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujenga sekta ya viwanda endelevu ni muhimu kuzingatia nguvu ya ushindani pamoja na vigezo vingine kama nilivyotoa mifano hapo juu uendeshaji wa shughuli kwa tija ni moja ya mbinu za kuhimili ushindani na katika uzalishaji wenye tija katika mzingira ya ushindani bei kubwa siyo hoja. Katika mazingira ya ushindani bei kubwa siyo hoja, hoja ni pato apatalo mzalishaji *(the profitability),* awe ni mkulima azalishae malighafi au kiwanda kinachosindika malighafi na kutoa bidhaa ya mwisho. Bei ya malighafi au bidhaa kutoka katika soko huru inaamuliwa na nguvu za soko siyo Serikali na Tanzania kwa bidhaa zilizo nyingi bei inaamuliwa na nguvu za soko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu matangazo.

Tangazo nililonalo hapa ni la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, mgeni wa kwanza ni Profesa Mussa Juma Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali ambaye ameambatana na Manaibu wake watano pamoja na Maafisa wengine kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, karibuni sana.

Wageni wengine wapo jukwaa la wageni hawa ni wageni wa Mheshimiwa Khalifan Hilaly Aeshi, Mbunge wa Sumbawanga Mjini ambao ni Ndugu Justin Emmanuel ambaye ni Meya wa Manispaa ya Sumbawanga. Sasa huyu kwa sababu ni Meya nadhani anaitwa Mstahiki. Kwa hiyo Mstahiki Meya Jastin Emmanuel, mgeni mwingine ni Isdor Munisi ambaye na yeye anatoka Manispaa ya Sumbawanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Mbunge wa Jimbo la Nzega ambao ni Ndugu Amos Kanuda, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Nzega na mwingine ni Ndugu Makuya Hetmas, Katibu wa CCM Wilaya ya Nzega, na hawa wameambatana na wageni wengine ambao ni Ndugu Peter Samson na Paulo Samweli.

Wageni wengine ni wageni 39 wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, wakiongozwa na Ndugu Murida Mshoto ambaye ni Mwenyekiti wa Wafugaji Kanda ya Ziwa na Ndugu Fyeka Sumera, Diwani wa Nyamswa huyu ni Mheshimiwa na mwingine ni Mheshimiwa Josephat Makina, Diwani wa Unyali na mwingine ni Ndugu Mabagida Gesura aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Katiba, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa January Makamba ana wageni wawili ambao ni Ndugu Zainab A. Issa, Mwenyekiti wa Shirikisho la CCM Vyuo vya Elimu ya Juu Taifa na mgeni mwingine ni Ndugu Luhende Luhebe, Mchumi wa Shirikisho la CCM vyuo vya Elimu ya Juu Taifa. Pia Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia Mbunge wa Jimbo la Kinondoni ana mgeni ambaye anaitwa Ezekiel Mwakigenda ambaye ni mjasiriamali kutoka Jimbo la Kinondoni.

Kuna wageni ambao wapo Bungeni kwaajili ya mafunzo kundi la kwanza ni wageni 67 wa Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro, karibuni sana.

Kundi lingine ni la wanafunzi 42 kutoka Chuo Kikuu cha Iringa Kitivo cha Sheria, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu ya kuhusu wageni, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha, 2016/2017.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa, tutaanza na Mheshimiwa Ikupa Alex ili aweze kuchangia Mheshimiwa Ikupa karibu.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, ninaomba tena nitumie Kanuni Na. 60 (11) nichangie nikiwa nimekaa.

**NAIBU SPIKA:** Tafadhali endelea,

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, moja kwa moja nitaenda kwenye pongezi, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa utendaji wake mahiri, chini ya Rais wetu mpendwa John Joseph Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyofanyika ni mengi siwezi kueleza moja moja, pia ninapenda nimshukuru Rais wetu kwa kusikia kilio cha watu wenye ulemavu kwa kutuhamishia Ofisi ya Waziri Mkuu, kilikuwa ni kilio chetu cha muda mrefu, tunashukuru kwamba alisikia ombi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijikite moja kwa moja kwenye masuala ya watu wenye ulemavu kwa sababu mengi yemeongelewa mambo ya maji watu wanaongelea, barabara, umeme na kadhalika.

Moja kwa moja ninaomba niongelee suala la elimu kwa watu wenye ulemavu. Katika sehemu hii ya elimu ninaiomba Serikali iangalie ni kwa jinsi gani ambavyo inaweza ikawasaidia watu wenye ulemavu hasa katika suala zima la kuongeza shule ambazo ni maalum na ambazo watu wenye ulemavu wanaweza wakapata elimu pasipo kipingamizi chochote. Ukiangalia suala zima la kusema kwamba majengo yaongezwe inaweza ikawa ni ngumu, lakini naiomba Serikali iboreshe majengo yaliyopo kwa upande wa miundombinu pamoja na walimu ili watu wenye ulemavu waweze kupata elimu pasipo vikwazo vyovyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninaomba nizungumzie suala la mikopo kwa watu wenye ulemavu vyuoni. Mimi pendekeza kwa Serikali kwamba kusiwe kuna vipingamizi kwa mtu mwenye ulemavu kupata mkopo ambaye tayari amechaguliwa na chuo fulani kujiunga hapo. Ninaomba sana

Serikali iliangalie hili suala la mikopo ili kusiwe kunakuwa kuna vikwazo kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba niongelee suala la ajira. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 18 ameongelea suala la ajira lakini ametoa takwimu za vijana. Katika sehemu hii haioneshi kwamba Serikali inatekeleza vipi ile Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 kwa upande wa ajira kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iangalie ni kwa jinsi gani ambavyo Sheria hii ya mwaka 2010 inatekelezwa hasa katika suala zima la ile asilimia tatu kwamba kila mwajiri awe na asilimia tatu ya watu wenye ulemavu katika wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba niongelee suala la mauaji kwa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi. Suala hili kwanza napenda niishukuru Serikali na kuipongeza kwa jinsi ambavyo mauaji haya yamepungua kwa kiasi kikubwa, lakini bado kuna taarifa ambazo zinaendele kuripotiwa za kupotea kimya kimya kwa hawa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi. Ninaiomba Serikali pamoja na ulinzi ambao inatupatia, pia ijikite katika suala nzima la elimu kwa jamii yetu. Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yao wanapopata fursa ya kukaa na wapiga kura wao watoe elimu hii kwa jamii kuhusiana na suala zima la mauaji kwa watu wenye *albinism.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee suala la kodi kwenye mishahara ya waajiriwa ambao wana ulemavu. Tumeona kwamba mishahara ya waajiriwa wenye ulemavu imekuwa ikikatwa kodi ninaiomba Serikali iondoe suala zima la kodi kwenye mishahara ya watu wenye ulemavu. Kama tunavyofahamu kwamba ulemavu ni kikwazo, sasa unapokata tena ile kodi ina maana kwamba unampunguzia huyu mtu uwezo wa hata kumwezesha kumpa posho mtu ambaye ni msaidizi wake. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iondoe kodi kabisa kwenye mishahara ya waajiriwa ambao ni walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala zima la vyombo vya usafiri ambavyo vinaagizwa na watu wenye ulemavu. Kumekuwa kuna sheria kwamba ili mlemavu asamehewe kodi ya chombo alichokiagiza ni mpaka kile chombo kiwe kina vifaa maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Binafsi ni mlemavu, lakini mimi huwa naweza kuendesha gari yoyote ambayo ni *automatic,* kwa hiyo, ninaomba sheria hii irekebishwe mradi tu kwamba mtu aliyeagiza kile chombo ni mlemavu basi ile kodi asamehewe siyo mpaka kile chombo kiwe na vifaa maalum kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la malipo ya *road license* kwa vyombo vya watu wenye ulemavu. Naomba Serikali itusamehe kodi hii ya

barabara katika vyombo ambavyo tunavitumia sisi watu wenye ulemavu, kwa sababu hili suala lipo ndani ya uwezo wa Serikali ninaamini kabisa kwamba inaweza ikaondolewa na vyombo hivi tukawa hatulipi hii *road license* badala yake tukawa tunalipa tu *insurance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu. Mfuko huu ninajua kwamba upo na ulishaanzishwa, ninaiomba Serikali kama vile ambavyo imekuwa ikitenga pesa kwa ajili ya barabara, pesa kwa ajili ya umeme, pia Serikali itutengee fungu maalumu kwenye huu mfuko ili huu mfuko uweze kutusaidia sisi watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie suala zima la Halmashauri na Manispaa hasa kwa wale watu wenye ulemavu ambao hawana kipato chao kujitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili Wakurugenzi wa Halmashauri na Manispaa wafanye utambuzi wa watu wenye ulemavu ambao hawajiwezi na baada ya kufanya utambuzi huu waweze kuwapatia zile shughuli ambazo zinapatikana kwenye Halmashauri zao ikiwemo shughuli mbalimbali kama kuzoa takataka, vyoo vya *city,* hili limefanyika katika Halmashauri ya Ilala kuna choo kimoja ambacho walitengewa watu wenye ulemavu, kwa hiyo hawa watu wenye ulemavu ambao walikuwa wanaomba barabarani, walikuwa wanapita pale kila asubuhi mtu anachukua shilingi 1,000 kwa sababu kile choo kilikuwa kina uwezo wa kupata shilingi 250,000 kwa siku, hivyo ilipunguza kwa kiasi kikubwa wimbi la ombaomba wenye ulemavu katika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri kuna ile asilimia ambayo inawataja wanawake na vijana tu, nilikuwa ninaomba asilimia hii iweze pia kuwataja na watu wenye ulemavu ili weweze kunufaika isiwe *general,* iwataje na wao kama vile ambavyo inataja vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninaunga mkono bajeti hii ambayo ipo mbele yetu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Hamid Aweso halafu Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ajiandae, Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaipongeza hotuba nzuri ya Waziri Mkuu, lakini nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

nimpongeze Waziri Mkuu na nipongeze Baraza zima la Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya, kazi yao inatutia moyo sana na inafanya sisi kama wana CCM tutembee kifua mbele. Tunawapongeza sana, tunaomba muendelee kufanya kazi kwa juhudi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kuchangia kuhusu mambo ya Tabora. Naomba nianze na suala zima la tumbaku, maana tumbaku ndiyo Tabora, bila tumbaku Tabora haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao hili la tumbaku limekuwa ni zao linalochangia kodi kubwa, pato kubwa la Taifa, lakini wakulima wa tumbaku wanatozwa tozo 19 za tumbaku, hili suala linadhoofisha sana wakulima wa tumbaku. Mkulima wa tumbaku ukimkuta leo hana maendeleo yoyote, tozo ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali yangu, ninamuomba Waziri Mkuu na Serikali ya Awamu ya Tano, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu mziangalie hizi tozo, muweke mkakati maalum wa kupambana na hizi tozo kuzipunguza ili wakulima wa tumbaku waweze kufaidika na kilimo wanacholima, najua Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya kusaidia wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora tunalima tumbaku kwa asilimia 60 lakini huwezi kuamini hatuna kiwanda cha ku-*process* tumbaku, hatuna kiwanda cha kutengeneza sigara, inaumiza sana nasema kwa uchungu mkubwa, juzi amekuja mwekezaji wa kujenga kiwanda cha sigara, kiwanda hicho kimewekwa Morogoro, Morogoro hawalimi tumbaku, ajira zetu watapata watu wa Morogoro kule sisi tunaumia, miti inakwisha, watu wetu wanakonda na moto wa tumbaku, hatuna faida yoyote na hiyo tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ya Awamu ya Tano iliangalie hili suala kwa makini sana, ninamuomba Waziri Mwijage ninamuamini, ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi. Tumehangaika naye kutafuta mwekezaji wa tumbaku mara nyingi, lakini Mheshimiwa Waziri Mwijage nikuombe sana hata kama tumekosa kiwanda cha sigara atusaidie tupate hata kiwanda cha ku-*process* tumbaku hali ya Tabora kwa kweli siyo nzuri, hatuna kiwanda chochote, ajira ni shida. Ninaiomba sana Serikali ya Awamu ya Tano itusaidie, ituonee huruma, tumbaku yote inapatikana Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumbaku imeliingizia Taifa dola milioni 3 lakini pia inachagia pato la Taifa asilimia 27 ya *GDP* ya Taifa. Kwa hiyo, tunaomba sana mtuangalie watu wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu suala la hospitali, Tabora Manispaa hatuna hospitali ya Wilaya, tumeliweka hili suala kwenye bajeti toka 2012, tumepata shilingi 150,000,000 tumeanza, lakini tunaiomba Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu iangalie jinsi ya kutuwekea hospitali ya Wilaya, pale ni Makao Makuu ya Mkoa *population* ni kubwa sana, mtu akiumwa malaria moja anaenda hospitali ya Mkoa, msongamano unakuwa mkubwa, matokeo yake tunawalaumu madaktari kila siku lakini kwa kweli msongamano ni mkubwa sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Uyui ambayo iko Tabora Manispaa haina hospitali ya Wilaya, ninaiomba Tabora Manispaa na Uyui tupate pesa za kuweka hospitali za Wilaya ili kupunguza *population* kubwa ya wagonjwa kwenye hospitali ya Mkoa wa Tabora. Leo siongelei Madaktari Bingwa, Mheshimiwa Ummy aliwahi kuniahidi hapa kwamba analishughulikia suala la Madaktari Bingwa na ninamwamini sana Mheshimiwa Ummy, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kazi anazozifanya ninaamini atatuletea Madaktari Bingwa ndani ya Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu kupata Mkoa mpya wa Tabora. Katika Mikoa mikongwe ya nchi hii, Mikoa ya kwanza toka tunapata uhuru ni Mkoa wa Tabora. Kwa kweli Mkoa ule umepanuka jiografia yake ni kubwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi Tabora, anaijua kabisa jiografia ya Mkoa wa Tabora, tunaomba atusaidie kuugawa huu Mkoa, *RCC* imeshakaa zaidi ya mara tatu, mara nne tukitoa mapendekezo ya kuugawa Mkoa wa Tabora, tunaomba atusaidie sana, tupate Mkoa wa Tabora na Mkoa mpya wa Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Manispaa lina *population* kubwa sana, lina Kata zaidi ya 30 watu ni wengi sana, leo ukiangalia watu wa Jimbo la Pangani ni kama watu 45,000 tu, lakini angalia watu wa Jimbo la Tabora Manisipaa, tuko kwenye 300,000 na kidogo uwajibikaji unakuwa mgumu, kuwafikia wananchi inakuwa kazi sana. Ninamwomba Waziri Simbachawene ni lini sasa atagawa hii Wilaya ya Tabora Manispaa na kuwa Majimbo mawili. Tunamwomba sana atusaidie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wilaya ya Uyui tuliomba Halmashauri ya Wilaya ya Mji Mdogo muda mrefu, tunaiomba Serikali ikija ku-*wind up* ije na majibu kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu milioni 50 ya kila Kijiji na kila Mtaa. Kwanza nianze kwa kukipogenza Chama changu cha Mapinduzi, viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuweka kwenye Ilani yao ya Chama cha Mapinduzi, kwamba kila Mtaa watu wapate milioni 50 na Kijiji ili kusaidia watu wanyonge, watu wa chini, vijana na sisi kina mama. Niwapongeza sana

Chama cha Mapinduzi na niseme hiki ni kitu kikubwa sana walichofanya *it is not a joke*. Kwa hiyo, mimi nawambie tu wale wanaosubiri kukitoa hiki chama madarakini watasubili sana! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Watasubiri sana hiki chama kutoka madarakani siyo rahisi, jambo hili ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Sikudhani kabisa kwamba bajeti hii ya mara ya kwanza Rais Magufuli na Serikali yake watakuja na mpango wa hizi milioni 50, nilijua wana mambo mengi, wana elimu bure, wana elimu bure kwa vyuo, mimi ninaiita elimu bure kwa vyuo kwa sababu *revolving* ya vyuo vikuu hatuanza kuiona, pesa zinazoenda kukopesha watoto wetu wa vyuo mimi niseme ni bure tu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu kwa kuanzisha bajeti yao ya kwanza tu kuweka hizi milioni 50. Mimi nilikuwa nadhania kwamba shilingi milioni 50 labda zitakuja 2018, niliwahi kwenda Tabora kwenye kikao cha akina mama wakaniuliza, nikasema jamani tumeingia juzi tu madarakani hebu tumpe Rais na Waziri Mkuu nafasi ya kufanya kazi. Mimi nilidhani labda itakuwa bajeti ya 2017 au 2018 lakini kwa mshangao mkubwa wameleta bajeti hii 2016 *big up* sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Hupati Uwaziri wewe.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuipongeza Serikali yangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde samahani kidogo. Mheshimiwa Lijualikali hii tabia yako siyo nzuri ya kuongea kwenye *microphone* wakati mtu mwingine anachangia. Endelea Mheshimiwa Munde. *(Makofi)*

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii imekuwa ikituahidi toka 2011 kutuletea maji ya Ziwa Victoria na leo hii nimesoma kwenye randama kuna maji ya Ziwa Victoria yanaonekana lakini sijaona pesa za maji ya Ziwa Victoria. Ninaiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ikija hapa Wizara ya Maji ituambie imetutengea shilingi ngapi kwa ajili ya Ziwa Victoria na mkandarasi anaanza lini kazi ili tuweze kumjua ni mkandarasi yupi na yupi, tunaiomba sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali hii, imeleta nidhani kubwa kwenye ofisi za Serikali, imeinua ari ya Watanzania na ari ya wafanyakazi. Leo hii mtu akienda Polisi anahudumiwa, mtu akienda ofisi ya Serikali anahudumiwa, mtu akienda hospitali anahudumiwa, yote hii ni juhudi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wako endeleeni kufanya kazi, tuko nyuma yenu tunawapongeza, tunawaunga mkono na tunawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vyama vya siasa haviwezi kutumbuliwa majipu! Naomba niulize kwa sababu kuna vyama hapa ni *SACCOS,* kuna vyama ni *NGO's* kuna vyama vinapata hati chafu. Hivi vyama mwanachama wa chama hicho akiuliza anaitwa msaliti, anafukuzwa. Lakini nimeona Chama cha Mapinduzi kwenye Ilani yake kimeweka milioni 50 kila Mtaa, lakini kuna watu wanaruzuku za Wabunge wao hawajawahi kuweka kwenye Ilani yao hata madawati kumi kila Wilaya. Leo hii wanakuja hapa wanalaumu na kusema kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haifai. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafaa na inawaona wananchi wake.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde kuna Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwanza nimwambie Mheshimiwa Munde, Chama cha Mapinduzi siyo ambacho kinatoa milioni 50 bali ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba nimpe hiyo taarifa kwamba, fedha za walipa kodi ndiyo zinaenda kutoa milioni 50 kila Mtaa na siyo Chama cha Mapinduzi na vile vile na hati chafu na ubadhilifu na ufisadi wa Chama cha Mapinduzi kinaongoza. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu mchangiaji anayechangia Chama chake kimemzuia kuchangia kwa hiyo, ahesabiwe amechangia au anataka kutuambia nini? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde naomba uendelee je, Taarifa unaipokea?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unitunzie dakika zangu siwezi kuipokea hiyo taarifa kwa sababu haina msingi wowote. Serikali hii ni ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi ndiyo kimeweka kwenye Ilani yake mambo yote haya yanayoendelea kufanyika, wao kwenye Ilani yao na wao wanapata pesa za walipa kodi za ruzuku wameweka nini kwa ajili ya wananchi wa Watanzania? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wao katika pesa za ruzuku ambazo ni za walipa kodi wamefanyia nini wananchi wa Tanzania, hawajawahi hata kujenga choo cha shule kwa ajili ya hela ya ruzuku ya walipa kodi. Pesa hizo wanageuza ni *NGOs* zao ni *SACCOS* zao kwa manufaa yao wao binafsi na familia zao, tunataka sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sisi ndiyo Wabunge tunatunga sheria, tutunge sheria Waziri Mkuu akatumbue majipu kwenye vyama vya siasa, hivi Vyama siyo kwa ajili ya *NGOs.* Ahsante sana, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali naomba ukae, Taarifa lazima mtu awe anachangia ndiyo unampa Taarifa sasa hivi hamna aliyeanza kuchangia. Naomba uendelee Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. AMINA S. MOLEL:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina kwa sababu kuna Mheshimiwa amesimama pale huwezi kutoa mwongozo, Mheshimiwa Aweso endelea. *(Makofi)*

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii adhimu na mimi nichangie hotuba ya Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu. Pia naomba niipongeze Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayoifanya. Lakini pia nimpongeze Dkt. John Pombe Magufuli ni jembe, tena ni jembe la palizi ambalo limekuja kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. Pia nimpongeze pia Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya, najua zipo changamoto nyingi lakini nasema bahari kubwa ndiyo ivukwayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika suala zima la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Pamoja na mafanikio ya kukuza uchumi katika Taifa letu, pia kuna changamoto kubwa ya umaskini wa watu wetu, ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba inatengeneza mazingira ya uwezeshaji

wananchi kiuchumi ili kuhakikisha kwamba inawasaidia katika kuepukana na umaskini uliokithiri katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imeahidi katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kutenga shilingi milioni 50 katika kila kijiji, hii itakuwa ni *solution* ya kuwasaidia Watanzania kwa sababu wapo mama lishe, wapo wajasiriamali wadogo wadogo wakiwemo bodaboda, kilio chao kikubwa ni mitaji, leo ukitaka mtaji unawaambiwa upeleke hati ya nyumba, kiwanja huna hiyo hati utaitoa wapi! Naamini kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya shilingi milioni 50 katika kila kijiji itasaidia sana Watanzania na wananchi wa Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa nilizungumzie ni suala zima la kilimo. Watanzania wanategemea sekta ya kilimo, lakini kilimo kilichopo sasa, ukuaji wake ni wa kusuasua na kutegemea kudra za Mwenyezi Mungu. Ninaiomba Wizara ya Kilimo ihakikishe kwamba inajikita katika sekta ya kilimo cha umwagiliaji kwa sababu nchi yetu Mwenyezi Mungu ameijaalia, kuna mito na maziwa mengi tukijikita katika kilimo cha umwagiliaji nadhani suala la chakula kwetu litaisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wetu wa Pangani tumejaaliwa kuwa na Mto wa Pangani ambao unamwaga maji baharini, ninamwomba kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ahakikishe kwamba anatutengenezea *scheme* ya umwagiliaji ili kuhakikisha kwamba jamii yetu ya Pangani tunajikita katika kilimo cha umwagiliaji ambacho kitakuwa katika mazao ya mbogamboga ambayo itaweza kulisha Wilaya ya Pangani na Mkoa wa Tanga pia tunachangia Pato la Taifa katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni suala zima la miundombinu ya barabara. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara ni kichocheo cha maendeleo katika jamii yoyote. Lakini katika Wilaya yetu ya Pangani, barabara yetu imekuwa ni ahadi ya muda mrefu lakini mpaka sasa barabara hii imeweza kuzorotesha maendeleo katika jamii yetu ya Pangani. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ya Awamu ya Tano iangalie kwa jicho la huruma kuhakikisha kwamba inajenga barabara hii ya Pangani, Tanga - Pangani - Sadani ili kuweza kuinua uchumi wa Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Wilaya ya Pangani ilivyo ni kama kisiwa, ili uende Pangani lazima uende kwa makusudio maalum, unaenda kuzika au umesikia kuna *kitchen party* ndiyo watu waweze kwenda, madhara ya barabara hii ni makubwa, ingawa tumekuwa na fursa nyingi ya kiutalii, tuna uvuvi bahari kuanzia mwanzo wa mji mpaka mwisho wa mji. Ninaiomba Serikali itengeneze barabara hii ya Pangani ili kuhakikisha kwamba uchumi wa Pangani

unapaa, badala ya kuwa pangoni, sasa tupae angani. Ninaamini Serikali hii kwa kazi inayofanya barabara hii itatengenezewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ni sekta ya uvuvi. Jamii yetu ya Pangani tunategemea sekta ya uvuvi, Lakini uvuvi tunaoufanya ni wa kutumia zana duni na ukitaka kwenda kuvua lazima utegemee ndoano na chambo; hivi samaki akishiba huyo samaki utamvua wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Uvuvi iangalie sasa suala la uvuvi ili kuhakikisha kwamba inawasaidia wavuvi wa Pangani kwa kuwapatia pembejeo na zana na kuhakikisha tunatengenezewa bandari ya uvuvi kwa ukanda wa Pangani na Tanga ili kuhakikisha kwamba wavuvi wa Pangani wanafaidika ni rasilimali bahari tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nizungumzie ni suala la afya. Huduma ya afya bora ni njia nzuri ya kuinua uchumi katika jamii yoyote, lakini katika sera ya Serikali inasema kwamba itajenga zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila Kata, lakini Pangani tuna kituo kimoja tu cha afya na asilimia kubwa ya wananchi wanakaa ng'ambo ya Mto Pangani ambapo hutegemea huduma katika hospitali yetu ya Wilaya ya Pangani. Hospitali ya Wilaya ya Pangani bado haijajitosheleza, ukitazama *x-ray* hakuna, bado dawa ni shida, leo ukitaka *x-ray* mpaka uende Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali ya Awamu hii ya Tano katika bajeti yake ihakikishe kwamba inashirikiana na sisi kuhakikisha tunatengeneza vituo vya afya vya ziada ili kuisaidia jamii yetu ya Pangani katika suala zima la afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kusema kwamba wapo watu ambao wanajigeuza bundi kukitakia Chama cha Mapinduzi mabaya kife, lakini nasema watakufa wao na ofisi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyofanya Chama cha Mapinduzi ni kubwa, ukiangalia katika Wilaya yetu ya Pangani mpaka mwaka 2005 tulikuwa na shule mbili tu za Serikali, lakini sasa hivi tuna shule saba hata mimi mtoto wa mama ntilie nimefika Chuo Kikuu, dogo hilo? Mungu atupe nini, hata Mwenyezi Mungu anasema katika vitabu vya dini *waamma biniimati rabbika fahadith* (zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru). Sasa leo usiposhukuru kidogo unataka ukashukuru wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kubwa lakini ninachokiomba iendelee kutengeneza miundombinu ya elimu, vilevile kuboresha maslahi ya elimu kwa watumishi ili kuhakikisha wanafaidika na kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sina maneno mengi ya kusema, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, hayupo. Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mheshimiwa Sebastian simon Kapufi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze tu kwa kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwenye sekta ya kilimo ambayo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imo kuanzia ukurasa wa 26 hadi 32. Nijikite kwenye zao la korosho. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, ndugu yangu Majaliwa Kassim, kwa kazi kubwa sana aliyoifanya wakati alipofanya ziara kule Ruangwa na kutoa tamko la Serikali la kuondoa tozo tano ambazo zilikuwa ni kero za wananchi, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tatizo la korosho ambalo ni zao la pili kwa kuiingizia pato Serikali yetu, ukiacha tumbaku ambayo ni ya kwanza. Lakini hali ya wakulima wetu Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua, hali za wakulima wetu ni hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna sakata linaloendelea katika Wilaya ya Masasi ambalo wakulima hawajalipwa fedha zao kati ya shilingi 200 hadi shilingi 400 kwa kila kilo, lakini hadi sasa kuna wingu ambalo halieleweki wakulima wale watalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linawafanya wakulima wetu wawe katika mazingira magumu sana. Wanahangaika, wanapalilia, wanapulizia, wanakwenda kuokota korosho zao, wanapeleka kwenye Vyama vya Msingi, vinakwenda kwenye Vyama Vikuu na hadi pale kupata soko, lakini baadhi ya wachache wakiwemo baadhi ya Maafisa Ushirika ambao siyo waaminifu wanashirikiana na baadhi ya Viongozi wa Bodi za Wakulima wa Vyama vya Msingi kuwaibia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Wilaya ya Masasi safari hii tumesema tunahitaji fedha walipwe wakulima, nani amechukua, ameziweka wapi, hiyo siyo hoja yetu! Ninamshukuru sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mwigulu baada ya mazungumzo naye amekubali kufanya ziara kwenda Masasi kujionea hali halisi na ninaamini kabisa kwa utendaji wake mzuri ataweza kuwaridhisha wakulima wale na kuwapa matarajio na mategemeo makubwa jinsi ambavyo Serikali inajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ili kuwasaidia wakulima wa korosho katika mikoa yote ambayo inalima korosho ni lazima kufanya *reshuffle* ya Maafisa wa Ushirika. Maafisa wa Ushirika waliokaa katika Mkoa wa Mtwara sasa wamekaa wengine zaidi ya miaka 10 wengine miaka 15, katika mazingira hayo wanatengeneza mtandao wa kutengeneza hata Bodi za Wakulima kule kwenye Vyama vya Msingi na kuhakikisha wanajipatia kipato kutokana na hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Ofisi ya Waziri Mkuu ilifanyie kazi hili kwa nguvu zake zote ili kumfanya mkulima sasa ajengewe matumaini kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano ni Serikali inayowajali wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya afya. Nimesoma kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesisitiza sana jinsi ambavyo Serikali itajitahidi sana kuhakikisha kwamba inaboresha sekta ya afya, nimueleze tu Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa hivi ameelekeza kwenye ukurasa wa 55 kwamba tujitahidi sana tuhakikishe tunawahamasisha wananchi waweze kujiunga na Bima ya Afya. nimthibitishie tu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba kazi hiyo zimeshaanza kufanywa na wananchi wamehamasika lakini nina mashaka juu ya jambo hilo, kukakatishwa tamaa wananchi kwa sababu wamekata Bima, lakini wanapokwenda kwenye zahanati zetu hakuna dawa! hivyo hawaoni umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya kama hawapati dawa kwenye zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu ijikite kuhakikisha kwamba haya yote yanakwenda sambamba, tunahamasisha suala la Bima ya Afya, lakini tunaongeza dawa kwenye zahanati zetu na watendaji wetu ili wananchi wawe na uhakika kwamba wakienda zahanati wanapata dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka niliseme ni juu ya suala la barabara. Mheshimiwa Waziri Mkuu umeelezea juu ya jitihada ya Serikali jinsi ambavyo itaimarisha sekta ya barabara lakini nataka tu nikuhakikishie Mheshimiwa kwamba wananchi wanaimani kubwa na Serikali ya Awamu ya Tano sana, haya yote mnayoyasema na mnayotuambia tunakubali kwamba awamu hii mambo mengi yatatekelezwa, lakini nasisitiza suala la barabara kutoka Mtwara - Newala - Tandahimba hadi Masasi ambayo ni barabara ya uchumi. Napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Ujenzi atekeleze agizo la Mheshimiwa Rais alilolisema ataweka wakandarasi wanne ili kuhakikisha barabara hiyo inamalizika kwa haraka ili kutatua tatizo lililoko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maelezo hayo ambayo umetupa matumaini lakini kuna suala la barabara ya kutoka Masasi kwenda Nachingwea ambayo inaunganisha hadi Ruangwa hadi Nanganga kwenye Jimbo la

Mheshimiwa Waziri Mkuu. Barabara hii tumeisemea muda mrefu, kwa kweli kuna kila sababu barabara hii ijengwe. Ni barabara muhimu inaunganisha mikoa miwili, ni barabara ya uchumi na kwa hakika wewe mwenyewe huwezi kujisemea, sisi lazima tuseme kwamba barabara hii sasa tunataka ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nijikite katika eneo hilo lakini pia nimalizie kwenye sekta ya elimu. Mimi niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu bahati nzuri alikuwa mwalimu. Naamini kilio cha walimu sasa kitapewa kipaumbele. Kilio kile ambacho kwa kweli muda mrefu wao wamekuwa wakilalamikia kuhusu marupurupu yao, kuhusu nyumba, kuhusu stahili zao nyingine, hatutegemei Serikali ya Awamu ya Tano walimu wawe ni sehemu ya manung'uniko kama ilivyokuwa miaka mingine.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili lipewe kipaumbele ili Walimu waweze kupewa umuhimu katika jamii na ndiyo sekta ambayo inaajira pekee kuliko sekta nyingine na Walimu ni wengi naamini kabisa Serikali hii na Walimu wameshaanza kuwa na imani, tuendelee kuwapa imani zaidi ili wafanye kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea kuchangia, naomba kuwakumbusha kuhusu utaratibu wa kuchangia, wakati tukianza Mwenyekiti alitukumbusha wiki iliyopita kuhusu Kanuni ya 99 (10) kinasema, wakati wa kujadili makadirio na matumizi ya Wizara, muda wa Wabunge kuchangia utatolewa kulingana na uwiano wa idadi ya Wabunge kutoka katika kila chama.

Waheshimiwa Wabunge, Kingozi wa Upinzani Bungeni wakati akitoa hotuba yake, ukurasa wa 6 na wa 7 nitanukuu baadhi ya maeneo, ukurasa wa 6 unasema hivi: "Katika hali isiyo ya kawaida Serikali pamoja na Uongozi wa Bunge imewapoka wananchi haki yao ya kupata habari za Bunge kwa kuzuia mijadala Bungeni kurushwa moja kwa moja na televisheni ya Taifa na vyombo vingine vya habari vya kujitegemea."

Katika ukurasa wa 7 anasema; "Katika mazingira kama hayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haiko tayari kuendelea kushiriki uvunjaji wa Katiba, Sheria na Haki za msingi za Wananchi," na pia anasema hivyo basi, Kambi bado inatafakari kwa kina na makini hatua za kufuata."

Waheshimiwa Wabunge, nitaendelea kusoma majina ya wachangiaji wa Chama cha Mapinduzi (CCM) watatu wanaosalia wakati nikisubiri hizi hatua ambazo wamesema watachukua kama sitapata maelekezo hayo basi wataendelea kuchangia Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu.

**MH. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyenijalia kusimama hapa na nichukue pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa kwetu, pia wala sitaki kusema neno baya kwa upande wa pili niwapongeze kwa sababu wametupa nafasi na sisi tuweze kuongea, wananchi wajue Serikali yao chini ya Chama cha Mapinduzi imefanya nini na itaendelea kufanya nini. Niseme kwa niaba yenu, niwaambie wale ahsanteni sana, acheni tujimwage kwa raha zetu ndani ya Ukumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia suala la afya. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake ameligusia vizuri sana suala la afya, ukiangalia bila afya bora hakuna ambaye anaweza akafanya kitu chochote, hata humu ndani kama afya zetu zisingekuwa bora tusingeweza kuja humu ndani, hivyo ninampongeza sana kwa kuliona hilo na kwa kulizungumzia lakini naiomba Serikali tusaidiane, tumeambiwa tuhamasishe suala la mfuko wa afya *CHF* wananchi wamepokea wito kwa nguvu zao zote, tatizo linakuja kwenye utoaji wa dawa. Wanafika kwenye dirisha hawapati dawa, sasa ni wakati muafaka, *MSD (Medical Store Department)* iwezeshwe vya kutosha, nimpongeze Waziri wa Afya na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini *MSD* isimamie suala la upelekaji dawa ili watu wapate dawa afya zao ziweze kuimarika na waweze kufanya kazi vizuri. Mtu hawezi kwenda shambani kama afya yake siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo. Bila pembejeo, bila mbegu nzuri hakuna kilimo kitakachoweza kuwa kizuri. Ufunguaji wa milango ya biashara, ukimwezesha Mkulima kuna uhakika wa kutosha, akipata pembejeo, akipata mbegu bora, atalima yeye na atalima kwa ajili ya kuuza nje hata ndani ya nchi, hilo naomba tuliangalie na tulipe kipaumbele chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani tuna mabonde na mito mingi sana, tuna Mto Ruaha, tuna Mto Wami, tuna Mto Rufiji, tuna Mto Ruvu, tuna mambonde mengi sana, tunaomba kilimo cha umwagiliaji kiwekewe mkazo katika mabonde hayo ili wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana wakiwezeshwa, wakipewa teknolojia ya umwagiliaji hatutaweza kuwaona tena wanakwenda kucheza *pool,* tuwawezeshe vijana walime zao ambalo ni jepesi kulima kwenye mabonde, zao la mpunga, zao la nyanya, zao la vitunguu, zao la bamia, mbogamboga hata mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo, naiomba Serikali iweke utaratibu mzuri katika kilimo, pia kutumia maji katika mito yetu na kuweza kufanya zoezi la umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya mito niliyoitaja mitatu, naiomba Serikali ifikie wakati sasa ule mradi wa Kisemvule uanze kazi mara moja. Mradi ule uko Wilaya ya Mkuranga lakini utakapowezeshwa utawanufaisha hata watu wa Dar es Salaam kama mradi wenyewe unavyosema. Lakini mpaka sasa hivi katika maeneo ya Wilaya ya Kisarawe, Wilaya ya Mkuranga, hata Wilaya ya Kibaha Vijijini na Mjini bado tuna matatizo ya maji, naomba sana Serikali ione umuhimu wa kuwezesha upatinaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha mradi huo wa Kisemvule tuone Serikali imechukua hatua zipi sasa za kuweza kuuwezesha mto Rufiji ufike kwenye maeneo jirani, ufike kwenye Wilaya Mkuranga, ufike Wilaya ya Kisarawe hata Dar es Salaam, maji ya Rufiji yanaweza yakasaidia badala ya kuyaacha maji yale yanakwenda yanaingia baharini hatuoni faida kwa watu wengine. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kutusaidia katika upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongee Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kauli mbiu yake aliyoitoa ya kwamba Tanzania sasa iwe nchi ya uchumi na viwanda. Kweli huu ndiyo wakati muafaka umefika, Serikali ina wajibu wa kufanya hilo na sisi tunaunga mkono. Kwa kuanzia katika Mkoa wetu wa Pwani pamoja na maeneo mengine viwanda vipo lakini Wilaya ya Mkuranga tayari inaongoza kwa kuwa na viwanda vingi, ninaiomba Serikali iangalie umuhimu wa kuwasaidia Watanzania kwanza, tuweke mikataba ambayo itakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwaangalie Watanzania wenye elimu ya kutosha, waweze kupata nafasi kusimamia shughuli za viwanda isiwe vijana wa ajira ndogo ndogo ndiyo waajiriwe katika viwanda vile. Kweli tunasema viwanda ni mkombozi, nimuombe kaka yangu na ndugu Mheshimiwa Mwijage ahakikishe kwamba wale Wawekezaji nazungumzia kwa upande wa Mkuranga sasa hivi ambapo ndiyo tunapokea malalamiko, wanalipwa shilingi 5000 kwa siku, anaingia saa mbili asubuhi, anatoka saa 2 usiku, shilingi 5,000 ukipiga hesabu elfu tano kwa mwezi ni shilingi 150,000, hapa tumemsaidia au tunatumia nguvu zake tu kuwasaidia wale wenye viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali iangalie hasa Wizara husika ya ajira ipite kwenye viwanda, ikibidi hata tufuatane naye Waziri husika akaangalie ili aweze kuona hata usalama wa wale wafanyakazi, tunachohitaji viwanda kwa ajili ya ajira, lakini pia vitakavyozalishwa vije kwa Watanzania waweze kununua na pato la nchi liongezeke, lakini tuangalie na maslahi ya Watanzania watakaouwa wameajiriwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mikopo. Suala la mikopo kwa wakulima limeoneka vizuri, lakini naomba kujua je, wavuvi wao wamefikiriwaje? Watajiendelezaje katika uvuvi mdogo mdogo? Tunao wavuvi wa baharini, tuna wavuvi wa kwenye maziwa, pia kuna wavuvi wengine wapo kwenye mito yetu ambayo inatuzunguka katika nchi yetu ya Tanzania.

Ninaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwawezesha wavuvi na kuangalia zile sheria, sheria zinamlindaje mvuvi mdogomdogo pamoja na hata yule mvuvi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuipongeza Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kuleta mkopo kuwawezesha wananchi milioni 50 kila kijiji, milioni 50 kila mtaa, ni wazo jema, tulipangie utaratibu mzuri, tuwawezeshe wanawake, tuwawezeshe vijana wetu bila kuwasahau wananume, wako ambao na wao wanahitaji kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafsi hii kusema kwamba naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu na tuko tayari Watanzania kufanya kazi kwa kuijenga nchi yetu na kukijenga Chama chetu ahsante sana.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, halafu Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nianze na pongezi. Naipongeza hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imesheheni mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya Mkoa wa Katavi naomba nianze na eneo la afya. Mkoa wetu ni mpya, najua zipo jitihada za maksudi za kuusaidia Mkoa ule kwa maana ya kupata hospitali ya Mkoa. Rai yangu ni kwamba kama kwa kila mwaka tunatengewa shilingi bilioni moja na mpango mzima unakusudia bilioni 27 maana yake kuna miaka 27 kuweza kuijenga hospitali hiyo. Ninaomba Serikali yangu sikivu tupaone hapo kwamba watu wale kwa namna yoyote ile wasaidiwe ili kuhakikisha hospitali ya Mkoa inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la maji niendelee kuishukuru Serikali hii, tulikuwa na mradi wa Ikolongo sasa hivi tunakusudia kuwa na mradi wa Ikolongo II. Mipango yote ya kuhakikisha mradi huo wa Ikolongo Na. II inaendelea kukamilika. Naendelea kuiomba Serikali maji haya ni msaada kwa wananchi wetu, pamoja na kwamba siyo wote wanaofikiwa na maji haya naendelea kuamini, utakapokuja mradi huu wa Ikolongo Na. II uwezekano wa eneo kubwa la Mji wa Mpanda kupata maji utakuwa umekamilika pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu eneo la barabara, mara ya mwisho tarehe 8 Aprili, kulikuwa na uzinduzi wa barabara Tabora – Koga - Mpanda kwa kiwango cha lami, mradi huo umeenda sambamba na watu wa Mbinga - Mbamba bay. Mimi nishukuru kwa jitihada hizo, lakini niendelee kuomba tena kwa maana ya barabara ya kutoka Sumbawanga - Mpanda na hiyo kama haitoshi kutoka Mpanda kwenda Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu mno kwa watu wetu, siku zote naendelea kusema sioni kama ni sahihi kuwaita wale watu ni watu wa wapembezoni maanake hata Dar es Salaam yenyewe iko pembezoni, lakini suala tu la kuwezesha miundombinu itapelekea kufanya maeneo yale yasisomeke kama ya pembezoni.

Mkuu wangu wa Mkoa nilimpenda siku moja, alisema badala ya kuita ni mikoa ya pembezoni ni bora ikaitwa mikoa ya mipakani maana yake pembezoni inafanya watu wajione kuwa wanyonge na hawana sababu ya kuwa wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la madini. Mkoa wetu una bahati ya kuwa na madini mengi. Kuna dhahabu, kuna shaba, kuna garena, ni rai yangu na bahati nzuri ndugu zangu wa madini wapo hapa, kwanza nitakuwa mtu wa ajabu nisiposhukuru jitihada za makusudi zinazofanywa hasa kuwawezesha wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba, kuna maeneo ya Ibindi, maeneo ya Kapanda, maeneo ya Dirifu, maeneo haya kwanza kuna vijiji kuna makazi lakini maeneo pia ambapo wachimbaji wadogo wamekuwa wakijipatia riziki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo maeneo mengine ya wachimbaji wadogo kutengewa maeneo, ninaomba Serikali hii sikivu iendelee kuyatenga maeneo hayo yawe rasmi kwa ajili ya wachimbaji wadogo, ili watu wao waendelee kukidhi shida zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la uvuvi, Mkoa wetu wa Katavi kwa ujumla wake upande mwingine tuna Ziwa Tanganyika. Tunapozungumzia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kama ambavyo tumekuwa tukisaidia wananchi wetu kuwapa taarifa mbalimbali za hali ya hewa, kwamba kutakuwa na mvua kali, kutakuwa na mawingu, kutakuwa na nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iende mbali zaidi, kama tutashindwa kuwa na vifaa vya uvuvi vya kisasa, walau basi iwepo na *centre* ya taarifa sahihi zinazogusa masuala ya kiuvuvi ili kuwasaidia wavuvi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yangu ni nini? Kama kuna taarifa zilizotoka kwa wataalam wetu kwamba kama Jumatano, Alhamis, Ijumaa mtakusudia kwenda Ziwani kuvua, uelekeo wa samaki utakuwa eneo la Kaskazini, uelekeo wa samaki utakuwa eneo la Kusini, kwa hiyo, mvuvi badala ya kwenda Kaskazini akaachana na samaki wako Kusini, kwa taarifa hizi zitamfanya avue uvuvi wenye tija. Lakini zaidi ya hapo ni kuwa na vifaa vya uvuvi vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba nizungumzie suala la bandari. Najua jitihada zinazofanywa na nchi hii na kwa kweli niombe sana, siyo dhambi kuwa hapa tulipo na kusomeka ni nchi ambayo inazungukwa na maji pande zote, tuitumie hii kama ni fursa. Sisi kule kwa maana ya Ziwa Tanganyika tuna bandari ya Kalema, ni bandari ambayo ikifanyiwa kazi vizuri itaendelea kuibua fursa mbalimbali za watu na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoke hapo nije kwenye eneo la misitu. Mkoa wangu wa Katavi kwa sehemu kubwa una misitu mizito. Nilichokuwa naiomba Serikali hii sisi kuwa na misitu isiwe dhambi. Nimeona vyombo vingine vya Kimataifa vinatoa fedha kwa ajili ya watu kuendelea kupanda miti na vitu vingine vya namna hiyo ikisaidia dunia hii kama maeneo ya mapumulio na kuachana na suala la hewa ukaa. Kwa hiyo, sisi ambao kwa bahati nzuri tumeendelea kutunza misitu hii isiwe dhambi sisi kuwa kwenye maeneo ya misitu. Serikali iendelee kuona kwamba watu hawa kwa kutunza mazingira na kwa kuwa na misitu mikubwa wanaendelea kuwasadia watu wa maeneo mengine, kwa hiyo tule nafasi ya sisi kutunza maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo niende eneo la utalii. Tuna mbuga nzuri ya Katavi nilisema mahali pengine na nitarudia tena. Tabia ya watalii kama hana kitu kipya cha kuona hana sababu ya kuja. Kwa hiyo, kwa nchi hii kuna maeneo mengine ambapo watalii wamekuwa wakiyatembelea miaka nenda miaka rudi. Sasa tusiwapoteze watalii hao kwa ajili ya kwenda maeneo ambayo wamekwishaona kwa zaidi ya miaka 15, tuibue fursa nyingine ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, mtalii huyo badala ya kuikimbia Tanzania atakuja kwa kwenda eneo lingine, naomba sana tuinue eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kilimo najua kuna suala la pembejeo, lakini niombe sana habari ya matumizi ya mbegu ambazo hazina uhakika tutaendelea kuwafanya watu wetu wasitoke kwenye mduara wa umaskini. Kwa sababu kama anapanda halafu hana uhakika wa kuvuna huyu mkulima tunamtoaje hapo? Ataendelea kuzunguka kwenye mduara wa umaskini. Kwa hiyo, niombe sana, sambamba na pembejeo lakini tuendelee kuangalia suala hilo la mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la uwanja wa ndege, sikatai maeneo mengine kujengwa viwanja vya ndege lakini kupanga ni kuchagua. Kama kuna viwanja vilikwishajengwa na vingine havikukamilika kwa nini tunakwenda kuanza na vitu vingine vipya? Uwanja wa ndege wa Katavi pale Mpanda ni mzuri, umebakiza mambo machache ili ukamilike na ndege ziweze kufika pale, leo siuoni ukizungumzwa popote pale. Kama tatizo ni *route* za ndege, Serikali yangu sikivu ifanye hilo kwa makusudi kuhakikisha kama ni shirika letu hili ambalo lengo lake ni kutoa huduma kwa watu wote wapangiwe *route*, wakienda mara moja wakiona idadi ya wateja inapatikana wao wenyewe ndiyo watajikita katika kuongeza idadi ya *route* za kwenda huko. Nalisema hilo kwa sababu wananchi wengi wa Katavi wakitamani huduma ya ndege ama wakaipandie Mbeya ama wakapandie Kigoma *sometimes* wakapandie Mwanza na uwanja uko pale. Nilikuwa naliomba sana hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, reli niendelee kushukuru lakini tukisema tafsiri ya reli ya kati ni kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Kigoma, hiyo inayokwenda Mwanza lakini bila kusahau matawi ya Kaliua, Mpanda na Kalema. Tukilifanya hili lina tija, si kwamba watu tunatamani kulisema hilo, hapana, ni kwa maana ya tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la vijana na mikopo niendelee kushukuru Serikali sikivu. Tukiendelea kuwawezesha vijana wao wenyewe ndiyo wataendelea kuibua miradi mbalimbali ya maendeleo. Kundi hili la vijana ambao wakati fulani wameonekana kama wamesahaulika tukiwajengea uwezo watatoka hapo walipo. Mimi nina mifano hai nikizungumzia kwa mfano wachimbaji wadogo wadogo ambao ni kundi la vijana, vijana hawa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kuungana na wenzangu kuunga mkono bajeti ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala ambao ulikuwa unaendelea humu ndani wako watu waliosema hakuna utawala bora, Rais anaingilia mihimili mingine, mimi niseme, hivi wewe ndiyo baba mwenye nyumba, mke uliyemuoa ana watoto amekuja nao...

**MBUNGE FULANI:** Duh!

**MHE. DEO K. SANGA:** ...amezaa na mtu mwingine na mtu mwingine, wewe ndiyo wa tatu…

**MBUNGE FULANI:** Wachaa!

**MHE. DEO K. SANGA:** Unasimamia watoto wa kwako na hawa, hivi hawa wengine wakiwa wezi huwezi kuwaambia acheni wizi?

**MBUNGE FULANI:** Unawaambia.

**MHE. DEO K. SANGA:** Utaambiwa unaingilia? Ndugu zangu, kwa nini tunadhoofisha nguvu zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano?

Rais anafanya kazi nzuri sisi sote ni lazima tukubaliane kwamba Rais anafanya kazi nzuri. Mawaziri wake wanafanya kazi nzuri ni lazima tuwaunge mkono, tumeona kwa macho yetu wenyewe. Halafu tunakuja hapa tunasema anaingilia mhimili mwingine. Hivi mtu unakuwa mwizi asiseme kwamba jamani acheni wizi? Hawa Ofisi yako Waziri Mkuu na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli lazima waangaliwe vizuri watumbuliwe na wenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM…

**MBUNGE FULANI:** Ehee.

**MHE DEO K. SANGA:** Kila wakati mmesema Serikali hii hakuna chochote, hakuna kitu, sasa imeleta bajeti tangu mimi nimekuwa Mbunge hakuna bajeti nzuri na yenye mwelekeo mzuri kama hii, hii sasa imebaki ni ukombozi kwa Watanzania. Tuseme kweli jamani, tuwe wapenzi wa Mungu bajeti hii ina mwelekeo mzuri, inaonesha dira kwamba sasa angalau wananchi wetu matatizo mbalimbali yatapungua au yatakwisha kabisa katika miaka mitano, lazima tuipongeze Serikali ya CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sasa Jimbo langu la Makambako. Rais alipotembelea katika mji wetu wa Makambako aliahidi ahadi sita na moja kutatua tatizo la maji katika mji wa Makambako.

Pili ilikuwa ni lami kilometa sita katika mji wa Makambako; tatu ilikuwa ni fidia ya soko la kimataifa kulipwa kwa wananchi wa mji wa Makambako na nne ilikuwa ni vifaa vya upasuaji katika hospitali ya mji wa Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mji wa Makambako tumepata madaktari wazuri, tatizo kubwa tunalolipata gari letu la kubebea wagonjwa kila siku linapeleka mara tano, mara sita Wilayani Njombe kwa ajili ya upasuaji. Tuombe sana Serikali itupe vifaa vya upasuaji ili kupunguza gharama za kupeleka watu kule Njombe kila wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ni kuimarisha uwanja wetu wa michezo na sita ilikuwa ni umeme vijijini. Ahadi hizi zote za Rais nimewapelekea Mawaziri wote wanaohusiana na Wizara hizi. Ombi langu wahakikishe wanazifanyia kazi ili ziendane na kasi ya Rais wa Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, pale Makambako upande wa Polisi ni Wilaya inayojitegemea Kipolisi, yupo *OCD* na kadhalika. Tuna eneo kubwa sana la kujenga nyumba za polisi hata nyumba moja ya polisi pale haijajengwa. Ombi langu tuhakikishe tunajipanga vizuri ili tuweze kuwajengea nyumba nzuri za kuishi hawa askari wetu wa polisi pale Makambako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo lingine upande huo huo wa polisi, katika kituo chetu pale ni *centre* kubwa sana ya kwenda Mbeya, Songea, Liganga na kadhalika. Gari la polisi linalotumika ni la siku nyingi na wakati fulani *RPC* amekuwa akitoa gari kutoka Njombe. Niombe sana tuhakikishe pale tunapewa gari na wakati fulani gari lingine limechukuliwa kutoka Ludewa na ndiyo lipo pale Makambako. Kwa hiyo, niombe sana katika bajeti hii kuhakikisha tunapata gari letu la polisi ili gari la Ludewa liweze kurudi Ludewa mahali ambapo walikuwa wameliazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu inaelezea kujenga *VETA* kila Wilaya. Naomba tuhakikishe tunajenga *VETA* katika Wlaya yetu ya Njombe ili vijana hawa wanaomaliza darasa la saba, kidato cha nne waweze kwenda kujifunza ujuzi mbalimbali katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe sana Waziri wa Ujenzi, tulikuwa tumeleta maombi kupitia kikao chetu cha *RCC* cha Mkoa kupandisha hadhi za barabara inayotoka Makambako – Mlowa - Kifumbe - Kitandililo na barabara nyingine ya *TANROAD* ambayo inatoka Ikelu - Ilengititu – Kifumbe. Niombe sana

kwa sababu Halmashauri haina uwezo wa kuweza kutengeneza barabara hizi tuombe zipandishwe hadhi ili kusudi ziwe zinapitika wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua bajeti hii hata kuchangia ni wajibu wa kuchangia lakini kama nilivyosema ni nzuri, ni lazima tuiunge mkono ili Serikali iende ikafanye kazi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Amen!

**MHE. DEO K. SANGA:** Serikali ya CCM kwa kweli sasa tunatembea kifua mbele kwa sababu ya Serikali ya Awamu ya Tano na watu wanaomsaidia Rais Waheshimiwa Mawaziri, songeni mbele msisikilize maneno ya watu hawa, wanataka kuchelewesha shughuli za maendeleo. Hawa wamejipanga kuchelewesha shughuli za maendeleo ili 2020 tukwame, songeni mbele na watakwama wao. *(Makofi)*

Sasa umekuja hapa hutaki kuchangia na watu wamekutuma hapa uje kuchangia maana yake nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu nimalizie kwa kusema naunga mkono bajeti hii naitaka Serikali kuhakikisha tunapotoka hapa inakwenda kufanya kazi zilizopangwa katika maeneo yetu, CCM!

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**. Mheshimiwa Deo nadhani ulitaka kumaliza vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, wanaofuatia ni Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae Mheshimiwa Ali Seif Ungando, atafuatiwa na Mheshimiwa Adad Rajab.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, nimpongeze sana Mheshimwa Rais na kumuombea kila lililo jema katika maisha yake. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na juhudi zake na Baraza la Mawaziri kwa ujumla. *(Makofi)*Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwatake Wabunge wetu wote tuendeshe siasa za kistaarabu na siasa za utashi mwema. Tumekuja huku Bungeni tukiwa na nia njema ya kuzungumza matatizo wa wananchi wetu.

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali kwa Mpango wake wa bajeti wa mwaka huu 2016/2017 ni mpango mzuri kwa kuwa unagusa maisha ya Watanzania na hasa hasa kupeleka fedha nyingi katika ngazi za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuzungumzia mambo machache. Kwanza, nizungumzie eneo la miundombinu. Kwa kweli tumekwama sisi Wilaya ya Mbulu katika ile barabara ya Magara, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake watuonee huruma waangalie ule mlima na jinsi ambavyo nguvu ya Serikali inahitajika sana. Kwa kweli katika mwaka huu wa bajeti nashukuru kwa nia njema ya Serikali kwa kutenga fedha za bajeti katika ule mpango wa kujenga bwawa la umwagiliaji kule kwetu na ile barabara pia kwa ajili ya mlimani kuna nia njema hadi sasa tuendelee kuona ni namna gani tunakusanya mapato ili tuweze kutatua tatizo hili la jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nizungumzie jinsi ambavyo tunaweka vipaumbele katika ule utatuzo wa kero za wananchi. Kwa kawaida mtu hawezi kutambua juhudi za aliyeko kwenye uendeshaji wa chombo, mara nyingi mtu mwingine huwa haoni kama anayeendesha chombo anaendesha vizuri. Mimi niseme tu kwamba jitihada hizi ni kubwa na juhudi za Rais ni kubwa na ndiyo maana anaamua kupeleka fedha kwenye yale maeneo nyeti inapobidi na ambayo ndiyo kero kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iendelee na kasi yake iliyoanza nayo, iendelee kufanya kazi zake kwa juhudi zote, iendelee kuona mawazo yote tunayochangia katika hii bajeti ni kwa namna gani yanaingia katika mpango wetu na yaweze kutatuliwa pale inapobidi. Si kwamba tunashindwa kutekeleza miradi, ni uwezo wetu lakini pamoja na makwazo mbalimbali. Niitake Serikali iangalie kwa dhati kabisa eneo la majanga. Eneo la majanga na dharura kwa maana ya maafa ya mvua, njaa, magonjwa na maafa mengine yoyote yanakwamisha mipango ya bajeti kwa kila mwaka kwa sababu yanajitokeza baada ya sisi kupanga mipango. Kwa hiyo, niitake Serikali ione ni kwa namna gani inatazama maeneo yanayoweza kuzuilika katika majanga yanayotokea. Mara nyingi tumepata majanga makubwa lakini yanatokea baada ya Serikali kupanga bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa bajeti ulioisha tulikuwa na dosari nyingi kwenye miradi mingi kwa kukosa fedha. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kadiri inavyowezekana ione ni namna gani basi hata ile miradi iliyokwama iaingizwa kwenye mpango wa bajeti. Kwa sababu katika ngazi za chini huwa wao bado wanategemea mpaka Juni 30 ile miradi itapata fedha lakini nikitazama naona miradi mingi itakosa fedha na isipohamishiwa katika mwaka wa fedha unaokuja basi ile miradi itakuwa imesahaulika na ni miradi viporo na haitaweza kukamilika kwa namna yoyote ile kwa sababu itakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza bajeti au mpango wa maendeleo wowote ni mpango endelevu unaotekelezwa kwa awamu na unapofika ukomo wa muda uliotarajiwa maeneo yote ambayo hayakufanikiwa hayana budi kuhamia kwenye ule mpango mpya unaoendelea. Kwa hiyo, kila mtu au kila mdau wetu atazame, tuunganishe nguvu katika kukusanya nguvu kwa wadau wa maendeleo, Serikali kama Serikali na wananchi wetu huwa wana mchango mkubwa katika eneo hilo kwa kutoa michango yao ya hali na mali katika kuchangia shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianza na mambo mengi sasa hivi tunakejeliwa na shule za kata lakini bado zimeendelea kufanya vizuri na tulikuwa na tatizo la madawati limeendelea kutatuliwa. Kwa kawaida isingekuwa rahisi kila mtu atambue mchango wa Rais kwa sababu hapa tunatofautiana kiitikadi na ndiyo jitihada zinakwamishwa. Kwa hiyo, wote kwa pamoja tuunge jitihada za Rais na Waheshimiwa Mawaziri wala msikwazike nendeni kwenye Majimbo, kama nilivyowaalika kwenda Jimbo la Mbulu Mjini nendeni bila kunitafuta mimi, hamna sababu ya kunitafuta mimi Mbunge niko wapi, jitihada kubwa inahitajika kutoka kwao wao waende kwa wakati na waweze kutusaidia katika ile hatua nzuri wanayotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala lingine la shilingi milioni 50 zinazolalamikiwa. Bado ni mapema sana, ndiyo tumeanza mwaka wa bajeti ya Serikali. Huu ni mwanzo wa kujadili bajeti ya Serikali na jinsi tunavyojadili hii, matokeo yake na changamoto zake baadaye ni sisi ndiyo tutakwenda kujadili kama Wabunge kwa niaba ya wananchi. Wananchi wana haiba na hamu kubwa ya kuona kwamba matatizo yao tunayajadili bila kupoteza muda na bila kuendeleza *propaganda* za kukwazana na porojo katika ukumbi huu wa mjadala wa matatizo ya wananchi kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuzungumzia maeneo machache katika bajeti hii ambayo yanahitaji kutazamwa sana. Moja ni yale yaliyoguswa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu Ilani hiyo ndiyo imeweka ahadi kwa wananchi na wananchi wanategemea ahadi yao itatekelezwa kwa jinsi ambavyo viongozi walioomba kura walisema na jinsi ambavyo Ilani imetafsiriwa kwao. Eneo hili linahitaji kutazamwa ni namna gani Ilani na zile ahadi za Rais zinaingizwa kwenye mipango ya mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais alipokuwa Jimboni Mbulu aliahidi lami kilometa tano, naomba basi Serikali kila mwaka iweke utaratibu wa kutatua ahadi yake hiyo. Aliweka ahadi ya kuweka zege mlima Magara na daraja la Magara na pia barabara ya Mbuyuni - Magara - Mbulu ipate lami. Kwa sababu eneo hilo kwa jiografia ni hatarishi na kila kiongozi aliyeenda Mbulu ilikuwa hatuna sababu ya kumpitisha huko lakini ndiyo barabara pekee

inayotuunganisha sisi na Babati kama makao makuu ya Mkoa na ndiyo inayotuunganisha sisi pia na mji mkubwa wa kibiashara wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ujumla niseme bajeti ni nzuri, naunga mkono hoja na naomba Serikali isimamie utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia vipaumbele na kwa jinsi ambavyo bajeti hii itagusa maisha ya mwananchi wa chini ili mwisho wa siku matokeo mazuri ya hapa kazi tu yaonekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Seif Ungando. Tunaendelea na Mheshimiwa Adadi Rajab atafuatiwa Halima Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Napenda kumshukuru kwa jinsi alivyoanza kuendesha Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa nguvu, kwa kasi na kwa weledi mkubwa na kwa vitendo na sio blah blah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia tukiwa na mipango mingi, miradi mingi, maneno mengi lakini sasa hivi tumepata mtu ambaye anaonesha vitendo. Rais ambaye anaonesha kitu gani ambacho kinatakiwa na sio kuzungumza blah blah. Kwa muda mrefu tumekuwa na sera nyingi lakini ndugu zangu mtakubaliana nami kwa kipindi kifupi mmeona vitendo ambavyo amefanya. Amechukua hela kutoka mafungu mbalimbali na kuyapeleka kwenye mambo muhimu ambayo yanawagusa wananchi wa kawaida kama mambo ya barabara, vitanda hospitalini, madeski ya shule na mambo kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu nimefurahi sana na nashukuru kupata mtendaji wa aina hiyo. Nchi yetu sasa hivi inataka kiongozi wa aina hiyo anayeweza kutoa amri, kutekeleza na kufuatilia. Naamini kama Rais Magufuli angekuwa amechukua mafunzo ya komandoo basi miezi sita tu hii nchi ingeweza kuwa kwenye mstari ambao unatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kupongeza uongozi mzima kwa jitihada kubwa ambazo zimefanyika hivi karibu mpaka tumepata mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Kampala na kuyaleta kule kwenye bandari ya

Tanga. Mradi huo ni mkubwa na lazima uende sambamba na sehemu ambazo bomba hilo litapita kwa kuonesha wananchi watafaidika namna gani. Bandari ya Tanga kama mlivyosikia ina kina kirefu kuliko bandari zote na ndiyo moja ya sababu iliyofanya tupate mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningefurahi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kama wangechambua sasa hivi hiyo bajeti ambayo ipo, wahakikishe kwamba wanaimarisha vitu vyote ambavyo vinahitajika kwenye bandari ya Tanga, kuna vifaa ambavyo ni vichakavu sana kwenye bandari ile. Vifaa vyote hivyo na mambo yote hayo ambayo yanatakiwa ni lazima tuhakikishe kwamba bandari hiyo inaimarika ili tuweze kukabiliana na huo mradi ambao unakuja.

Ningeshukuru sana kama reli ya Tanga na yenyewe ingewezwa kuimarishwa. Najua imewekwa kwenye bajeti lakini nitashukuru kama na yenyewe inaweza kuwa kwenye *standard gauge* ili iweze kuungana na reli ya kati iweze manufaa makubwa kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru pia kama kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Tanga kitaimarishwa kwa sababu sasa hivi kutakuwa na watu wengi, wimbi litakuwa ni kubwa, kwa hiyo, tunaomba uwanja huo na wenyewe uweze kuwekwa kwenye mpango huu na kuweza kuimarishwa kwa kupanuliwa tayari kwa kupokea wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, sisi Muheza bomba hilo litapita, tunataka kutayarisha kituo cha matunda *(center* ya matunda) kuhakikisha kwamba kwa mradi huo panakuwa na *additional value* ili kuona tunafaidika vipi na mradi huo. Kwa hiyo, tumeshatayarisha sehemu za wawekezaji kuhakikisha kwamba tunatengeneza sehemu ya matunda, tunataka Mji wa Muheza uwe mji wa matunda. Matunda yote ya Mkoa wa Tanga yaweze kupatikana kutokea Muheza. Tumeshaanza kukaribisha wawekezaji na tungeomba Serikali ituunge mkono kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo lakini vitu hivyo vinakwenda na miundombinu, ni lazima tuhakikishe kwamba tunaziimarisha barabara, mkoa wa Tanga tuna barabara ya Muheza kwenye Jimbo langu, barabara ambayo Serikali imeahidi kuiweka lami, barabara ya Amani mpaka Muheza. Amani kutoa vitu chungu mzima, kuna viungo, karafuu, pilipili manga, kuna vitu vingi sana na wakulima wa kule wanapata taabu sana kuleta vitu hivyo mjini. Pamoja na kuweka kituo cha matunda tuna mpango tuweke viwanda vya kusafishia viungo ili kuhakikisha kwamba Muheza inakuwa ni Muheza kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna tatizo la maji ambalo tumeanza kulishughulikia kwa kumuomba Waziri anayehusika lakini ningeomba liwekewe mkazo. Bila maji Muheza haiwezi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichangie suala la utalii. Vivutio ambavyo tunavyo nchi hii haviendani na watalii waliopo. Hatuwezi kusema tunakadiria watalii milioni 1.2 wakati tuna *National Parks* karibu 15, uwiano wake haupo. Kuna nchi ambazo zina kivutio kimoja tu, mimi nilikuwa Zimbabwe wana *Victoria Falls* tu lakini wanaingiza watalii milioni 2.5 kwa mwaka, sasa ni kwa nini sisi tushindwe kufanya vitu kama hivyo? Naomba suala hilo liangaliwe na tuone tunaweza kufanya nini kuweza kuongeza watalii. Kuna sehemu nyingi sana za utalii, Amani kule Muheza ni sehemu mojawapo ya watalii ila wanashindwa kwenda vizuri kule kwa sababu ya barabara. Naamini tutakapoiweka lami ile barabara kutakuwa na ongezeko la watalii sehemu za Amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo ni muhimu na linakwenda sambamba kabisa na sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ya viwanda. Bila kilimo, mazao na malighafi hatuwezi kufika. Tuchukue mifano ya nchi nyingine ambapo wanawawezesha wakulima, wanawakopesha pembejeo, wanawapa mbolea bure halafu baadaye wanakuja kuelewana na Serikali namna ya kuwakata. Kwa hiyo, naamini tukifanya hivyo tutaweza kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanaweza kufaidika na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake kubwa anazozifanya za kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata maendeleo. Vilevile naomba kuwapongeza ndugu zangu Wazanzibar kwa kumaliza uchaguzi salama, kwa kurudi na amani, sasa ni kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajielekeza kwenye hoja yangu, naomba sana kumshukuru Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa suala zima alilosimamia kuhusu kuonekana kwa Bunge *live*. Napata shida sana pale watu wanapong'ang'ania kuonekana kwenye *tv at least* ningekuwa nasimama mimi Mbunge mpya, mdogo niseme nionekane lakini kuna watu wana majina, nina mdogo wangu ana miaka sita anamjua Mbowe ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, sasa anang'ang'ania kuonekana kwenye *tv* ili iweje? Tukiachilia mbali hilo, tumeona sasa hivi Wabunge wa Upinzani wakisema hoja zao zikisikika. Kwa hiyo, naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Nape. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba kuzungumzia bajeti ya Waziri Mkuu na naomba nijielekeze kuzungumzia mustakabali wa vijana katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri Mkuu inasema utafiti wa mwaka jana vijana ni asilimia 59 hii inaonesha vijana ni kundi kubwa. Vijana hawa wanatakiwa kuwekewa mazingira mazuri, mazingira bora kwa sababu ndiyo nguvu kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ambao wamegawanyika katika makundi matatu, kuna kundi la vijana ambao wanamaliza elimu ya msingi wanashindwa kuendelea na elimu, hawapewi vitu vya kufanya na mbaya zaidi Wabunge wengi au watu wengi ndiyo wanaowachukua kuwafanya wafanyakazi wa ndani, hii inaumiza. Unajua suala la ajira inabidi tuliongelee kutoka moyoni, wewe unamuona ni binti ana miaka 13 anakuja kukuomba kazi za ndani unamwajiri na umesimama hapa Mbunge unasema ajira kwa vijana huu ni unyanyasaji. Tunapozungumzia ajira inabidi sisi wenyewe tuonekane kwamba suala hili sisi wenyewe halitufurahishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kuna suala linaniudhi sana, vijana wengi sasa hivi wanamaliza chuo kikuu *mashallah* unamkuta mtu amemaliza *degree* yake ya kwanza anaenda kusoma *masters* anafika hadi *Ph.D,* linapokuja suala la kupata ajira anaambiwa awe na *experience*, *experience* inatoka wapi. Usiponipa ajira ili nifanye kazi *experience* nitaitoa wapi? Suala hili linaumiza na naomba Wizara husika ilitilie maanani. Tunamwona Mheshimiwa Rais kawateua Wabunge ambao hawakuwepo katika mrengo wa kisiasa, wameteuliwa kuwa Wabunge wamekuwa Mawaziri na wanafanya kazi nzuri kwa nini hawa vijana tusiwape nafasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati yangu nilikuwa nazunguka sana naona wanakuja mainjinia, mimi ninamdadisi tu, baba shikamoo, hivi una muda gani hapa, mwanangu niko muda mrefu nina miaka 40 wakati kuna watu wamemaliza chuo, wanaweza, ni vijana wadogo hawapewi nafasi, wanawaacha tu walewale wa siku zote wanang'ang'ania zile nafasi. Si jambo zuri tuwape vijana nafasi waonyeshe uwezo wao.

Naomba Wizara iseme kama kila mwaka tunaajiri watu labda 500 katika hao asilimia 20 wawe ni vijana waliotoka vyuoni ili na wao waweze kupata nafasi, bila kuwapa nafasi hatuwezi kuona nguvu kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nataka kuzungumzia ni vijana wajasiriamali wapewe mikopo. Juzi nimeuliza swali Mheshimiwa Waziri kanijibu, lakini hawa vijana wajasiriamali ndiyo wengi wamejiajiri lakini mitaji yao

ni midogo. Naomba bajeti ya Wizara ione inaweza kuwasaidia vipi vijana wajasiriamali. Kama nilivyotangulia kusema awali niliomba hifadhi za jamii ziweze kujengewa uwezo ili vijana waweze kwenda kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine Mheshimiwa Rais aliagiza vijana wanaocheza *pool table* wachukuliwe na watafutiwe sehemu ya kupelekwa, hii imekuwa ni shida. Mheshimiwa Rais hakusema wale vijana wachukuliwe wapelekwe Polisi au watishiwe maisha maana sasa imekuwa tafrani. Lengo la Mheshimiwa Rais lilikuwa zuri kwani alisema vijana wale wachukuliwe watafutiwe kazi za kufanya kwenye mashamba makubwa ambayo watu wanayahodhi. Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watumie zile fursa wakimkuta kijana anacheza *pool table* wamchukue wamwambie heka yako moja hii hapa lima nyanya, naamini kijana umemfundisha analima, amepata faida shilingi milioni mbili hawezi kurudi kucheza *pool table*. Kinachoshangaza Maaskari wanawachukua wanawafunga na kwa kuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais anamwambia nipe hela nikuachie, wamefanya kama ni mtaji, kwa hiyo hili suala Wakuu wa Wilaya na Mikoa walisikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hili suala linaitwa *betting* maarufu kama mkeka sijui mnalijua suala hili, siyo vijana tu hata watu wazima wanaenda kucheza lakini hii ni kamari na hili ni bomu linalokuja kulipuka, likija kulipuka tutakuwa tumechelewa. Kijana kama mimi saa mbili asubuhi anaenda kucheza *betting*. Hao watu wa *betting* wanaenda kuomba leseni Halmashauri na wanapewa wanasema ni biashara, si biashara inaua nguvu kazi za vijana. Naomba wahusika walifuatilie kwani siyo suala zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba kila Halmashauri huwa zinatenga asilimia tano kwa ajili ya vijana. Halmashauri nyingi hazitengi asilimia hiyo. Nilikuwa nashauri Serikali iwape hati chafu kila Halmashauri ambayo haitatekeleza jambo hili ili kuwalazimisha kufanya kile kinachotakiwa kupeleka asilimia tano kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba Wizara katika bajeti hii Mfuko wa Maendeleo ya Vijana uongezewe uwezo. Kwa kufanya hivyo itarahisa pesa kufika kwa vijana kiurahisi zaidi na kuwawezesha kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho kabisa naomba kuzungumzia hili agizo tena la Mheshimiwa Rais kwa Serikali za Mitaa kutenga maeneo maalum yaani hili suala mimi linanikera.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewashuhudia Mapolisi wanawakuta vijana wengine wamekaa tu mtaani wanakamatwa, Mheshimiwa Rais kaagiza watu hawatakiwi kuonekana, Mheshimiwa Rais tusimchonganishe na wananchi, tusimchonganishe na vijana. Wakuu wa Mikoa na viongozi wengine yale

mashamba wanayohodhi wao kama wao watumie fursa zile kuwapa vijana ili waweze kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii leo ya kuweza na mimi kuchangia.

Awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanahu Wataala,* aliyenijalia uwezo na *satwa* ya leo kuwa mimi Asha Abdullah Juma kuwa Mbunge na kuweza kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi ya kwanza kabisa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuweza kuwa Rais na kuongoza kwa *speed* hii ambayo anakwenda nayo, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana.

Vilevile nachukua nafasi ya kipekee kupongeza hatua iliyochukuliwa na chama chetu ya kuweza kumpendekeza Mheshimiwa Samia Sukuhu Hassan akawa Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Napongeza pia uteuzi wa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, anao uwezo wa hali ya juu sana na anakubalika na tuna matumaini atafanya kazi nzuri sana. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi hii, nawapongeza pia wale waliopata nafasi ya Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa nampongeza Mheshimi Dkt. Ali Mohamed Shein kuwa Rais wa Zanzibar na kwa kushinda uchaguzi. Mheshimiwa Ally Saleh nakuona hapo, nakuambia kwamba Mheshimiwa Dkt. Shein ndiyo Rais wa Zanzibar na amechagua *cabinet* nzuri naamini itamsaidia kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Kwa kupitia Bunge hili, nilaani kitendo alichofanyiwa Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein cha kuzomewa lakini lile halikumrudisha nyuma yeye ameendelea kuwa Rais wa Zanzibar kwa kura nyingi na sisi tunamuunga mkono kwa sababu ndiye tegemeo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kitu kimoja, hii tabia ya kususasusa si nzuri, tabia ambayo inaoneshwa hapa kwa sababu inavunja demokrasia.

**MBUNGE FULANI:** Nani amesusa?

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Anajijua mwenyewe aliyesusa. Inavunja demokrasia, watu wamewachagua mje hapa muwawakilishe, muisemee Serikali au muikosoe, mnakuja hapa kisingizio hiki, kile, mara kutoka nje, mara uzomee, mara unune, mara ugome, sasa ndiyo umechaguliwa kwa ajili hiyo? Ilimradi hakuna lililo zuri kwa upande wenu. Usichukue mshahara wa kutwa bila kufanya kazi ya kutwa. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Baniani mbaya ila kiatu chake dawa. Mshahara, posho yote mazuri mbona hamyakatai? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha…

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo, sasa niende kwenye hoja.

**MBUNGE FULANI:** Wewe bibi au kikongwe wewe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha naomba ukae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu mia juu ya mia.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Heshima kitu cha bure.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni wazi ukiwa umekaa eneo kama hili unaona upande unaoshangilia na upande unaozomea. Sasa naomba tuwe watulivu, mtu anayepewa nafasi ya kuchangia anaweza kuzuiwa kwa mujibu wa Kanuni siyo kwa kuzomea. Kwa hiyo, kama mtu ana taarifa tofauti asimame ampe Taarifa, kama mtu anaona utaratibu unavunjwa asimame aniombe nimpe nafasi atoe utaratibu, sio kuzomea. Sisi wote hapa ni watu wazima, tuheshimiane na wote kwa sababu tumeamua kubaki humu ndani kwa ajili ya

zoezi hili tuliache hili zoezi liende sawasawa. Mheshimiwa Asha endelea. *(Makofi)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba pia unilindie muda wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuchangia kwanza kwa kupongeza safu nzima ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba niseme kwamba kwenye Ofisi yako ukianzia na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi na Mheshimiwa Anthony Mavunde, hawa ni vifaa, tumewapima kupitia Kamati yetu ya Katiba, wanafanya kazi nzuri sana. Naamini watatusaidia sana kwa maendeleo husika katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze rasmi na naanza na eneo la Tume ya Uchaguzi. Naanza kwa kupongeza kazi nzuri iliyofanywa na Tume ya Uchaguzi kuanzia Mwenyekiti wake Jaji Lubuva…

**MBUNGE FULANI:** Jecha.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Kailima na Jecha pia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii ya Uchaguzi imethibitisha demokrasia, kama tulivyoona vyama 22 vimeshiriki na vimeshinda vingine na sasa hivi tupo hapa kuwawakilisha wenzetu. Hivyo, ukipata wapiga kura waliofikia 15,596,110 sawasawa na 67.3% ni hatua nzuri. Tuiombe Serikali iiongezee Tume ya Uchaguzi nguvu ili kudhibiti wizi wizi na vitendo vya kuivurugia kazi Tume hii ambayo inafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka kuligusia ni hili linalohusu vijana ambalo kwenye hotuba hii limezungumzwa vizuri la kuwapatia mafunzo. Tunajua vijana wanatuzidi kwa namba, ni wengi, kwa hiyo inahitajika mikakati na imara zaidi ya kuwahusisha ili wasitutoke wakawa kundi la wanaofanya vurugu na fujo. Kwa hiyo, mipango hii iliyopangwa nafikiri ingekuwa vizuri pia ikaelezwa waziwazi kila Wilaya watapata mafunzo kiasi gani na mafunzo gani ili kujua hawa watu wanashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nalotaka kuligusia ni hili la bandari. Tumeridhishwa na mpango ulioelezwa hapa lakini tuongeze kuoneshwa kwamba kunaongezwa vifaa vya kisasa zaidi ili kuharakisha upakizi na upakuaji na pia kudhibiti bila kutumia nguvu zaidi na pesa nyingi huu uvujaji na wizi katika bandari zetu. Pia nadhani kama ingekuwa vizuri kwenye eneo hili la bandari kukaimarishwa masuala ya uokoaji inapotekea *disaster* katika maeneo ya bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jicho pia liongezwe katika kuimarisha bandari ya Mtwara na Tanga. Naona kama hii mipango iliyopangwa haijatosha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali hii ione umuhimu huo na hasa kwa vile kule Mtwara tuna mategemeo ya kupata shughuli nyingi za kupokea na kusafirisha mizigo. Kwa hiyo, ni vyema jitihada ikaongezwa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine la muhimu kabisa ambalo linatakiwa lipewe nguvu ya ziada ni elimu. Pongezi pia kwa Serikali kwa kuweza kuboresha elimu ya awali. Naomba tuendelee kuunga mkono juhudi hizi, kama tulivyofanya kwa kutenga pesa tukaziweka kwenye madawati hivyo na kila anavyofikiria mtu kuna namna nyingine ya kufanya ili kuweza kuiboresha elimu hii basi na tufanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kuwepo katika Bunge hili. Haikuwa rahisi lakini kwa uwezo wake leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu napenda sana niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi, kwa kuchagua kwa kura nyingi viongozi wanaotokana na CCM. Wamempa kura nyingi Mheshimiwa Rais, lakini wamechagua Wabunge wote wanaotokana na CCM, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niahidi mbele yako kwamba nitashirikiana na Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wanaotokana na CCM nikiamini kwamba wao wamechangia uwepo wangu katika Bunge hili. Ninaahidi kufanya nao kazi hasa zinazohusu akina mama usiku na mchana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijaendelea kusema niunge mkono hoja, lakini nianze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba nipongeze sana hotuba hii imekaa vizuri lakini kwa kuwa ni wajibu wetu kusema neno na mimi naomba niseme neno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la shilingi milioni 50 za kila kijiji. Sote tunafahamu kwamba Mheshimiwa Rais wetu alitoa ahadi kwa

wananchi wetu kwamba Mwenyenzi Mungu akimjalia kushinda katika nafasi hii…

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani, naomba ukae.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1), mchangiaji anayechangia sasa hivi anasoma kinyume na utaratibu. Kwa hiyo, naomba meza yako impatie utaratibu wa jinsi ya kuchangia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani…

**MBUNGE FULANI:** Si mmesema hamuongei?

**MBUNGE FULANI:** Wabunge hewa.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie kwamba miongoni mwa mabingwa wasemaji bila kusoma ni pamoja na mimi. Naomba nimhakikishie hilo na ili kuthibitisha naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia shilingi milioni 50 ambazo Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kwa wananchi wetu. Namuomba awe anaangalia ahakiki kama hapa nilipo sisomi ili kumthibitishia kwamba niko vizuri na sina shaka, nimepikwa nikapikika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu wakati anaomba kura alitoa ahadi ya kutoa shilingi milioni 50 kila kijiji na mimi napongeza ahadi hii na sina shaka ahadi itatekelezwa na kwa bahati nzuri kwenye hotuba ya Waziri Mkuu imeelezwa. Kwa kuwa zoezi hili la ugawaji wa hizi pesa wamesema watahakikisha zinatolewa kupitia *SACCOS* na baada ya utaratibu huu kukamilika kinachofuata sasa ni utekelezaji. Nashauri kabla hatujafika kwenye hatua ya utekelezaji maelekezo yatolewe kwa wananchi wetu ya namna njema ya upatikanaji wa pesa hizi ili kusitokee mkanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo mbele ya Bunge lako kwa sababu hivi tulivyo hapa kule vijijini tayari akina mama wanaendelea kuchangishana pesa na kufungua akaunti. Inawezekana kabisa wakafungua akaunti lakini mwishoni mtu akajikuta hapati kile alichokusudia. Kwa hiyo, naomba yatolewe maelekezo wakati tunaingia kwenye utaratibu huo kila

mmoja anajua vigezo gani vitatumika vya kutoa hizi pesa. Sina shaka na Serikali yangu, naamini watatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia pia masuala ya Mfuko ule wa *TASAF*. Mheshimiwa Waziri Mkuu atakubaliana na mimi kwamba jambo hili ni jema na kwa kweli linasaidia kaya maskini na kwa bahati nzuri wameelezea kaya ambazo zimenufaika na kiasi ambacho kimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile ambavyo tunahakiki watumishi hewa, naomba na katika eneo hili turudi tuhakiki wanufaika. Kwenye eneo hili kuna watu ambao wananufaika lakini siyo maskini kama vile ambavyo tumekusudia. Kwa hiyo, inawezekana kabisa jambo likawa jema lakini lisilete manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Ofisi ya Waziri Mkuu kama vile ambavyo tunahakiki watumishi hewa basi na kwa upande wa *TASAF* kwa kuwa tumekusudia kusaidia kaya maskini, twende tusaidie kaya maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la ugawaji wa maeneo ya utawala. Kama nilivyosema kwamba mimi natokea Mkoa wa Ruvuma lakini naomba niizungumzie Wilaya ya Tunduru. Wilaya ya Tunduru ni miongoni mwa Wilaya kongwe katika nchi hii, ina Kata 39 na Majimbo mawili. Tumezungumza kwenye vikao vyetu na tumeomba kupata Wilaya nyingine. Niombe kupitia ofisi yake wakati utakapofika basi waiangalie na Wilaya ya Tunduru kwa kuiweka katika mgawanyo ule wa kuongeza Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri huwa tunaongeza maeneo ya utawala kwa ajili ya kurahisisha kutoa huduma kwa wananchi wetu. Kwa dhati ya moyo wangu na kwa bahati nzuri Waziri Mkuu ni msikivu na naamini pale alipo Waziri Mkuu ananisikia, wakati utakapofika wataangalia na kuipa umuhimu Wilaya ya Tunduru. Wala hapigi *story* Mheshimiwa Waziri Mkuu pale ananisikiliza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la asilimia 10 ya mikopo ya wanawake na vijana. Kwenye eneo hili wachangiaji wamesema kwamba utaratibu wa siku za nyuma tulikuwa tunaziagiza Halmashauri zetu zitenge asilimia 10 kwa ajili ya kusaidia mikopo ya wanawake na vijana. Mimi naomba ukubaliane na mimi kwamba yako maeneo hayafanyi vizuri. Naomba sana sana tusisitize Halmashauri zetu zitenge hizi pesa kwa ajili ya kusaidia wanawake na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi ya kusema lakini naomba niseme mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Wewe utakuwa shahidi, Kamati ya UKIMWI imewasilisha taarifa yake hapa, miongoni mwa

mambo ambayo tumekuwa tukiyajadili kwenye vikao vyetu ni kwamba utaratibu wa uendeshaji wa Bunge hauna tofauti sana na utaratibu wa uendeshaji wa Halmashauri. Utakubaliana na mimi kwenye Halmashauri zetu Kamati hizi haziko kama zilivyo kwenye Bunge. Tulileta maombi kwako, tulikaa na wewe, nikubali inawezekana kabisa kabla sijawa Mjumbe wa Kamati pengine nilikuwa sijajua ugumu na tatizo kubwa lililopo la dawa za kulevya na UKIMWI lakini nilipokuja kwenye Kamati hii nimeona kwamba hili tatizo ni kubwa na Wajumbe wenzangu watakubaliana na mimi kwamba ni tatizo kubwa. Tumewasilisha hapa bajeti yetu, tutaomba Bunge liridhie kwa kile ambacho tumeomba na wakati utakapofika basi kitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaomba kwa heshima na unyenyekevu na tunaamini nyie viongozi mlioko mbele ni sisi ndiyo ambao tumewaweka na kiongozi msikivu ni yule anayesikia kilio cha watu anaowaongoza, tunaomba sana Kamati hii irudi kwenye mfumo uliokuwepo huko nyuma ambapo Wajumbe wa Kamati hii walikuwa wanapata nafasi ya kushiriki kwenye Kamati nyingine. Wanakuwa na nafasi ya kwenda kuzungumzia masuala ya barabara, maji, zahanati lakini leo sehemu kubwa sisi ni ku-*deal* na masuala ya maboksi ya *condom,* masuala ya dawa za kulevya na uingizaji wa vidonge hivi vinavyowasaidia wenye UKIMWI. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikuombe kwamba katika eneo hili, naamini wewe ni msikivu na Spika ni msikivu na wote nyie ni wasikivu na mmekaa hapo kwa ajili ya kusikiliza kilio cha watu mnaowaongoza na sio wengine ni pamoja na sisi Wajumbe wa Kamati hii, tuko tayari kufanya kazi. Kwa nafasi hii naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama lakini nimpongeze na Naibu wake wametupa ushirikiano sana, pale tulipowataka kwenye Kamati yetu wamekuja wametupa maelezo, niombe sana mliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini liko tatizo lingine la *MSD*. Tumefika sisi mpaka *MSD* wanadai pesa na inawezekana kabisa itafika wakati watashindwa kabisa hata kupakua mizigo bandaraini. Kuna pesa ambayo wanaidai Serikalini na kwa bahati nzuri Naibu Waziri wa Afya tulikuwa naye wakati tumeenda *MSD* na yeye aliahidi kwamba kile kiasi cha pesa kitatolewa. Niombe watekeleze ahadi yao ya kuwalipa *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. Nawatakia kila la kheri na kazi njema, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama katika hili Bunge Tukufu kuzungumzia kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza ndani ya Bunge hili, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Dodoma kwa kunichagua na kunifanya niwe Mbunge wao. Sambamba na hilo niwashukuru pia wanaume wa Mkoa wa Dodoma kwa kuwaruhusu wake zao na watoto wao kuweza kuja kunichagua kwa hiyo, nawashukuru sana wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyoitoa. Nalipongeza pia Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuzungumzia kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 73 ambao ulikuwa unazungumzia suala la Ustawishaji Makao Makuu. Naamini sote tunafahamu kwamba suala la Ustawishaji wa Makao Makuu lilianzishwa mwaka 1973 lakini kwa masikitiko makubwa sana mpaka leo hii hakuna sheria ambayo inazungumzia uwepo wa Makao Makuu Dodoma. Kukosekana kwa sheria hiyo imechelewesha sana kuhamia Makao Makuu Dodoma. Pamoja na taarifa nzuri ambayo imetolewa kwamba kuna baadhi ya mambo yamepangwa katika Ustawishaji Makao Makuu, lakini kumbe ipo sababu ya msingi kabisa ya kutungwa sheria ambayo itaharakisha Makao Makuu yawe Dodoma na Ofisi ziweze kuhamia Dodoma, hatimaye Mji Mkuu wa Tanzania yetu uwe Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niwakumbushe tu kwamba wenzetu Nigeria walibaini kwamba wanatamani wapate Mji Mkuu mpya mwaka 1976, wakajitahidi *by* mwaka 1991 wakaweza kufanikiwa kuhama kutoka Lagos kwenda Abuja. Sisi tangu mwaka 1973 mpaka leo mwaka 2016 bado hatujaweza kuhamia Dodoma. Kwa kweli hili jambo inabidi zichukuliwe hatua za uhakika kuhakikisha kwamba sheria hii inatugwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa sheria ya kutambua kwamba Dodoma ni Makao Makuu utasaidia sana kwa sababu kuna muingiliano mkubwa sana wa utendaji kati ya Manispaa pamoja na hii Mamlaka ya Makao Makuu. Kwa hiyo, naamini kwamba ukiwekwa mkazo wa uhakika kutungwa kwa hii sheria utasaidia kabisa kutofautisha kazi kati ya Manispaa pamoja na hii Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni kwamba uwepo wa sheria ile utasaidia kuharakisha kuwa na uwekezaji katika Mkoa wetu wa Dodoma. Kwa kweli katika Mkoa wa Dodoma, miaka ya nyuma kulikuwa na baadhi ya viwanda kwa mfano, Kiwanda cha Coca-cola lakini tunashangaa kiliondoka vipi, kulikuwa kuna Kiwanda cha Mvinyo bahati mbaya kikafa, kulikuwa kuna Kiwanda cha Magodoro, tunaona tu Magorodo Dodoma lakini magodoro yale hayatengenezwi hapa Dodoma.

Kwa hiyo, naamini kabisa kama ukiwekwa mkazo na naamini katika Bunge hili tutahakikisha sheria hii inatungwa basi uwekezaji utaweza kupata tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili kupunguza mwingiliano wa kazi kati ya Manispaa pamoja na *CDA*, ikiwezekana kiundwe chombo kimoja tu ambacho kitasimamia ustawi na upimaji wa mipango miji katika Mkoa wa Dodoma kwa sababu Manispaa wanafanya shughuli hizohizo ambazo zinafanywa na *CDA*. Kama sheria itaweka chombo kimoja ambacho kitasaidia sasa kufanya mambo yote ya mipango miji, naamini kabisa itasaidia ustawishaji na hatimaye Makao Makuu yanaweza yakaja Dodoma lakini kubwa zaidi ni suala la sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie pia suala la miundombinu. Katika Mkoa wetu wa Dodoma pamoja na kwamba mji umepangwa vizuri lakini kuna maeneo tofauti tofauti kwa mfano maeneo ya *Area C,* Nkuhungu, Medeli na maeneo mengine mapya ambayo yameanza kujengwa, zile barabara za ndani za mitaa hazipo, mvua zikinyesha kwa kweli kunakuwa na adha kubwa sana kwa wananchi. Kuna maeneo ambapo mashimo ni makubwa sana, kuna maeneo mifereji iliyopo sio mifereji ambayo inaweza ikasaidia kupitisha maji, kwa hiyo inaleta madhara makubwa sana. Kwa kuwa Waziri Mkuu yupo hapa na analisikia sheria hii ikitiliwa mkazo naamini kabisa mambo mengi yanaweza yakafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisisitiza ni kuhusu *sewage system* katika huu Mkoa wa Dodoma. Kuna maeneo ni kweli imejengwa *sewage system,* lakini maeneo mapya ambayo Ustawishaji Makao Makuu wameyaweka *sewage system* bado sio nzuri. Kwa hiyo, tunaomba na jambo hilo lifikiriwe kwa ajili ya afya ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nililokuwa nataka nilizungumzie ni kuhusu uwanja wetu wa ndege katika eneo la Msalato. Ninaamini kabisa kwamba uwanja huu uko katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini bado sijaona hatua za haraka au zinazoenyesha kwamba uwanja huu unaweza kujengwa haraka. Kwa sababu uwanja huu kwa kweli utakuwa una tija sana kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma lakini pia na wananchi wengine wote wa Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, nimeona na hilo nalo nilizungumzie ili uwanja huo nao uweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba katika Mkoa wa Dodoma kuna eneo karibu kama kilometa nane kutoka pale Chuo cha Mipango bado halijawekwa lami. Kwa kweli imekuwa ni kero sana kwa wananchi na wamekuwa wakiilalamikia sana Serikali kwa kuona ukimya uliopo kwa sababu limekuwa la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naamini kabisa katika bajeti hii nalo litatiliwa mkazo ili kusudi eneo lile liweze kuwekewa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu suala la maafa na majanga na hasa kwenye janga la moto. Tumekuwa tukisikia matukio mbalimbali kuhusu janga la moto lakini bado nchi yetu haina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kukabiliana na janga hili. Kwa hiyo, niombe Serikali waone ni utaratibu gani tunaoweza kuufanya walau wa kuweza kupata magari na vifaa vya uokozi wa moto katika kila Wilaya ili kusudi inapotokea dharura yoyote ya moto waweze kupata fursa ya kuweza kuzima huo moto kwa sababu wananchi wengi sana wamekuwa wakipata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi wameyazungumza wenzangu kuhusu masuala ya afya, maliasili na kadhalika lakini naomba tu nizungumzie kidogo kuhusu suala la Bima ya Afya au *CHF*. Wenzangu wamelizungumza na mimi naomba nitoe msisitizo, hebu Serikali ione kwa sababu hii asilimia 27 ya wachangiaji ni asilimia ndogo sana, bado tuna sababu ya msingi sana ya kuhamasisha wananchi ili kusudi waweze kujiunga na huu Mfuko wa *CHF* kwa sababu una tija sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kushangaza sana Watanzania wenzangu hatuko makini sana kuchangia masuala mbalimbali ya kimaendeleo. Watu wako makini sana kuchangia harusi na sherehe mbalimbali, lakini kwenye suala afya inaonekana watu hawana mwamko. Nitoe shime kwamba na sisi viongozi tulifanyie kazi suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, ajiandae halafu wengine tutawasoma kama muda utaruhusu.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Awali ya yote, nipende kumshukuru Mwenye Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, lakini pia nipende kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa

Pwani kwa kuniamini niweze kuja kuwawakilisha. Sambamba na hilo, napenda niwashukuru wanawake wa CCM Taifa na Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniteua Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naelekea kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, napenda kutoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na timu yake ya Baraza la Mawaziri inayoongozwa na Jemedari Mkuu, Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo inavutia moyoni mwa Watanzania, kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo inaleta furaha katika macho ya Watanzania. Hakika Mungu mbariki Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza lake la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kwa kuanza ukurasa wa saba. Katika ukurasa wa saba hotuba hii inajielekeza katika namna ya kuchukua hatua kuhakikisha wanaongeza mapato na wanabana mianya ya ukwepaji kodi. Mimi nipende kuunga mkono jitihada hizi, ni jambo jema sana na *I believe for sure* kama tuna uwezo wa kukusanya hata zaidi ya shilingi trilioni 1.3 endapo *TRA* itajizatiti kweli kweli lakini pia kila Mtanzania atimize wajibu wake, anayepaswa kulipa kodi alipe kodi, tudai risiti tunapofanya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuelekea kuongeza mapato kama ambavyo Serikali imedhamiria tuna shida moja, *EFD* mashine bado kuzungumkuti. Suala zima la *EFD* mashine ni tatizo. Nimeshashuhudia nimepata risiti za aina tatu tofauti pale unapofanya manunuzi. Kuna risiti ambayo unakuta ina maelezo ambayo kwa mtazamo wangu mimi naweza kusema yamejitosheleza. Kuna *TIN* namba pale, utakuta jina la ile kampuni ama kile kituo cha kufanyia biashara, kuna *VRN* pale lakini pia utakuta jumla ya *amount* uliyonunua, muda, tarehe pamoja na ile *amount* inayokuwa *deducted* kwenda Serikalini, lakini zipo risiti nyingine zinazotoka katika hii mashine unakuta zina *lack* hizo *details.* Kwa hiyo, naomba sana hili suala la *EFD* mashine tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia baadhi ya wafanya biashara hawana hizi mashine, wanaendelea kutumia risiti za kuandika. Niseme kwamba hizi risiti siyo afya sana katika ongezeka la ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimewahi kwenda *petrol station* kuweka mafuta, nimeweka saa tatu asubuhi lakini risiti inaniandikia nimeweka saa tano usiku. Kwa hiyo, inaonekana kwamba hizi mashine watu wanaweza kucheza nazo. Kwa sababu hiyo, nasisitiza tena tuziangalie mashine hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye *petrol station* kuna matatizo makubwa sana ndiyo maana nasisitiza *TRA* inabidi ijizatiti au ifanye kazi kweli kwenye hili suala la ongezeko la mapato. Utakuta kuna visima viwili, cha dizeli na petroli, vya dizeli viwili na vya petroli viwili, kimoja ni cha risiti ya kuandika na kingine ni cha risiti ya *TRA*. Kwa hiyo, naomba sana katika suala hilo mnaohusika mliangalie kwa ukaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mchango wangu mwingine uko katika ukurasa wa 16 ambao unazungumzia shilingi milioni 50 katika kila kijiji lakini pia umeelezea maandalizi ya namna fedha hizi zitakavyowafikia walengwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha vikundi vya kiuchumi vinavyokidhi vigezo. Hii ni ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo unaikuta katika Ibara ya 57(d) kwa ruhusa yako naomba nikisome na kinasema; "kutenga kiasi cha shilingi milioni 50 katika kila kijiji kama mfuko wa mzunguko *(revolving fund)* kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wajasiriamali kupitia ushirika wa kuweka na kukopa (*SACCOS)* katika vijiji husika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kampeni kilichokuwa kinawavuta Watanzania wengi ni pamoja na kifungu hiki cha 57(d) cha shilingi milioni 50 katika kila kijiji. Ukiangalia muktadha wa hiki kifungu hizi shilingi milioni 50 siyo kwamba watu watagawiwa, watakopeshwa *then* watarudisha. Wakati wa ziara yangu ya kushukuru wapiga kura wa Mkoa wa Pwani nilipata maswali kutokana na kifungu hiki, wazee wanauliza wao watanufaika vipi na kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi wazee ambao wameshafika umri wa kushindwa hata kufanya kazi huoni moja kwa moja kama kinaweza kuwanufaisha. Isipokuwa naomba Serikali masuala mazima ya mapendekezo ya *universal pension, pension* kwa wazee wote yaweze kufanyiwa kazi kwa haraka ili yaende sambamba na hii shilingi milioni 50. Wakati watu wenye nguvu zao wananufaika na hii shilingi milioni 50 kukopa na kufanya biashara ama ujasiriamali basi wazee waweze kunufaika na *pension* ya wazee wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine uko ukurasa wa 23 ambao unazungumzia suala zima la kazi na hifadhi ya jamii. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo inaelezea mwelekeo wa shughuli za Serikali, nilitarajia kuuona hapa Mfuko wa Fidia *(Workers Compensation Fund – WCF)*. Sikukuu ya Mei Mosi mwaka jana kati ya mambo ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi alifafanua na kueleza kwamba kati ya mafanikio ya Serikali yake basi ni pamoja na kuanzishwa kwa *Workers Compensation Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nipende kusema na niwe mkweli na utakubaliana na mimi kabisa kati ya kitu ambacho Serikali ya Awamu ya Nne imefanya kwa wafanyakazi wa Taifa hili basi ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa

Fidia Kazini. Ikumbukwe hapo awali ilikuwa inatumika sheria ya zamani, Sheria ya Fidia, Sura Na.263 ambapo mtumishi akiumia kazini, akipoteza kiungo alikuwa analipwa shilingi 108,000 kwa upande wa wafanyakazi wa *private* lakini kwa upande wa wafanyakazi wa *public sector* ilikuwa inatumia Sheria ya *Public Service Act* ambayo mtumishi akiumia ama akipoteza kiungo ama ulemavu wa maisha alikuwa anapewa shilingi milioni 12 na yenyewe ilikuwa inatolewa *once*.

Kwa hiyo, naomba sana Waziri Mkuu na Waziri mwenye dhamana ya kazi na hifadhi ya jamii kuuangalia mfuko huu kwani umeelezea namna njema ya kuwafidia wafanyakazi wetu wanapoumia ama kupoteza viungo sehemu yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda tena kujikita ukurasa wa tano wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao unazungumzia uwajibikaji na maadili ya viongozi wa utumishi wa umma. Baadhi ya watumishi wa umma walifika mahali walijisahau sana, lakini pia baadhi ya watumishi wa umma wasiokuwa waadilifu hao ndiyo walikuwa wameigharimu Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, Serikali yetu ya Awamu ya Tano imeamua kuchukua hatua ku-*deal* na hawa watu ambao walikuwa hawana uadilifu wametumia madaraka yao vibaya ama wametumia nafasi zao vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza wenzetu hawa hawa waliokuwa wanapigia kelele kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inachelewa kuchukua hatua leo wamekuwa mstari wa mbele kutetea wabadhirifu, wamekuwa mstari wa mbele kutetea mafisadi, wamekuwa mstari wa mbele kutetea watumishi ambao hawana maadili. Wamekuwa vigeugeu, ni wao ndiyo waliokuwa wanasema tunaenda taratibu, sasa tunaondoka na *supersonic speed*, wanatoka tena mbele na kuanza kuwatetea wale watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine…

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Wafuate sheria.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Muache atoe taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Chakoma naomba ukae, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**TAARIFA**

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba sisi kama Kambi ya Upinzani tunasema kwamba siyo watumishi wote wa umma wako salama, wako ambao kweli wana makandokando mengi lakini tunachotaka ni taratibu za kisheria zifuatwe. Kwa hiyo, nampa taarifa hii aelewe siyo anapotosha hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Chakoma taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siipokei, mimei-*shred. (Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutende haki, inavyoonekana ni kama tunajikanyaga vile, Kiongozi wa Upinzani Bungeni anatakiwa atumbue majipu ambayo hayamsikilizi, ameagiza watu wasiseme lakini wanaendelea kusema. Wakipigwa sindano wanasimama wanasema, tuwahesabu wanachangia au wanavuruga michango wa Wabunge wengine?

Mheshimiwa Mbowe tumbua majipu, hapa kuna majipu kwenye Kambi yako, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza, naomba kukumbusha Taarifa na pia Kuhusu Utaratibu unapaswa kuitaja Kanuni unayoongelea. Naomba tusikilizane, Mheshimiwa Heche tafadhali, naomba tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukumbusha hilo, Mheshimiwa Heche, naomba uheshimu Kiti.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Naomba uheshimu Kiti Mheshimiwa Heche.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukumbusha hilo, utaratibu alioomba Mheshimiwa Lusinde nadhani nilishatoa maelezo asubuhi kuhusiana na hiki walichokiomba Kuhusu Utaratibu na kwa kuwa wako humu ndani wanaweza kuomba utaratibu. Mheshimiwa Chakoma, endelea. *(Makofi)*

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema kwamba taarifa yake siipokei nimei-*shred,* lakini pia nipende kumkumbusha anaweza akaenda *YouTube* akaona Mwenyekiti wao Mbowe analalamika watumishi wa umma ambao wanasimamishwa anataka wahojiwe kwanza, tayari TAKUKURU imeshatoa ushahidi, anahojiwa kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda ukurasa wa tisa unaozungumzia kukua na kuimarika kwa demokrasia. Nchini Tanzania demokrasia imekuwa na ndiyo maana kuna uwepo wa vyama vingi. Pia niseme tunatambua uwepo wa upinzani nchini, tunatambua uwepo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na tunatambua chama kikuu cha upinzani. Wakati tunaelekea kwenye mustakabali wa kuwafanya Watanzania wawe na maisha bora, ukiacha kazi nzuri inayofanywa na Chama Tawala ama na Serikali, pia tunahitaji mchango makini kutoka kwa chama cha upinzani ama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Kama tunakuwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo kwanza haiko makini, mbili inaendeshwa na mihemko, tatu inaendeshwa na sintofahamu, hatuwezi kufika mahali kokote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Chakoma umemaliza muda wako.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, Kanuni ya 68(9).

**NAIBU SPIKA:** Naomba tuendelee, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Muda wangu umekwisha, Taarifa iko wapi?

**MBUNGE FULANI:** Umekwisha.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, napenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kavuu, kwa kuniamini na mimi nawaambia sitawaangusha tuko pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 15, uwezeshaji wananchi kiuchumi. Katika hili, napenda kwanza niishukuru Serikali yangu kwa kuweza kuanzisha *VICOBA* na *SACCOS* ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kuinua pato la wananchi. Pia napenda nishukuru Chama changu cha Mapinduzi katika Ilani yake ilipokuwa inajinadi kuanzisha mfuko wa shilingi milioni 50 katika kila kijiji. Katika hela hizi kutokana na namna tulivyokuwa tunajinadi, basi ziende zikatumike hivyo, kwa makundi mbalimbali ndani ya kila kijiji ambavyo vitakuwa vimesajiliwa na Halmashauri na kutambuliwa kisheria. Kwa sababu tunaelewa katika makundi ya vijana na

akina mama tuna asilimia 10 ya kila mapato ya Halmashauri. Kwa Halmashauri ambazo hazifanyi hivyo basi Serikali isimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende ukurasa wa 25 kuhusu Hifadhi ya Mifuko ya Jamii. Mifuko hii imekuwa na michango mikubwa katika shughuli za maendeleo katika kuendeleza Taifa letu kiuchumi. Niwaombe na niiombe Serikali, kwa sababu tumekuwa tunawahimiza wananchi wajiunge na Mifuko ya Bima ya Afya na kwa sababu hii Mifuko ya Bima ya Afya inachangia katika maendeleo ikajenge zahanati kwenye vijiji, ikatusaidie hata kupata vifaa tiba katika zahanati zetu na vituo vya afya. Kwa nini natamka hivyo? Hii itatusaidia kujenga imani kati ya wananchi na hii mifuko na hivyo itakuwa rahisi kwa wananchi kujiunga na mifuko hii kwa sababu wataona wananufaika, wataona faida yake na watajiunga kwa urahisi. Kwa hiyo, niwaombe *NHIF* watusaidie kuwekeza katika zahanati zetu na vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la mifugo hususani suala la migogoro, nafikiri Serikali imepokea malalamiko mbalimbali kutoka katika kila Jimbo kuhusiana na migogoro ya ardhi. Naongelea katika Jimbo langu kuhusiana na migogoro inayojitokeza kati ya wafugaji na mipaka ya Hifadhi ya Taifa hususani Hifadhi ya Katavi. Migogoro imekuwa ikiwasilishwa mara kwa mara. Serikali hii nafahamu ni makini kweli kweli na inafanya kazi kweli kweli na Mbunge mwenyewe Kikwembe anafanya kazi kweli kweli, kutokana na namna tulivyojipangia kutatua hii migogoro, niombe sasa baada ya Bunge hili, baada ya Bajeti, Serikali ikaanze kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji, kati ya wananchi wanaoishi mipakani na Hifadhi za Taifa, tuondokane na kero hii ili tuweze kufanya shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niongelee suala la uwekezaji kwa wananchi. Tunakuwa na uwekezaji mzuri ambao unalenga kukuza pato la mwananchi. Napenda niongelee uwekezaji katika masuala la mawasiliano. Mawasiliano ni kitu cha msingi sana, napenda niishukuru Serikali yangu kutoka awamu iliyopita mpaka hii tuliyonayo kwa kuwezesha mawasiliano vijijini kupitia mtandao wa *Halotel*, Mkoa wa Katavi sasa hivi tuna 100% ya mawasiliano. Ninachopenda kusema tumekuwa na migogoro kati ya wawekezaji hasa wanapokwenda kuweka minara. Nafahamu *Halotel* imekuja kutatua tatizo ambalo makampuni mengine yalishindwa kwa sababu yanajiendesha kibiashara zaidi lakini *Halotel* wamefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kupunguza matatizo ambayo yanajitokeza hivi sasa kati ya wawekezaji hawa wa *Halotel* na wananchi katika maeneo husika, waweze kuangalia namna watakavyoweza kutoa zile tozo. Siamini kabisa kwamba hawa *Halotel* wanatoa huduma bure na sisi tunalipia hizo huduma.

Kwa hiyo, huu mpango wa kusema shilingi 30,000 kwa mwezi katika eneo husika, kwa kweli bado si sahihi, naomba Serikali waliangalie hilo. Pamoja na kwamba wametusaidia kiasi cha kutosha na nawapongeza sana Serikali kwa kuwaleta hawa Wavietnam ambao wamekuwa mkombozi katika mawasiliano vijijini lakini naomba tuangalie upya hizo tozo kuondoa migongano kati yao na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee upande wa barabara. Naishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Bunge lililopita Mheshimiwa Rais alikuwa Waziri wa Ujenzi. Amejitahidi kwa kadiri ya uwezo wake, tumepata pesa ya kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mpanda – Tabora. Wananchi wa Katavi, Tabora na Kigoma kwa ujumla tunasema ahsante.

Kama ilivyokuwa kwenye mipango ya Serikali iliyopita ya kutengeneza barabara ya lami kutoka Majimoto - Inyonga naomba iwemo ndani ya bajeti kwani sijaiona na Daraja la Kavuu sijaliona na liko kwenye mpango. Kwa hiyo, niombe sana wazingatie kuweka kwenye bajeti hii mipango iliyokuwepo kipindi kilichopita. Si kwa Jimbo la Kavuu tu ambalo ni jipya, niombe katika Majimbo yote mapya, tuwekeeni hata barabara za vumbi ambazo zinapitika kwa kuanzia si haba tofauti na ambavyo hatuna barabara kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la reli. Lengo la Serikali ni kutandika reli mpya na nzito zaidi kwa kiwango cha *standard gauge*. Huu wimbo umekuwa ni wa muda mrefu si chini ya miaka saba iliyopita. Kwa sababu Serikali yetu ni ya hapa kazi tu tunachohitaji ni vitendo. *Let us put our ideas into action.* Tumechoka na huu wimbo kwenye reli ya kati, tunataka tuone reli ya kati inatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la maji. Tarehe 20 Aprili nilipata majibu mazuri kutoka Serikalini kwamba kuna pesa imetengwa kwenye kata zangu kwa ajili ya suala hili. Hizo pesa ni za bajeti iliyopita, bajeti itaisha tarehe 30 Juni, niombe pesa hizo zitoke kabla ya bajeti mpya ili tuanze shughuli za kujipatia maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende ukurasa wa 47, aya ya mwisho inaongelea umeme Gridi ya Taifa. Mkoa wa Katavi ulikuwa kwenye mpango wa kupita Gridi ya Taifa kutoka Biharamulo sijaona kwenye mpango huu. Kwa vile kwenye bajeti iliyopita tulitenga naomba iendelee kuwepo na itekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye bajeti iliyopita kulikuwa na suala la *generator* mbili zilizokuwa zinatoka Belgium kwenye bajeti iliyopita hazijafika Katavi mpaka leo na hivyo kuifanya Mpanda na Katavi kwa ujumla kutokuwa

na umeme wa uhakika, na kushusha mapato ya Mkoa. Kwa hiyo, tunaomba kabisa hilo suala la *generator* hizo mbili nalo lipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali yangu katika sekta ya elimu kwa kubana matumizi katika shughuli za Bunge lakini isibane tu katika shughuli za Bunge ibane hata kwenye baadhi ya vifungu ambavyo vinasemekana viko kisheria kwenye mafungu ya bajeti mtayaona, kwenye masuala ya simu, magazeti, nyumba, umeme, haitavumilika, haiwezekani milioni nane, milioni 10, milioni 20 zinakwenda kule zirudishwe. Wote tunafunga mikanda, hakuna atakayesema nalipiwa simu kisheria, tunafunga mikanda. Kwa hiyo, wote tufunge mikanda tuiweke pesa kwenye maendeleo ya maji, tupeleke elimu, tupeleke kwenye barabara na tupeleke afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la Ustawishwaji Makao Makuu Dodoma. Hili suala limekuwa ni tatizo kwa wananchi wote wanaokaa Dodoma, ni shida, ni taabu, ni kero isiyokuwa na majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CDA* wana mambo yao, Manispaa wana mambo yao, mwananchi unalipa kodi zaidi ya mara mbili, kunakuwa na mgongano wa kazi kati ya Manispaa na *CDA*. *CDA* wanapandisha kodi, una kiwanja ulikuwa unalipa shilingi 97,000 leo unalipia ile kodi mara nne yake, si sahihi. Lazima iletwe sheria kwa niaba ya wananchi wa Tanzania tuweze kujadili hili suala. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Haya Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Kanuni ya 68(7), naomba ninukuu, inasema; "Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome Katiba, Sura ya Tatu, Ibara ya 63(3)(b) ambapo inasema; "Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza:-

(b) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti."

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nisome Katiba, Ibara ya 73, Masharti ya Kazi ya Wabunge kwa mujibu wa Sheria ya Na.15 ya 1984 inasema; "Wabunge wote wa aina zote watashika madaraka yao kwa mujibu wa Katiba hii, na watalipwa mshahara, posho na malipo mengine kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge."

Mheshimiwa Naibu Spika, nNaomba Mwongozo wako, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeamua kutokushiriki mjadala, lakini wenzetu wanasaini na wanalipwa mshahara. Kwa hiyo, naomba tu mwongozo wako kwamba ni haki na ni sahihi wenzetu kupokea posho wakati hawashiriki na kutimiza wajibu wao wa Kikatiba na kisheria? Ahsante. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, Mheshimiwa Esther Matiko, naomba tusikilizane, Mheshimiwa Savelina umesikika.

Naomba Waheshimiwa Wabunge, tuheshimu yale niliyoyasema mwanzo. Kuhusu huu Mwongozo ulioombwa sasa hivi nitautoa baadaye lakini ule utaratibu kwamba kwa nini wanachangia watu wa upande mmoja ni kwa sababu Kambi Rasmi ya Upinzani imetoa tamko lake tayari. Kwa hiyo, uwepo wao na kutokuchangia wakiwa humu ndani, Mwongozo huo nitautoa hapo baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu naona umekwisha maana ilikuwa anayefuata achangie kwa muda wa dakika kumi, sasa nitaleta kwenu matangazo…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani, mmebaki humu ndani kwa uchaguzi wenu, tafadhali, mtulie basi, wenzenu wametulia wale ambao hawajaambiwa watoke, kwa hiyo, tusikilizane nina matangazo machache.

Nitawataja Waheshimiwa Wabunge ambao wataanza kuchangia mchana tutakaporudi nao ni Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Rashid Chuachua, Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Bonnah Moses Kaluwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Hawa ndiyo tutakaoanza nao mchana tutakaporejea.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 06.55 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Hati za Kuwasilisha Mezani.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA (MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI):-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, kwamba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Wazir Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017; majadiliano yanaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Wazir Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Atakayeanza kuchangia jioni hii ni Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi atafuatia Mheshimiwa Emmanuel Papian John na baadaye Mheshimiwa Josephine John Genzabuke. Mheshimiwa Mariam hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa John.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imejaa mambo mengi ambapo yote yanakidhi matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kilimo. Wizara ya Kilimo nilidhani ingeweza kutusaidia kwa maana kwamba Benki ya Kilimo ingeweza kubeba zile pesa ambazo ziko *TIB* ili kuongezea mtaji ambao ni ile shilingi bilioni 60 inayotajwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Fedha nyingine nilizotaka ziweze kuhama ni zile za Mfuko wa Pembejeo wa Kilimo ambazo ziko *Exim Bank*. Zile pesa kama zingehama zingeweza kuongezea *capital* kwenye ile bilioni 60 ili wananchi waweze kukopa kwa urahisi kwa sababu itakapokuwa fedha zote ziko mahali pamoja itatusaidia kuweza kukopa na wananchi wetu wengi ambao ni asilimia 80 wako vijijini wangeweza kukopa pesa hizo, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili *NFRA* wamesema watanunua tani laki moja. Tani laki moja ni kiasi kidogo cha chakula, naomba Serikali iweze kununua chakula karibu tani laki mbili ili itakapotokea *shortage* tuweze kukabiliana na uhaba wa chakula. Hata hivyo, tutakapokuwa na *excess* wana uwezo wa kuuza nje kwa maana kwamba kurudisha pesa ili waweze kwenda kwenye *season* nyingine ya ununuzi wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo za kilimo. Hebu tuangalie ni njia ipi ambayo inaweza kutusaidia. Kwenye kilimo ningeshauri tuangalie ni namna gani ya kuweza kuzalisha mbegu zetu wenyewe kuliko *importation* ya mbegu ambapo tunatumia *foreign currency* kuziingiza hapa nchini, ni gharama kubwa. Pia Serikali iangalie ni namna gani ya ku-*invest* kwenye kilimo cha mbegu ili tuweze kuzalisha mbegu wenyewe nchini na kupunguza hali ya kutegemea mbegu za nje ambazo mara nyingine ni hatarishi kwa maana ya kilimo chetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni dawa za ruzuku za mifugo. Ukiangalia dawa za ruzuku za kuogesha mifugo hapa nchini zinasumbua, haziui isipokuwa kwenye ile *zero grazing* (ng'ombe wale wa majumbani) lakini ukienda kwenye wale ambao wanafuga nje mifugo mingi kupe hawafi. Nashauri na kuiomba Serikali iangalie *importation* ya dawa hizi au wale watengenezaji basi waangalie mara mbili kwa sababu kupe hawafi, ng'ombe wanazidi kuumwa na hii inachangia sana kusababisha mifugo yetu kutokuwa na afya na mwisho wa siku tunakuwa na mifugo ambayo haiko kwenye kiwango kwa sababu ya dawa ambazo hazikidhi kiwango cha kuweza kutibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuomba ujenzi wa Kiwanda cha Nyama pale Ruvu. Naomba Serikali ijikite kuangalia namna gani ya kujenga Kiwanda cha Nyama ili mifugo yote inayoweza kuingia Pugu iishie pale Ruvu ikachakatwa, nyama zikaingia kwenye *supermarkets* na masoko yetu tukawa na nyama bora. Hii itasaidia kuwa na nyama ambazo zimepimwa na ziko kwenye viwango. Pia tutaweza kujua ni mifugo kiasi gani tumechinja lakini hata ili *revenue* yetu haiwezi kupotea kuliko kwenda kushindana pale Pugu. Hilo ni jambo ambalo ningeomba Serikali ijikite kulishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba soko la mazao Kiteto, sisi tunazalisha mazao mengi sana. Ukiangalia *central zone* nzima inategemea mazao ya Kiteto, Dar es Salaam inategemea Kiteto, Tandale nzima inategemea Kiteto kwa asilimia karibu 50 lakini hatuna soko.

Naomba Serikali ilione hili itujengee soko ndani ya Wilaya yetu hata kama kuna soko la Kibaigwa lakini tuwe na soko letu la ndani. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda alione hili, tuwe na soko letu la ndani tuweze kuwa na *internal collection* yetu, tuweze kuona ni namna gani na sisi tunaweza kuvuka huko mbele tunakokwenda ili tuweze kupata namna gani ya kuweza kuingiza mapato lakini na watu wetu waweze kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na hilo, lile soko pamoja na *NFRA* kwa mfano inanunua mazao Kiteto zaidi ya tani labda 10,000 au 15,000 ile *transportation cost* ya kuja *NFRA* tungependa wapewe wananchi wetu wenye magari wasafirishe kile chakula kuliko kumpa zabuni mtu akasafirisha kile chakula na wananchi wakabaki pale. Ni mojawapo ya *creation employment* kwa vijana wetu. Watu wetu waweze kufaidi hata hii asilimia ndogo ya kusafirisha hicho chakula kwa sababu na wao magari wanayo. Hii inaweza kusaidia kwa sababu *tenderer* anaweza kusafirisha kwa gharama kubwa wakati wale wananchi wanaweza kusafirisha kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shilingi milioni 50 kila kijiji, *plan* yake vyovyote vile itakavyokuwa kwa Kiteto tumejitahidi kufungua *VICOBA*, *SACCOS* na vikundi mbalimbali lakini ningeomba nitengeneze *commitment*. Hebu

twende tuangalie kwenye maeneo hizi pesa zikienda, je, kwa mfano Kiteto tunaweza kutengeneza *commitment* yetu ya kutumia pesa hizi, tukazalisha, zikazunguka kwa wananchi, tukazisimamia wenyewe, kukaja *returns* kwa kufikiria muundo wetu wa namna gani ziweze kuzunguka zikafikia watu. Maana tukienda kwa maana kwamba kuna watu wale ambao watakuwa ni wajasiriamali ndiyo wapate hizo pesa *then* wale ambao siyo wajasiriamali katika ile *routine* ya mzunguko wa zile pesa wao watakuwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sisi Wilaya ya Kiteto tulete *plan* yetu mkiona inafaa basi tu-*guarantee*, tu-*sign contract,* mtupe hizo pesa tuzizungushe kwa maana ya wananchi wetu katika zile SACCOS *and then* tuzalishe ile riba na bado tuoneshe ile *flow* ya matumizi ya zile pesa na jinsi ambavyo zinavyoweza kurudi Serikalini ili ziwasaidie wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo *trend* ni kwamba tutakapokuwa tumeweza kuwapa watu wengine wale wazee ambao hawawezi kupata hizo pesa basi watakwenda kwenye ile *role* ya *TASAF*. Ile asilimia 10 ya vijana na wanawake ambayo itakusanywa kutokana na ile *collection* ya Halmashauri basi itasaidia vijana. Lengo letu ni ku-*make sure* kwamba tunaweza ku-*monitor* wenyewe, tukajua ni watu gani wanaweza kupata pesa hizo na nani hana, nani anastahili na nini kifanyike ili mradi ile *community* nzima iweze ku-*benefit* kutokana na hiyo *collection* na zile *generation* ya *income* ambazo tutakuwa tumezipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kuhusu mapato. Tumekubaliana ndani ya Serikali zile *electronic machines* zitatumika kukusanya mapato. Kuliko sasa hivi kwenda kwenye ku-*tender*, sijui *tenderer* amepata pesa, nashauri kwamba Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Halmashauri wasimamie kwa kutumia *electronic machines* tukusanye mapato wenyewe. Hii ni *creation of employment,* tujue tumepata nini, Halmashauri zetu zinaweza kukusanya zaidi kuliko *tenderer* ambaye anaweza ku-*benefit* zaidi kuliko Halmashauri zetu ambazo zingeweza kusimamia zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna barabara ambayo inatoka *NARCO* hapa njiapanda kwenda Kiteto. Hii barabara wakulima wengi wanaitumia, tunaomba Serikali ituone. Ni ahadi ya Serikali tangu mwaka juzi, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alituahidi kwamba angeweza kuitengeneza barabara hii. Tunaomba Serikali ya awamu hii kupitia mpango wake wa fedha hebu tuoneeni huruma, hii barabara haina shida kabisa, ina madaraja mawili tu au matatu. Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa, tuokoe kidogo angalau na sisi tupitishe mazao yakafikie walaji kwa gharama nafuu lakini na mkulima aweze ku-*benefit* kale ka-*profit* kwa sababu *transportation cost* zitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya Handeni – Kilindi – Kiteto – Chemba – Singida. Barabara hii inafungua mikoa mitano, inafungua Tanga, Manyara, Dodoma na Singida. Ile *pipeline* ya mafuta wanayosema ya kutoka Uganda itapita pale. Hebu Serikali tuoneni huruma, tunaomba hii barabara muiweke kwenye mpango. Barabara hii itakapofungua mikoa hii itapunguza hata msongamano wa hii barabara ya Dar es Salaam ili watu wengine wapitie kule lakini tutakuwa tumefungua mikoa kwa maana ya programu ya kufungua mikoa yote kwa barabara za lami na watu wote waweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *CDA* naomba Serikali ijaribu kuona ni namna gani inaweza kutengeneza *plan* ya *EPZ zone* kubwa hapa Dodoma ili vitu vingi na *investors* wengi waje Dodoma wakuze mji wetu na ivutie watu ili tupunguze msongamano Dar es Salaam. Hilo la msongamano linaweza kuhamia Dodoma, tukaweka kijiji kingine ambacho ni *business city center* ndani ya mji wetu wa Dodoma na ikapanua mji na kuongeza ajira na watu wakaongezeka Dodoma na sisi tukaendelea ku-*benefit*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ni mchache naona umekwisha, naomba kuishukuru Serikali. Nimpongeze Rais Magufuli kwa kazi anayoichapa, wote tumuunge mkono. Tulimuomba Mungu atupe Rais ambaye anatufaa Watanzania kwa sasa. Hebu tumuunge mkono, tukubaliane naye, maamuzi anayoyafanya tumuunge mkono, tusibaguane kwa itikadi za vyama, tuhakikishe kwamba tunamuunga mkono, tumpe *full support* ili aweze kulisukuma gurudumu la maendeleo ya Watanzania kule tunakotakiwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu, anachapa kazi, yuko makini, hana mjadala, kazi lazima iende, tusiwakatishe tamaa viongozi wetu. Tunawaunga mkono Mawaziri wetu, chapa kazi tuko nyuma yenu, fungulieni *speed* zote, fanana kama gari linaloshuka mlima halina *break* tusonge mbele, huko tutakakoishia Watanzania wote tutakuwa tumekubaliana kwamba lazima maendeleo yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Emmanuel. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Johnson na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili la Kumi na Moja, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru kwa moyo wangu wa dhati kabisa wanawake wa Mkoa wa Kigoma kwa kunirejesha Bungeni kwa mara nyingine na mimi nasema sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa ushindi mnono alioupata. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wengine kwa kuteuliwa ku wa Mawaziri katika Baraza la Mawaziri la mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuendelea kuishukuru Serikali kwa moyo wangu wa dhati kwa kuendelea kufanya mambo mazuri katika Mkoa wa Kigoma. Naishukuru sana na naendelea kuwapongeza viongozi wa Awamu ya Nne walioweza kuufungua Mkoa wa Kigoma. Daima tutamkumbuka Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweza kuufungua Mkoa wa Kigoma, lakini na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi ambaye kwa sasa ni Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa waliyoifanya ndani ya Mkoa wa Kigoma. Walitujengea barabara, wakatujengea Daraja la Mto Malagarasi maarufu kwa jina la Kikwete, daraja kubwa ambalo ni mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha mwaka 2015 niliwahi kusimama nikasema wananchi wameona na kwa vile wameona hawatatuangusha. Wakati ule tulikuwa tukiitwa sisi ni wapinzani lakini tuliufuta upinzani sisi ni Chama Tawala. Naomba nimshukuru Katibu Mkuu na aliyekuwa Katibu Mwenezi kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuwaelimisha wananchi wa Mkoa wa Kigoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyokuwa ikitekelezeka na hatimaye tukaweza kurejesha Majimbo yaliyokuwa yamepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa barabara zile ambazo hazikukamilika ikiwepo barabara ya Kigoma – Kasulu – Nyakanazi iweze kujengwa. Pesa zilizotengwa zipelekwe ili barabara ile iweze kukamilika. Pia kipo kipande cha kutoka Uvinza - Malagarasi kilometa 48 kwenda kwenye Daraja la Mto Malagarasi kwenye Daraja la Kikwete, naomba kilometa hizo ziweze kujengwa kusudi wananchi waweze kupata manufaa kupitia barabara hiyo. Kipo kipande kingine kutoka Chagu - Usinge - Kaliua, nacho naomba kiweze kukamilishwa kutuunganisha na Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 43 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia kuhusu reli. Reli katika Mkoa wa Kigoma, Tabora na Ukanda wa Ziwa ni kilio kikubwa sana. Kabla reli nyingine haijajengwa tunaomba reli ya kati iweze kujengwa kwa sababu itakuwa ni

mkombozi kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma, Tabora na Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi huu wa reli tunaomba uwe ni wa kutekelezeka isiwe ni ahadi isiyotekelezeka kwa sababu kwa muda mrefu tumekuwa tukisema kwamba reli itajengwa, lakini haijengwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa wakati huu iwe ahadi ya kutekelezeka, isiwe ni ahadi isiyotekelezeka kwa sababu reli inaboresha uchumi. Reli ikijengwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma pamoja na Tabora wataweza kunufaika na uchumi wao utaweza kuimarika. Reli itaweza kufungua fursa ya kibiashara kati ya nchi jirani na Kigoma itakuwa ni kitovu cha biashara. Watu wa Burundi, *DRC* wataweza kusafirisha mizigo yao kwa kupitia Mkoa wa Kigoma na reli hiyo ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa muda mrefu kabisa wananchi wa Mkoa wa Kigoma mpaka sasa hivi barabara hazijaweza kukamilika vizuri na kwa sababu hiyo reli ndiyo usafiri wa bei nafuu. Kwa sababu sasa hivi mtu akitoka Kigoma kuja Dar es Salaam anatumia shilingi 70,000 hapo hajapata chakula njiani, kwa kutumia basi anaweza kufika Dar es Salaam kwa shilingi 100,000 lakini reli ikikamilika itawapunguzia gharama ya usafiri wananchi wataweza kusafiri kwa bei nafuu na wataweza kusafirisha mizigo yao kwa bei nafuu lakini gharama za maisha nazo zitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi mfuko wa *cement* Dar es Salaam shilingi 13,000 mpaka shilingi 14,000, lakini Kigoma shilingi 19,500. Tunaomba reli ikamilike ili wananchi wanaotumia reli waweze kunufaika lakini hivyo hivyo kwa kupitia reli uchumi uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuzungumzia kuhusu elimu. Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuondoa ada kwa wanafunzi. Watoto wengine wa shule walikuwa wanafichwa kwa sababu ya ada lakini kwa sababu ada imeondolewa wanafunzi sasa wamepelekwa shuleni kwa wingi. Darasa la kwanza mwaka huu tumeona wameanza kwa wingi na ninaamini wataendelea hivyo hivyo ni kwa sababu Serikali imeondoa ada kwa wanafunzi. Naomba ada hii isiwe tangu darasa la kwanza mpaka *form four* iendelee mpaka *form six* ili watoto waweze kusoma kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuondoa ada tuangalie sasa ni jinsi gani tunawekeza katika elimu. Ninaamini watoto watakaomaliza *form four* watakuwa wengi, wengine watabahatika kuendelea na wengine wengi hawataendelea watarudi kukaa vijijini. Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali iwekeze katika kujenga vyuo vya *VETA* ili watoto wanaomaliza kidato cha nne

na pengine *form six* waweze kwenda kusomea *VETA*, hatimaye wajiajiri katika shughuli za mikono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwasemee walimu ambao wanadai stahiki zao nyingi. Wapo walimu ambao wamepandishwa madaraja na wamestaafu na walikiri kupanda daraja lakini mpaka wanastaafu mishahara yao haijaweza kurekebishwa. Nilitaka kuuliza, je, Serikali itafanya marekebisho kwa kutumia mishahara yao pale walipopanda madaraja? Kama si hivyo, naomba Waziri anayehusika wale ambao watakuwa na malalamiko wamepanda daraja mishahara haijarekebishwa waweze kurekebishiwa mishahara yao kusudi wanapotapa pesheni zao iendane na mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie maji. Maji ni afya, maji ni uhai. Kwa muda mrefu wanawake wa Tanzania wameendelea kuteseka kwa kukosa maji. Sisi Tanzania tumejaliwa kuwa vyanzo vingi vya maji, tumejaliwa kuwa na bahari, maziwa, mito mikubwa na modogo.

Kwa hiyo basi, naomba Serikali ijipange kutumia vyanzo hivyo ili kuweza kufikisha maji vijijini na kuwaondolea adha wanawake ambao wamekuwa wakipata shida kufuata maji kwa umbali mrefu na kukosa muda wa kufanya shughuli za kuwaletea maendeleo na kuinua kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kasulu ipo miradi iliyoanzishwa lakini miradi hiyo haijaweza kukamilika kwa sababu fedha zimekuwa hazipelekwi. Naomba sasa katika bajeti hii fedha zipelekwe ili miradi iliyoanzishwa katika Wilaya ya Kasulu iweze kukamilika. Ipo miradi ya Kasangezi, Ahsante Nyerere, Helushingo na Nyarugusu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jahmuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri Mkuu na Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameshuhudia juhudi zao katika kutekeleza dhamira ya uwajibikaji na maadili kwa viongozi, watendaji na watumishi wasiyo waadilifu kwa kuwatumbua majipu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikishafika sasa hivi saa moja kwenye taarifa ya habari, ikifika saa mbili kwenye taarifa ya habari wananchi wanakimbia kwenda kusikiliza leo kunatokea kitu gani. Wananchi walikuwa wameshachoka na tabia ya baadhi ya watendaji wa Serikali ambayo walikuwa wakiifanya, kwa hiyo, sasa wanafurahia juhudi ya Serikali ambayo inafanya ya kuhakikisha kwamba hakuna matabaka kati ya walio nacho na wasiyo nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nianze kwa kunukuu maneno aliyosema Kitilya Mkumbo kwenye mtandao wa *twitter* amesema; "Tunahitaji upinzani utakaojikita katika sera mbadala. Upinzani unaotegemea makosa ya Serikali ya CCM pekee unaweza kupwaya sana katika kipindi hiki." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ninukuu hili la Mkumbo kutokana na kitendo cha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kutowasilisha hotuba ya bajeti ya Kambi ya Upinzani na hasa ukiangalia bajeti yetu sisi ya Waziri Mkuu ina karatasi kama 100 kitu hivi lakini ya mwenzetu huyu amekuja na karatasi tatu. Matokeo yake kwa sababu kashindwa kuiandika bajeti anashawishi wenzake watoke nje. Hoja ya Kitilya Mkumbo iko sahihi kabisa hawa watu wamefilisika na wamepwaya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Tanzania kwa kupata mradi mkubwa wa bomba la mafuta kutoka Uganda kuja Tanzania hususani Mkoa wa Tanga. Ni matarajio yangu kwamba fursa hii ambayo tumeipata tutaisimamia vizuri na kuweza kuanza kufanya maandalizi ya maeneo ambayo mradi huu utapita kwa kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo yale na hatimaye kuanza kufanya maandalizi ya fidia kwa maeneo yale yatakayokuwa yamepitiwa na mradi kama kwenye mashamba na nyumba ili kuondoa usumbufu katika utekelezaji wa mradi huu. Ni matarajio yangu kwamba watatoa elimu kwa wananchi ili waweze kutambua faida ya mradi huu ambao umepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane kabisa na kaulimbiu kwamba Tanzania kuwa ya viwanda inawezekana. Ili kufanikisha jambo hili ni vizuri tukaimarisha suala la kilimo. Tukiimarisha kilimo vizuri tukakipa kipaumbele kitaweza kuzalisha malighafi ambazo ndizo zitakazoweza kulisha hivyo viwanda.

Tusiposimamia vizuri kuhakikisha kwamba kilimo tunakipa kipaumbele tunaweza tukajenga viwanda na hatimaye tukakosa malighafi, viwanda vikawa vipo na havifanyi kazi na ile kauli mbiu ya kwamba Tanzania iwe ya viwanda ikawa ni kazi bure. Hivyo, naishauri Serikali tusimamie na tuhakikishe kwamba kilimo kinapewa kipaumbele, kiende sambamba na upatikanaji wa maji. Kama maji hayapo kiwanda hakiwezi kufanya kazi, kama hakuna umeme wa uhakika kiwanda hakiwezi kufanya kazi, kama miundombinu hakuna, kiwanda kinaweza kikafanya kazi lakini usafirishaji wa hayo mazao itakuwa ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni pamoja na reli. Tunapozungumzia reli kama ambavyo wezangu wengine wametangulia kuzungumza reli ni kitu muhimu sana. Reli inapunguza uharibifu wa barabara, magari makubwa yanapita yanaharibu barabara kila siku inafanyiwa matengenezo. Reli ikitengenezwa nadhani mizigo yote itapita kwenye reli na viwanda vyetu vitakapokuwa vimezalisha mazao yatapitishwa kwenye reli, hivyo angalau shughuli za uzalishaji na mali kupeleka kwenye mikoa kupitia reli. Napozungumzia reli basi naomba ifahamike kwamba ni pamoja na reli ile ya kutoka Tanga - Kilimanjaro - Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala zima la Mfuko wa *PSPF*. Huu Mfuko wa *PSPF* unachelewesha mno mafao ya watumishi waliostaafu. Niiombe Serikali, watumishi hawa ambao wanakuwa wamestaafu hizi fedha zao ndizo zinazowasaidia kuweka maisha yao vizuri. Inapokuwa wanacheleweshewa kupata mafao yao inakuwa ni shida. Kwanza, inawapa ugumu wa maisha kwa sababu ameshajipanga kwamba amestaafu kuna hizo fedha anategemea kufanya shughuli ambazo zitamwezesha kupata kipato, lakini anacheleweshewa kupata fedha hizi. Niombe Serikali, hawa wastaafu wanapostaafu basi iwe ni muhimu sana kuwaandalia mafao yao mapema ili waweze kutoka wakiwa na fedha zao na hatimaye waweze kuishi muda mrefu kuliko ilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, suala la walimu. Lipo tatizo kwa walimu kuhusiana na upandishwaji wa madaraja. Walimu wamekuwa wanachukua muda mrefu kwenye kupandishwa madaraja na hata wakipandishwa mishahara yao kwa maana ya stahiki zao zile zinachelewa sana kufanyiwa marekebisho, inachukua hata miezi sita mtu hajarekebishiwa. Niombe wanapopandishwa madaraja basi na zile stahiki zao ziwe zimeandaliwa. Kule Korogwe wapo baadhi ya walimu wanadai malimbikizo toka 2010 hadi hivi sasa hawajalipwa na wamepandishwa madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie upya suala la posho ya kufundishia *(teaching allowance)* kwa walimu. Tuseme tusemavyo walimu wana jukumu kubwa sana, wanafanya kazi kuliko mfanyakazi mwingine yeyote.

Tukirudisha *teaching allowance* kwa walimu haki ya Mungu hii elimu itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Serikali hebu tulitazame jambo hili. Walimu hawa wamekuwa wakitoka shuleni wakifika nyumbani ni kazi ya kuanza kufanya maandalizi, kusahihisha mitihani, kusahihisha madaftari na kuandaa maandalio ya kesho. Kwa bahati mbaya sasa itokee mama ndiyo mwalimu, baba labda ni mhasibu, yule mama anakaa kufanya kazi ya ualimu pale nyumbani mpaka saa nane ya usiku hebu niambie, baba amelala yupo kitandani. Unatarajia hiyo nyumba ya mwalimu na huyo mumewe inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali hata kama atafanya kazi kwa o kwa muda huo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umemaliza muda wako naomba ukae!

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa sasa hivi anafutia Mheshimiwa Nassoro Amar na baadaye atakuja Mheshimiwa Chuachua na kufuatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya njema kwa siku ya leo na kuweza kusimama hapa. Pia nimshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa na Baraza lote la Mawaziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kutumbua majipu. Ni kazi nzuri sana inayofanyika pamoja na kwamba wengine wanakasirika lakini ndiyo ilikuwa kiu ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hotuba hii nzuri ambayo imesheheni mambo mazuri. Napenda niwakumbushe wenzetu Kambi ya Upinzani, kuna mchangiaji mmoja alisema kipindi cha nyuma kwamba ninyi wana CCM mnapenda sana kupongeza, mimi sipongezi, wakati Mwenyezi Mungu anasema usiposhukuru kidogo hata kikubwa hauwezi ukashukuru. Hata kwenye maombi kwanza unamshukuru Mwenyezi Mungu kwa alichokupa na unachohitaji unaendelea kuomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, napenda niikumbushe Serikali yangu Tukufu, tunaambiwa tunalalamika, hatulalamiki tunakumbushana. Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni kwenye Jimbo langu la Nyang'hwale tulimweleza matatizo yetu na akaahidi. Tulikuwa na ahadi ambayo tuliahidiwa na Rais wa Awamu ya Nne kuhusu barabara ya kutoka Kahama – Nyang'hwale - Busolwa - Busisi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. Pia alipokuja Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kampeni nilimkumbushia hilo na akaahidi kwamba barabara hiyo itajengwa. Kwa hiyo, naendelea kukumbusha barababa hiyo ijengwe angalau kwa kilometa chache kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niishukuru Serikali yangu kwa ahadi yake ya kusambaza umeme vijijini. Jimbo la Nyang'hwale tayari tumeshapata umeme lakini ni kwa kiwango kidogo sana. Vijiji vingi havina umeme na Watanzania wengi waliopo Jimbo la Nyang'hwale wanasuburi kwa hamu umeme kwa ajili ya kufanya kazi zao mbalimbali ambazo zinahitaji umeme. Wanahitaji wafunge mashine ndogondogo kwa ajili ya kukamua alizeti, mpunga na mambo mengine.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati muda utapofika utukumbuke sana Jimbo la Nyang'hwale kutukamilishia ahadi ambazo ametuahidi mara nyingi kutupa umeme katka Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Jimbo langu la Nyang'hwale tuna tatizo kubwa la maji, nimeshaongea tangu nilivyoingia mwaka 2010. Nimezungumzia suala la maji kwa nguvu zote na Serikali ilisikia na ikaitikia wakatuahidi kutujengea mradi wa maji. Tuliahidiwa mradi mzuri na mkubwa wa kutoka Ziwa Victoria na kusambaza maji katika Jimbo la Nyang'hwale. Tumepangiwa shilingi milioni 15.7 ndani ya miaka mitano na huu wa sita tumeshapewa shilingi bilioni 1.9. Naomba sasa ili niweze kurudi tena Bungeni mwaka 2020 mradi huo wa maji ukamilike.

Mheshimiwa Waziri Mkuu kama utapenda tuwe pamoja tena mwaka 2020, naomba mradi huu ukamilike. Waziri wa Maji nipe hayo maji ili mama zangu na dada zangu waweze kunipa kura tena niwe na jambo la kusemea vinginevyo sirudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya. Kwenye Jimbo langu kuna hospitali ambayo imepandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya lakini kwa bahati mbaya hospitali ile ina majengo ya kizamani, haina wodi, haina *x-ray* na vifaa tiba hakuna. Kuna wodi mbili tu, wodi moja ya akina baba wanachanganywa wagonjwa wa maradhi yote mle ndani na wodi ile ina vitanda kama tisa tu. Kwa hiyo, naomba ili sasa iwe Hospitali ya Wilaya tuletewe

vifaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na vifaa tiba na kupanua majengo ikiwemo majengo ya wodi ya kulaza wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja Jimboni kwangu aliwaahidi wachimbaji wa madini ya dhahabu kwamba watatengewa eneo, kuna eneo moja linaloitwa Mwasabuka huko Nyijundu, alisema watagawiwa wachimbaji wadogo wawe huru wapewe leseni ili waweze kuchimba na waweze kusaidiwa na Serikali ili waweze kunyanyua kipato chao na kipato cha Serikali.

Naomba kumkumbusha Waziri wa Nishati na Madini kwamba ahadi hiyo aifuatilie ili wananchi hawa, vijana hawa ambao wanapata kipato chao kutokana na uchimbaji wa madini basi wawafikirie na kuweza kuwatekelezea ambayo waliwaahidi wakati wa kampeni wasione kwamba tulikuwa tunawadanyanga kwa ajili ya kutupa kura, waone kabisa tulikuwa tukiwaahidi mambo yaliyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu, naishukuru Serikali imeanza kutekeleza mpango wa elimu bure. Kama walivyosema wachangiaji wengine, tuangalie stahiki za walimu wetu, wazipate kwa muda ili wawe na ari na kasi na nguvu mpya kabisa ya kuweza kusimamia suala la elimu. Kwa sababu stahiki zao zinachelewa, zikichelewa amani ama imani ya kazi inashuka. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kuangalia sana stahiki zao ili waweze kuwa na moyo wa kufanya kazi hiyo bila kutetereka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuongelea kuhusu wafugaji. Katika Jimbo la Nyang'hwale wafugaji wetu wamesahaulika. Nimeangalia katika mipango yote iliyopita sijaona wafugaji wa Jimbo la Nyang'hwale wamefikiriwa nini, hakuna soko, malambo wala majosho. Kwa hiyo, naomba wafugaji wa Jimbo la Nyang'hwale nao wafikiriwe kuboreshewa soko la mazao ya mifugo yao. Nimeangalia kwenye kitabu cha mpango, Mkoa wa Simiyu vinajengwa viwanda vitatu vya ngozi lakini Geita hakuna kiwanda hata kimoja cha ngozi, inakuwaje namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Jimbo la Nyang'hwale na wakulima wote wa Tanzania kwa kweli wamekuwa wanakata tamaa kutegemea kilimo kwa sababu soko la mazao siyo la uhakika, pembejeo zinakuja mbovu, za gharama kubwa na zinachelewa kufika. Naiomba Serikali, kwa sababu wimbo mkubwa ni kwamba tuwasaidie wakulima, hebu tujaribu kweli kuwasaidia wakulima kwa kuwasaidia pembejeo na soko lao liwe la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu, kulikuwa na mchakato wa Makao Makuu ya Wilaya

ya Nyang'hwale na bahati nzuri ulishaisha na Serikali ikatamka Makao Makuu ya Nyang'hwale yatakuwa Karumwa. Kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi hati ya kujulisha kwamba Makao Makuu ya Nyang'hwale yako wapi haijatoka.

Mheshimiwa Waziri Mkuu utakaposimama hapa, waambie wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale, hawa wapinzani hususan CHADEMA niliowashinda vibaya sana wanapiga kelele na kusema kwamba haya Makao Makuu hayapo mnadanganywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Naomba utakaposimama uwajibu hawa Watanzania wa Nyang'hwale pamoja na hao wapinzani, waelewe Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale yako Karumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu ardhi. Tuna ardhi nzuri, tunaomba ipimwe ili wananchi wetu waweze kunufaika na ardhi yao. Kwa bahati mbaya kuna zile hati za kimila, wananchi wetu wamepimiwa tangu mwaka 2011 mpaka leo hawajazipewa, ni zaidi ya hati 800 na kitu. Serikali ina mpango gani sasa kuwapa hizo hati za kimila ili ziweze kuwasaidia hawa wananchi kupata mikopo midogo midogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo napenda kulizungumzia ni UKIMWI. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI na dawa za kulevya. Tunajaribu kuangalia matatizo makubwa ya UKIMWI yanaanzia wapi, tumejaribu kuzunguka na kuongea na wadau mbalimbali wakatushauri na kutuambia na sisi wenyewe kwa kuona kwa macho matatizo ya UKIMWI yanaanzia kwenye ulevi. Kuna ulevi wa aina nyingi, kwanza mirungi, viroba, bangi, watakapokunywa na kuvuta wanajisahau wanaingia kwenye ngono zembe. Kwa hiyo, angalieni sana UKIMWI unaanzia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iweke utaratibu mzuri kutoa elimu ya UKIMWI kuanzia chekechea, shule za msingi, sekondari mpaka vyuo vikuu waelezwe UKIMWI unaanzia wapi na ni tatizo gani. Serikali ipange utaratibu wa kutoa elimu kwenye shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na hii bajeti ambayo imesomwa na Waziri Mkuu kuhusu shilingi milioni 50. Nategemea kwangu kupata shilingi bilioni 3.2, naamini kabisa ikitolewa elimu nzuri kwa hawa ambao wanalengwa, watanyanyua vipato vyao lakini kwanza wapewe elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri. Halmashauri yangu ina vipato vingi lakini vidogovidogo lakini mapato yale hayakusanywi. Kwa nini hayakusanywi? Wanatumia stakabadhi za kuandika kwa mkono. Naomba zile mashine zisambazwe katika Halmashauri zote…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umemaliza, naomba ukae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja kwa mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi naomba niungane na waliotangulia kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kuwa hapa leo katika Jumba hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja asilimia mia moja. Niwapongeze wananchi wa Tanzania kwamba katika uchaguzi uliopita Taifa limeibuka na kiongozi. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake na niwapongeze wananchi wa Tanzania kwa kumpa zana na silaha ya Urais. Maana ifike mahali tutofautishe kati ya urais na uongozi, vinaweza vikawa vitu viwili tofauti, inapokuwa kitu kimoja mambo yanaweza kwenda kwa kasi na inakuwa hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana pia Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri wetu Mkuu ambaye hakuna shaka anafanya kazi inayoonekana na sisi ambao tumepata bahati ya kumfahamu ni mtu ambaye anafanya kazi kwa umakini sana. Kwa hiyo, sina wasiwasi kabisa kwamba timu ya Baraza la Mawaziri ilivyopangwa kwa umakini Taifa hili linaweza likaiona neema na naona *speed* inaanza kuwapa wenzetu kiwewe. Wasiwe na kiwewe watulie kwa sababu kazi isipofanyika watu watalalamika kazi haifanyiki, sasa inapofanyika watu wanalalamika, hatuwezi kuwa na Taifa la walalamikaji tunataka Taifa la watu wa kujenga hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuzungumzia kwamba Taifa letu sasa tunaingia katika awamu muhimu ambayo inatufafanua hata kwa ngazi za ulimwengu. Naomba nimpongeze sana Rais wetu kwamba katika diplomasia yake amefanya kitu ambacho wanadiplomasia wanakienzi sana, ameanzia kutembelea nchi jirani. Katika diplomosia iliyobobea hiyo ndiyo diplomasia kwa sababu unaanza kuwatembelea watu ambao wanaitwa *your natural allies*, watu ambao una maslahi nao kwa karibu sana. Kwa hiyo, ni jambo la kupongeza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti iliyo mbele yetu nimeiangalia, nimeipitia kwa umakini sana, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu

kwamba imekaa vizuri. Tunaposimama hapa kuchangia ni kuboresha hasa kwa upande wangu kuzungumzia mtazamo wa wananchi wa Muleba Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana wananchi wa Muleba Kusini, hali yangu ilikuwa ngumu lakini mnaniona nimerejea mjengoni, ahsanteni sana Muleba Kusini. Waswahili wanasema ukweli ukidhihiri uongo hujitenga. Kwa hiyo, nimesimama hapa kwa mantiki hiyo na nataka kusema kwamba kazi inaendelea na tumeshapata watu wa kutuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mawaziri wamejipanga chini ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais na Mama Samia Suluhu ambaye ni kielelezo tosha kwamba wanawake tunaweza, naye nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninawawakilisha wakulima, wavuvi na wafugaji wa Muleba Kusini. Hali yao siyo nzuri sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nchemba alikuja akaona tuna matatizo ya wafugaji na wakulima. Hapa ninavyozungumza mifugo katika Mkoa wa Kagera iko kwenye hifadhi.

Kwa hiyo, naomba kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu na wewe utuwekee nguvu zako tuweze sasa kuhaulisha hii ardhi ambayo iko kwenye hifadhi ambazo zimepitwa na wakati tuweze kupata mahali pa kuchungia. Ni tatizo kubwa sana kwamba ukitaka kutoa mifugo ile kwenye hifadhi itabidi upeleke kwenye mashamba ya wakulima itazua migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo pia tusisahaulike sisi. Suala la mnyauko bado halijakaa sawasawa na magonjwa yanaibuka kila siku. Kituo chetu cha Utafiti cha Maruku kimesahaulika. Naomba Kituo cha Maruku kwa ajili ya Ukanda wa Mkoa wa Kagera kipewe kipaumbele na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili utuunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo. Muleba ni wakulima wa maharage, migomba na nafaka mbalimbali lakini hatujawahi kuona vocha hata moja. Kwa hiyo, katika hili tumesahaulika na tunaposahaulika inakuwa njaa. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyestaafu aliwahi kunipa mahindi nipeleke Muleba, hii sio tabia yetu, lakini tukisahaulika katika uwezeshwaji, mambo yanakuwa magumu sana. Kwa hiyo, suala hili nalo tuliwekee mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikimbilie sasa kuzungumzia suala la miundombinu. Bahati nzuri nchi yetu sasa hivi inaendeshwa na wahandisi na mainjinia naona kila siku wanapangwa katika sehemu mbalimbali. Suala la reli halina mjadala, nchi haiwezi kuendelea bila reli. Nikizungumzia kwa mtazamo wa sehemu yoyote ile, ukienda nchi za Ulaya unakuta reli inafanana na mishipa ya damu, wanasema ni *capillary system*. Kwa sababu nchi ya kilimo kama haina reli haiwezi kushindana kwenye masoko ya dunia. Ukibeba mizigo,

hususan mahindi, kahawa kwa ma-*semi trailer* huwezi kushindana katika uwanja wa dunia. Kwa hiyo, suala la reli lipewe mkazo, napongeza kwamba limepewa kipaumbele lakini tunazungumzia reli *basically* kwenda kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi watu wa Mkoa wa Kagera hususan Muleba Kusini, tunaomba kabisa Serikali hii Tukufu, chini ya Jemedari wetu Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na chini ya *Prime Minister,* Mheshimiwa Kassim Majaliwa, meli ya Ziwa Victoria imekuwa sasa lazima niseme aibu, imekuwa ni aibu ya Taifa wananchi wanasubiri meli. Wale watu walioangamia kwenye *MV Bukoba* wakiibuka leo zaidi ya miaka 20 baadaye hatujanunua meli jamani hatutapata mahali pa kukimbilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo niunganishe usalama katika Ziwa Victoria. Ziwa Victoria sasa hivi, wavuvi wenyewe ndiyo wameweka ulinzi wao shirikishi. Naomba sana Waziri wetu wa Mambo ya Ndani na hapa naomba Waziri Mkuu utuwekee nguvu kwamba ulinzi katika Ziwa Victoria uimarishwe kwa sababu wananchi wametelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda siyo rafiki nikimbilie sasa suala la miundombinu hasa barabara. Nilishapiga magoti, kila jioni nasali tupate barabara ya kwenda kwenye Hospitali yetu Teule ya kutoka Muleba – Rubya**.** Hospitali Teule unapita kwenye mlima mkali na miamba, akina mama wanajifungua pale kwa sababu ya mtikisiko kwa ile barabara ilivyokuwa mbovu kwenye Mlima Kanyambogo. Sisi Muleba Kusini tupo tayari kuchapa kazi chini ya Jemedari wetu Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na timu yake aliyoipanga na Waziri Mkuu lakini sasa msitusahau tuko mbali, lakini nashukuru kwamba Waziri Mkuu umshapita umeona wewe mwenyewe umbali wetu, kwa hiyo bila kuwekewa juhudi maalum mambo yatakuwa magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wale waliozungumzia suala la vijana na ajira. Tusipowawekea vijana wetu utaratibu wa ajira itakuwa vigumu. Sisi watu ambao tumeajiriwa tunapenda kuwaambia vijana wajiajiri, watajiajiri namna gani bila uwezeshwaji? Kwa hiyo, suala la kuwezesha vijana ni muhimu sana na uwezeshaji ni taasisi za Serikali kuweka mazingira wezeshi, siyo kuwa-*harass* wale vijana kama vyombo vya kuwafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kulipa kodi, unamwezesha kijana, unaangalia *accounts* zake unaona kama kweli amepata faida, siyo kila mfanyabiashara anapata faida. Ifike mahali ijulikane kwamba mfanyabiashara pia anaweza akapata hasara na anapopata hasara itambuliwe. La sivyo vyombo vyetu vinaweza vikafunga *small micro enterprises,* viwanda vidogo vidogo vya vijana vikafungwa vyote kwa sababu ya *harassment* tukashindwa kwenda mbele kama Rais alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo ya kwangu na naomba niwasihi vijana kwamba dawa za kulevya ni hatari, UKIMWI ni hatari, lakini nasema na viroba ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme viroba ni hatari, navikemea Muleba Kusini, navikemea popote pale. Nilikuwa tayari kushindwa uchaguzi kama nikisema eti vijana wanywe viroba ndiyo wanipigie kura, wasinipigie kama ni mambo ya viroba. Kwa hiyo, suala la viroba ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ya Sweden, pombe inauzwa na Serikali, labda niseme maana yake Taifa hii limetusaidia sana. Katika nchi ya Sweden, Shirika la kuuza na kununua pombe Kali ni Shirika la Serikali, hili nalo tujifunze kutoka kwa hao wenzetu ambao wamepiga hatua katika yale ambayo yanatukwaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni wale ambao wanabeza juhudi za Rais, kwa mfano kusema mizigo imepungua bandarini, bandari yetu ya Dar es Salaam lazima tuiboreshe, kama mizigo imepungua ilikuwa hatuna faida nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda sio rafiki …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, naomba ukae.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja moja kwa moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Chuachua atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka, Mheshimiwa Allan Kiula na Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe kwa kazi kubwa na nzuri inayopendeza ya kuandaa hotuba hii ambayo kimsingi inatafsiri kwa kina Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi na Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme tu kwamba kazi kubwa inayofanywa na Serikali iliyopo madarakani ni kazi ambayo inapaswa kuungwa mkono na sisi Wabunge. Tuiunge mkono Serikali yetu ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisahau kusema kwamba wakati tuna harakati za kisiasa, wananchi wangu hawakunituma ili nije kuonekana kwenye *tv*. Wamenituma nije kufanya kazi kwa sababu wao hawahitaji *tv*, wanahitaji maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda niiambie Serikali kwamba wakati tunajiondoa kwenye hali ya utegemezi lazima tufahamu kwamba maendeleo haya tunayoyataka ni vita kubwa sana. Hili ni jambo la msingi sana, maendeleo ni vita. Nachukua kauli ya Profesa wangu Mheshimiwa Norman Sigalla King ameandika maendeleo ni vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo viongozi wengine ni waandamizi, wanazungumza kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Rais wake wanapofanya kazi kubwa ya kuwawajibisha watumishi ambao kimsingi wanatenda kinyume na taratibu za utumishi wa umma wanakosea, hili ni suala la ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ni suala la ajabu kwa sababu viongozi hao wanafikia hatua ya kudiriki kuzungumza kwamba wanaowajibishwa ni watu wa mkondo fulani wa kisiasa, ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais tunamuona anavyofanya kazi na Waziri Mkuu akiwa anawawajibisha viongozi ambao kimsingi wengine ni waandamizi katika Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, lazima tuzungumze mambo ambayo hatuwapotoshi Watanzania. Tukisema hivi maana yake tunataka kuwaaminisha Watanzania kwamba hao wanaoharibu wao ndiyo wamewatuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba wakati Serikali inakwenda kwenye hatua ya maendeleo ya viwanda, naomba waendee katika hatua hiyo wakijua kwamba maendeleo haya ni vita. Unapokwenda kwenye viwanda unahitaji rasilimali kubwa inayozalishwa nchini iende kwenye *processing industry,* lakini wakati huo huo tunawakwaza Watanzania wenzetu ambao kimsingi tuliwategemea watusaidie, wao kazi yao ilikuwa ni kusafirisha malighafi, wanakwazika na kitendo cha Tanzania kutaka kwenda kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kwenda kwenye uchumi wa viwanda na kuziwezesha sekta zinazotegemea viwanda, wapo Watanzania

wenzetu wanaishi hapahapa, wanakwazika na ununuzi wa ndege kwa sababu wana hisa kwenye makampuni mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kuboresha reli tunawakwaza Watanzania wenzetu kwa sababu wengine wana malori, wanataka bidhaa zisafirishwe kwa malori wapate faida hata kama tunadidimia katika uchumi wetu. Maendeleo ni vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ikaze buti kuhakikisha kwamba inasimamia yale ambayo wameyasema na sisi tutawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, niseme tu kwamba wakati tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda tunategemea sana kilimo lakini mipango yetu inaonyesha wazi kabisa kwamba mchango wa sekta ya kilimo ni asilimia 25 tu katika Pato la Taifa wakati nguvu kazi iliyopo katika kilimo ni zaidi ya asilimia 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kwamba kiasi kikubwa cha nguvu kazi kipo kwenye kilimo lakini tija ya kilimo bado haiwezi ku-*support* uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Naiomba Serikali iliangalie hili na ihakikishe kilimo kinatengewa pesa za kutosha. Wakati wa kuondoa kero kwa wakulima wetu ni sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kauli aliyoitoa Waziri Mkuu, alipotembelea maeneo ya Kusini. Amefanya uamuzi mkubwa wa kufuta baadhi ya makato ambayo yalikuwa ni kero kubwa kwa wakulima. Huu ni uamuzi mkubwa sana. Wakulima wetu wamelalamika kwa miaka mingi na tunaendelea kuitia moyo Serikali kwamba iendelee kuona namna ambavyo inaweza kuondoa kero kwa wakulima wa mazao yote yanayotegemewa kukuza uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, tunategemea pia Serikali sasa itoe kipaumbele katika suala zima la pembejeo. Katika bajeti iliyopita, Serikali ilitoa *voucher* za pembejeo kwa takribani *voucher* milioni tatu. Mkoa wa Mtwara peke yake ulipata *voucher* 10,000 tu na Jimbo la Wilaya ya Masasi lilipata *voucher* 3000. Hili ni jambo ambalo linaweza kuwakatisha tamaa wakulima kwa sababu *voucher* hizi hazikutosha. Naiomba Serikali iongeze mkazo mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba *voucher* zinatoka za kutosha ili wakulima wetu wapate pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze haraka haraka kwenye suala la elimu. Tunazo changamoto kubwa na Serikali imefanya juhudi kubwa. Mimi naamini kwamba changamoto hizi ni sehemu ya maendeleo. Kwa hiyo,

niendelee kuiomba Serikali iendelee kufanya juhudi kubwa, lakini naiomba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, iweke msisitizo mkubwa sana kwenye suala la Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya mfumo rasmi. Ukiangalia historia ya elimu ya nchi hii, toka Serikali ya awamu ya kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa, alifanya kazi kubwa katika eneo la Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya mfumo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa sababu tunahitaji nguvukazi kwenye Sekta ya Viwanda, hatuwezi kuhakikisha kwamba tunawaelimisha Watanzania wengi kwa wakati mmoja kwa kutegemea waingie madarasani. Pia naiomba Serikali ifahamu kwamba kiwango cha Watanzania kutokujua kusoma na kuandika kinaongezeka na vijana wetu wengi hawana elimu ya kutosha. Kwa hiyo, tunaweza tukawa na viwanda vya kutosha lakini tukaishia kwenye kuwa wabeba mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana, Serikali yangu ihakikishe kwamba inapanua wigo wa elimu ili wale ambao hawana uwezo wa kwenda kwenye sekta rasmi ya elimu waweze pia kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto kubwa katika ardhi, lakini juhudi za Serikali za kutaka kuwapimia wananchi tunazipongeza ila tunamwomba kwa heshima kubwa Waziri wa Ardhi afike Jimbo la Masasi ili atatue kero za wananchi wa Masasi. Wananchi wa Masasi wana matatizo mengi katika ardhi na bahati nzuri tumezungumza na Waziri, amesema atapanga muda. Naomba baadaye atuambie ni lini atakwenda ili kusudi wananchi waweze kutatuliwa matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo matatizo katika eneo la afya, lakini pia Serikali imepiga hatua katika kutatua kero za afya kwa wananchi wetu, isipokuwa katika Jimbo la Masasi matatizo bado yapo. Tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba katika bajeti ya mwaka huu inatoa pesa za kutosha ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze tu suala la ulinzi na usalama. Tunaishukuru Serikali kwa juhudi zake, tunashukuru Serikali kwa kuhakikisha kwamba inawajali Askari Polisi. Isipokuwa katika Jimbo la Masasi, kuna tatizo kubwa. Jeshi la Polisi wanaishi katika maeneo ambayo hayana nyumba. Tunaomba Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumze tu kwamba Askari wetu wa Jeshi la Kujenga Taifa, tunaomba wapatiwe Bima ya Afya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naungana na wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwanza niseme kwa moyo wangu wa dhati naipongeza Hotuba ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika cchango wangu nitaanza na suala la ukusanyaji wa mapato. Kwa kuwa ukusanyaji wa mapato ni suala la Muungano, napenda pia tuiangalie bandari yetu ndogo ya Mkokotoni. Bandari ile huwa inachukua mizigo ya kwenda Tanga, Mombasa, Dar es Salaam na maeneo mengine kimya kimya. Sasa naona ni vizuri tuiangalie bandari yetu ya Mkokotoni tuweze kuiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika bandari yetu ya Mkokotoni ni vizuri pia tukaandaa kivuko ili tuweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Tumbatu. Wananchi wa Jimbo la Tumbatu kwanza hakuna gari hata moja, siyo kwamba Serikali imeshindwa kutokana na miundombinu iliyokuwa kule, hakuna.

Sasa ni vizuri basi tuwasaidie kuwe na kivuko cha uhakika kupitia ukusanyaji wa mapato utakaotokana katika bandari ile. Kabla sijaendelea kuchangia, napenda nikumbushe; wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, nilishasema kwamba inawezekana na itawezekana ifike wakati Waheshimiwa Wabunge tuanze kupimwa akili kabla ya kuingia Bungeni. *(Makofi, Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zipo, watu wana akili zao timamu, lakini wao wamegoma wenyewe kuongea kwa idadi yao, halafu mwenzao akiongea, wanamtilia fujo. *(Kicheko/Makofi/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina akili zangu timamu nimetumwa na wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuja kuwasemea. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Siwezi kuja hapa nikasaini posho ya mwezi ya kikao…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka naomba ukae…

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA: …**halafu nikakaa kimya.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka, naomba ukae, kuna taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa kwa kitendo chao cha kila siku kukubali taarifa, wanatuchanganya, tunashindwa kumaliza sentensi zetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka, naomba ukae.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Tafadhali naomba ukae Mheshimiwa Malembeka. Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Wakulipe muda wako…

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachangia bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa naona tena vikokotoni bandari… *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Soma kanuni!

**MBUNGE FULANI:** Nishapewa nafasi, kanuni ya nini? Kwani haijulikani hiyo! *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unayezungumza, naomba ufuate utaratibu. Naomba useme taarifa yako.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa ninayompa ni kwamba anachochangia, hakihusiani na Bunge hili. Anachochangia inabidi aende katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Ahsante sana. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka, endelea.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante. Kwanza taarifa yake naikataa kwa sababu hajitambui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa mapato ni wa Muungano, ndiyo maana na Mawaziri wa Fedha kule Zanzibar na hapa wapo. Sasa kwa kuwa

yeye hajui ukusanyaji wa mapato ni suala la Muungano, naomba akajifunze na aende kule Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu na ninaendelea. La pili nataka nikuhakikishie, kwa umri niliokua nao, sijawahi kumwambia *housegirl* wangu aache kazi kwa ajili ya kuangalia *TV* kwa sababu najua madhara yake. Mboga zitaungua, kazi zitakuwa hazifanyiki na ana muda maalum kwa kufanya ile kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu umetumwa na Jimbo lako, unkuja hapa unashindwa kuchania eti kwa sababu ya *TV*. Mbona *housegirls* wenu mnawakataza kuangalia *TV*? Mna matatizo gani? Huko kwenye *TV* kwenyewe kuna mambo yanafanyika ambayo hayaruhusiwi kuonekana hadharani. Watu wanabadilkishana Tai, watu wanapaka poda, watu wanabadilishana vipindi, hatuonyeshwi moja kwa moja. Vinazuiwa! Kwa nini Bunge mnaling'ang'ania hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 12, suala la viwanda. Naipongeza Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayoifanya. Ni mikakati iliyojipanga kwa ajili ya kuboresha na kuanzisha viwanda kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika mkakati ule, tuangalie upya wawekezaji wetu kutokana na kwamba kuna baadhi ya wawekezaji ambao wanapenda sana kuwanyanyasa wananchi wetu wakiwepo vijana wanaofanya kazi katika maeneo yale. Ninafurahia viwanda viwepo na vigawanye katika Kanda mbalimbali ili kila Mkoa uweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia ni mdau wa Jimbo la Ukonga, nina nyumba yangu kule na nimekuwa Diwani kwa miaka kumi. Kwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga Chama chake kimemkataza kusema, naomba niseme haya kwa niaba ya Mbunge wa Ukonga ambaye kanyamaza. *(Makofi/Vigelegele/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Ukonga nataka nizungumzie Barabara. Kuna barabara iliyoanzishwa miaka ya nyuma, naomba Serikali imalizie. Ni barabara ya Chanika - Kitanga mpaka Masaki, kuna barabara ya Chanika - Homboza mpaka Masaki, kuna barabara ya Mvuti kuelekea Dondwe, barabara ya Pugu – Majoe - Mbondole, barabara ya Mbondole -Msongola mpaka Mbande, barabara ambayo inatoka Banana – Kitunda - Kivule hadi Msongola.

Barabara hizo ziliweza kufanyakazi na wananchi wana shida na barabara zile na Mbunge wao amekatazwa kusema; ninaomba kama Mbunge wa Viti

Maalum mwenye hisia na Jimbo la Ukonga, nalisemea Jimbo hilo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nikiwa na uwakilishi wa wananchi napenda niingie katika ukurasa wa 54 Sekta ya Afya. Katika Jimbo la Ukonga, bado tuna Hospitali ya Kivule. Naishukuru Serikali hii imetenga fedha ya kuongeza kwa ajili ya kukamilisha hospitali ya Kivule. *(Makofi/ Vigelegele)*

**MHE. MWITA MWIKABE WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Naomba Serikali isaidie pia kwa ajili ya Zahanati. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naomba pia isaidie hospitali ya Chanika ya akina mama ya watoto ambayo…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** …ilianzishwa kwa nguvu kubwa ya Mheshimiwa Jerry Silaa akiwa Mstahiki Meya kwa ridhaa yake. Naomba Serikali i-*support* tukamilishe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka, naomba ukae kuna taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Zahanati ya Mbondolwe, Luhanga, Lubakaya na Yongwe, ziweze kufanya kazi katika Jimbo la Ukonga. Nataka nizungumzie kuhusu; eeh! *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka, naomba ukae, kuna taarifa. Haya Mtoa taarifa!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kanuni ya ngapi? *(Kelele)*

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Haya, mtoa taarifa!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 68(7), naomba nitoe tu taarifa kwamba Mheshimiwa aliyekuwa anachangia sio Mbunge wa Jimbo la Ukonga. Nipo mwenyewe mashine ya kusaga na kukoboa, mwanaume wa shoka, nimeenea kila sekta...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. MWITA MWIKABE WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawezi kulisemea Jimbo la Ukonga wala sijashindwa kuchangia. Nipo vizuri sana!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Aendelee kupiga makofi. Ndiyo maana mwenzie amekimbia Msongola ameenda Zanzibar. Kule tuko wanaume wenyewe. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Taarifa yako umeitoa wakati hujavaa vazi rasmi. Hujavaa tai Mheshimiwa! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika! *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malembeka, naomba uendelee. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba muda wangu uendelee kulindwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ngoja tuwavuruge! Mwongozo wa Spika!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa naikataa. Nimekuwa Diwani miaka kumi nikikaa ndani ya Jimbo la Ukonga, sikumjua. Haya ninayozungumza nina uhakikanayo, niliyapanga nikiwa Mwenyekiti wa Huduma za Jamii Manispaa ya Ilala.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuhusiana na vita dhidi ya rushwa na ufisadi. Napongeza kwa dhati juhudi zinazofanywa na Mheshimiwa Rais za kupasua majipu na ninaomba majipu haya yasiishie ndani ya wananchi wa huku, twende kwenye Vyama.

Hata kama mtu akibadilisha shati; akivua shati la kijani akivaa leupe, tumfuate huko huko, tukamtumbue. Kwa sababu wengine wamehama; wametoka huku wameenda upande wa pili. Tuwafuate tukawatumbue majipu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusiana na suala la vijana kwa upande wa bodaboda. Nafurahi kwamba Serikali hii imewatambua bodaboda, naomba waendelee kupewa mafunzo, waelekezwe waweze kukata Bima ya Afya, lakini pia naomba Serikali hii iandae utaratibu kuona jinsi gani ya kuagiza vifaa vya bandia kwa sababu sasa hivi tumepata walemavu wengi sana kutokana na suala la bodaboda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie ukurasa wa 21 kwa ajili ya suala zima la walemavu. Naishukuru Serikali yangu Tukufu ambayo ni sikivu, imeweza kutenga mambo maalumu kwa ajili ya walemavu. Ninaomba tuendelee kuwasaidia kupata miradi na kuwapa elimu, tuwasaidie kuwapangia maeneo ya kufanya biashara zao. Lakini pia tuangalie utaratibu wa kuwapunguzia masharti ili waweze kupata mikopo nafuu na kuendesha biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe masikitiko yangu; nasikitika sana kuona baadhi ya walemavu viungo vyao wanafanya kama vile mradi au kichekesho. Kile kitendo, binafsi mimi kinaniuma, kinaniudhi. Ninafahamu kabisa ulemavu siyo kushindwa, lakini bado wapo baadhi ya walemavu wanakubali kutumika kama kichekesho kwa ajili ya shughuli nyingine. Mimi hiyo tabia kwa kweli siipendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee zaidi pia kuhusiana na suala la maslahi ya Watumishi. Siku zote niseme kwamba kazi nzuri inavyoenda na kazi yoyote utamu wake fedha. Hatuwezi tukakaa kila siku tunataja *section* mbili tu; Walimu, Madaktari! Naomba nisemee sekta nyingine zote zilizobaki kwamba maslahi yao yaboreshwe ili waweze kufanya kazi vizuri na kwenda sambamba na kasi ya Hapa Kazi Tu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nizungumzie katika suala zima la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Malembeka, inatosha naomba ukae muda umemalizika.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Eeeh! Muda umeisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda umeisha namalizia kwa kusema kwamba nyoka wa kijani haumi, siku akiuma hana dawa. Naunga mkono hoja!

**MBUNGE FULANI:** Akae kama muda umeisha! *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu Waheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo si ndiyo! Si naomba mwongozo!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa hivi ni Mheshimiwa Allan Kiula.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipatia nafasi nami nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nachukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake. Hotuba hii imekaa vizuri kwa sababu imegusa maeneo yote ya utendaji kazi na maeneo yote ambayo ni matarajio ya nchi. Pia nampongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa utendaji kazi wake mzuri. Wanasema unakunywa chai ya moto na andazi moto. Maana yake nini? Maana yake unatoa ahadi, unaanza kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, elimu bila malipo imeanza kutekelezwa, changamoto zipo, inabidi sisi sasa tuziboreshe. Hotuba hii imejengwa katika msingi mzima wa Mipango ya Miaka Mitano. Kwa maana hiyo, imezingatia na ni hotuba ambayo ina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo habari ya mapato. Ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa mipango mbalimbali ambayo tunapanga ndani ya Bunge hili, ni lazima suala la mapato liangaliwe kwa kina. Ninapozungumzia mapato, maana yake ni nini? Maana yake ni lazima tupanue wigo wa mapato, tutafute vyanzo vipya vya mapato, tuachane na ule utamaduni wa kupandisha gharama kodi kwenye sigara, pombe lakini pia na kodi ya wafanyakazi. Lazima tupanue wigo wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi ni kubwa lazima tuirasimishe. Tukiirasimisha, wigo utapanuliwa, lakini pia wawekezaji wanaokuja kuwekeza ndani ya nchi yetu, inatakiwa tuziangalie kodi wanazostahiki kulipa. Kodi hizo zikiwekwa vizuri, tutapata mapato. Pia liko jambo ambalo na lenyewe sisi kama Wabunge inabidi tuliangalie. Yako mambo kwa sababu Sheria za Ukusanyaji wa Mapato zinatungwa na Bunge hili lakini imeshafikia mahali sisi Wabunge ndiyo tunazihoji. Sasa tunapozihoji, inakuwa ni changamoto kubwa.

Kwa hiyo, naomba Waziri anayehusika aje atuelimishe upya, hizi sheria zinazopitishwa hapa na zinazotumika. Kwa mfano, Sheria ya Uondoaji wa Mizigo Bandarini kwenda nje ya nchi, hizi *transit goods;* uamuzi ulifikiwa wa taratibu za kuondoa na ulipaji kodi, lakini wako watu ambao wanahoji na zilipita humu

humu ndani. Sasa ni muhimu jambo hilo na sisi tukalielewa kwa sababu sisi kama Wabunge tunatakiwa tuwe Walimu na ndio tuwaelekeze watu wetu. Kwa sababu mtu wa kijijini hawezi kujua hayo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa eneo hilo limeanza kuendeshwa na *Clearing and Forwading,* hao Mawakala wa Forodha. Haiwezekani! Kama sisi ni Wawakilishi wa wananchi lazima tulisimamie, kama sisi ni Wabunge, lazima tulisimamie na tuisaidie Serikali katika kutoa mwongozo na kuwaambia watu jambo lipi linatakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Cha pili, nizungumzie ajira. Nitajikita zaidi kwenye maeneo ya vijijini. Zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wetu ni wakulima. Sasa tunapozungumza ajira na kilimo, ina maana kilimo kinatoa ajira kubwa kwa watu wetu wa vijijini na kwa wananchi wetu wa vijijini. Jambo la muhimu ni nini? Wananchi wetu wanatakiwa wapate mbegu bora kwa bei rahisi, wapate pembejeo kwa bei rahisi. Mambo hayo yakifanyika, tunaweza kuchangia kupanua wigo wa ajira badala ya kutegemea hizi wanaita *white colour job* au Ajira za kuajiriwa maofisini. Kilimo ni sekta kubwa ambayo inaweza ikatoa ajira. Ukiangalia ukurasa wa 28 suala hilo limezungumziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 32 kuna suala la viwanda na kilimo. Ukienda kwa mfano Wilaya ya Mkalama, tunalima sana alizeti, vitunguu, mahindi na mazao mengine. Sasa lazima kuwe na muunganiko kati ya hii malighafi ambayo itakwenda viwandani. Kwa hiyo, kitu cha msingi zaidi ni kusisitiza suala la kilimo ambacho kitatoa malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kilimo, kuna suala la masoko. Wananchi wetu lazima tuwatafutie masoko. Tunawatafutia masoko vipi? Kwa kutengeneza masoko ya kukukusanyia mazao, kwa sababu mwananchi ananyonywa sasa hivi. Kwa mfano, kule Mkalama, kuna mtu anatembea na debe linaitwa Msumbiji; debe nane kwa debe sita. Sasa mkulima anapunjwa. Kwa hiyo, tukiwa na sehemu za kukusanyia mazao, kwa Mfano Kibaigwa kuna soko la Kimataifa na sehemu kama Iguguno kunaweza kukawa na soko la Kimataifa la kuuza mazao tukawasaidi wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ardhi. Maeneo mengi yamekuwa na migogoro ya ardhi ikiwemo Mkalama. Ipo migogoro mingi ya ardhi. Pia hao watu wanaokuja kupewa ardhi kubwa kubwa; kuna mtu anapewa ekari 700 na anapewa ndani ya kijiji, maana zinapimwa mpaka zinaingia ndani ya kijiji. Sasa hao wataalam wetu wanaona jambo hilo? Hilo ni jambo ambalo inabidi likemewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wilaya zinaanzishwa, hakuna Afisa Ardhi Mteule. Nalo ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, naomba Ofisi hii iangalie, kuwe

na Maafisa Ardhi Wateule. Wilaya inapoanzishwa, ateluliwe Afisa Ardhi Mteule na Hakimu wa Wilaya ili mambo yaweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la barabara. Hapa ndiyo ipo changamoto kubwa. Maana tunapozungumza suala la barabara, mimi huwa naangalia, wenzetu wa Dar es Salaam barabara zote ni lami, lakini ukienda Mkalama na maeneo mengine ya pembezoni barabara zote ni vumbi; na uwezo wa Halmashauri zetu wa kukusanya mapato ni mdogo sana. Kupandisha hadhi barabara ya Halmashauri yenyewe ni changamoto, acha kupandisha iwe barabara ya *TANROAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hilo linatakiwa liangaliwe kwa makini. Zipo barabara kwa mfano kutoka Mwangeza mpaka Endasiku, zipo barabara za kwenda Iramoto, zile hazipo kabisa kule ni mapalio tu, lakini maeneo hayo ndiyo yanayozalisha mazao kwa wingi kama alizeti na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kwa kuipongeza Serikali kwa kutoa pesa daraja la Sibiti kuanza kujengwa. Hapo ndipo sera ya kuunganisha Mkoa kwa Mkoa wa Singida na Simiyu, tutapata unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wamesema maji vijijini yamesambazwa kwa asilimia 72, lakini nikiangalia vijiji vyangu vyote havina maji, halafu asilimia 72 imetokea vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waziri mhusika anatakiwa angalie jambo hili, iko miradi ambayo imefadhiliwa na Benki ya Dunia, haijamaliza; lakini inahesabika kwamba mradi upo na unafanya kazi. Wahandisi ni wa aina gani? Bomba za maji zinapita mtoni. Mto unakuja unazoa maji pale Iguguno, unasema mradi wa *World Bank*. Mradi wa *World Bank* lazima uwe na hadhi ya *World Bank*, siyo unakuwa mradi kama wa kimachinga tena. Kwa hiyo, Waziri wa Maji anatakiwa aangalie matumizi ya pesa na watu wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya mpya zina changamoto kubwa; Hospitali za Wilaya hazipo! Kama hazipo, Halmashauri ikijitahidi hata ikiweka kwenye mpango haiwezi, kwa sababu kipato ni kidogo. Wilaya hizi ziangaliwe kwa jicho la karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ulinzi na usalama. Jeshi la Polisi na wengine lazima waangaliwe kwa karibu. Sisi tunaokaa porini kule, amezungumza Mheshimiwa Musukuma huko, watu wanakatwa mapanga tu! Kwetu, vijana wa bodaboda wanatekwa tu! Suala la ulinzi lazima liangaliwe, magari na mafuta yapelekwe ili tuweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Wilaya mpya na wenyewe ni changamoto. Kwa mfano, Wilaya ya Mkalama, mwaka 2014 ilitengewa shilingi bilioni moja ikapewa Shilingi milioni 450; mwaka huu ilitengewa shilingi bilioni moja, haijapelekwa hata senti tano! Hiyo Wilaya mpya itakwisha lini? Hiyo na yenyewe ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, niipongeze tena hotuba ya Waziri Mkuu, naunga hoja mkono, tushikamane. Watu walikuwa wanataka maamuzi magumu, haya ndiyo maamuzi magumu. Ukiangalia maeneo yote yaliyotumbuliwa, yameguswa maeneo ambayo hayajawahi kuguswa. Sasa maeneo hayo yaliyoguswa, wameguswa ndugu zetu, kaka zetu; tuvumilie! Tunataka kujenga Tanzania mpya. Utajengaje Tanzania mpya kama huchukui hatua? Nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa Kujali muda, sasa tunakwenda na Mheshimiwa Zainab Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kukutana katika Bunge hili Tukufu kujadili mambo muhimu kwa maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kupongeza jitihada za Rais wetu wa awamu ya tano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli za kuboresha maisha ya Watanzania, lakini za kupambana na rushwa, kujenga nidhamu na uwajibikaji kwa wananchi na watumishi wa umma. *(Makofi)*

Aidha, kwa muktadha huo ninaishauri Serikali iimarishe Taasisi ya Kupambana na Rushwa ili iweze kufanya majukumu yake vizuri na kwa weledi. Sanjari na hilo, Serikali iweze kuimarisha Taasisi za Kutoa na Kusimamia haki ili kulinda haki za Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kipekee nimpongeze Waziri Mkuu kwa kasi yake katika usimamizi wa Serikali, lakini pia kwa ziara yake aliyoifanya Mkoani Kigoma. Hakika ziara yake imeacha manufaa makubwa sana na hasa katika ulinzi na usalama wa Taifa letu hili. Pia imewaacha Watanzania na wananchi wa Mkoa wa Kigoma wakiwa na ari na imani kubwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi; Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujielekeza katika ukurasa wa 46 wa hotuba ya Waziri Mkuu ambayo inazungumzia nishati. Ni dhahiri kwamba katika maendeleo ya viwanda nchini, haitowezekana maendeleo hayo kufanikiwa pasipokuwa na nishati ya umeme na umeme wa kutosha na wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nangependa kuchukua fursa hii kupongeza jitihada za Serikali za kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme kutoka *Megawatts* 1226.24 katika mwaka 2015 mpaka *Megawatts* 1,516.24 kwa Januari, 2016, ambalo ni ongezeko la asilimia 24 na ambalo limetokana na maamuzi sahihi ya Serikali ya kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la gesi. Pamoja na mradi wa kufua umeme wa Kinyeresi I ambao unazalisha *Megawatts* 150. Aidha, napenda kuunga mkono ujenzi wa Kinyerezi II ambayo itazalisha *Megawatts* 240.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa lile lengo la Serikali la kipindi cha miaka mitano la kuhakikisha kwamba kuna uzalishaji wa umeme wa kufikia kiwango cha *Megawatts* 4,915 linafikiwa pasipo na shaka. Nami nina imani kabisa kwamba itakapofika mwaka 2020 asilimia 60 ya Watanzania wataweza kupata nishati hii muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani mafanikio makubwa sana ya mikakati hii ya kuzalisha umeme utafaidisha sana vijana. Utawafaidisha kwa sababu utaweza kukuza uchumi na tutaingia katika uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda utaweza kuleta ajira kwa vijana, kwa maana wataweza kuajiriwa katika viwanda, lakini wao wenyewe wataweza kutumia nishati hii ya umeme kuanzisha viwanda vidogo. Kwa mfano, kuanzisha mashine za kukoboa, viwanda vidogo vya kukamua juisi, kukamua mafuta ya alizeti, ufyatuzi wa matofali kwa kutumia mashine za umeme. Kwa hakika mipango hii madhubuti sisi kama vijana tunaiunga mkono kwa sababu inatunufaisha sisi vijana moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kupongeza jitihada za kipekee za Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo, za kupunguza bei ya umeme. Punguzo la umeme linapelekea punguzo katika gharama za uzalishaji na gharama za uzalishaji zinapopungua, zinaleta upatikanaji wa faida; na faida inayopatikana inaweza kukuza uchumi zaidi, lakini kurahisisha na kuhakikisha kwamba ajira za vijana zinaendelea kuwepo, kwa sababu biashara hazitakufa, viwanda vitaendelea kuwepo, lakini na wao wenyewe vijana kwa faida wanazopata katika biashara zao, wataweza kunufaika na kukuza zaidi uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba sana jitihada hizi za Serikali ziendelee na Serikali itambue kwamba sisi vijana tunathamini na kuunga mkono jitihada hizi, maana sisi ni wanufaikaji wa kwanza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana jitihada za Serikali kupanua mradi wa *REA* awamu ya pili, kufikia katika vijiji 1,669 katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja 2015/2016. Vijana wa Mkoa wa Kigoma Wilaya Kakonko,

Buhigwe na Uvinza wananufaika sana na jitihada hizi kwa sababu wamesogezewa nishati ya umeme; na hivyo wao wenyewe wanaweza kufanya shughuli mbalimbali za kijasiriamali, ambazo zinahitaji nishati hii muhimu ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kupongeza jitihada ya Serikali katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuanzisha Mfuko wa Shilingi milioni 50 kwa kila Mtaa na kila Kijiji. Napenda kuishauri Serikali kwamba iweke maandalizi mazuri na nafahamu kuna jitihada zinazofanywa na Serikali kuandaa maandalizi mazuri ya Mfuko huu. Napenda kuishauri zaidi Serikali, iboreshe na kuimarisha Mfuko wa Maendeleo wa Vijana *(Youth Development Fund)*. Katika Mfuko huu, tumeona vijana wengi wameweza kufaidika kwa kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao za kijasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kumejitokeza changamoto mbalimbali, hivyo napenda sana Serikali ichukue mfano au itumie uzoefu na changamoto ilizopata katika kuendesha na kusimamia Mfuko huu wa *Youth Development Fund* ili iweze kutengeneza mfumo bora zaidi utakaosimamia Mfuko huo wa shilingi milioni 50 kwa kila Kijiji na kila Mtaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kupongeza mipango endelevu ya kukuza uchumi wa viwanda, lakini inabidi tufahamu kwamba katika mipango hii endelevu ya kukuza uchumi wa viwanda, ni lazima mipango hii iende sambamba na uzalishaji wa nguvu kazi yenye weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutoa elimu ya bure kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari. Imani yangu ni kwamba tunapoelekea katika uchumi wa viwanda, inabidi tufanye jitihada zinazoonekana za kuandaa nguvukazi kwa kuwapatia wanafunzi wetu elimu ya kutosha na yenye ubora wa kuwaandaa kupokea na kukabiliana na changamoto na uchumi wa kati na ushindani wa ajira, biashara na taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutegemei hapo haadaye tutakapokuwa na uchumi wa viwanda vijana au ajira ziende kwa watu wa nje. Tunategemea sana kwamba uchumi wa Viwanda utawanufaisha vijana wetu wa ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Katimba. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona jioni hii, nami nitumie fursa hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimpongeze kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba iliyogusa maeneo mengi ambayo kwa nchi hii tunahitaji viongozi kama hawa ambao walithubutu kutumbua jipu ambalo lilikaa muda mrefu la watu ku-*bypass* bomba la kushusha mafuta bandarini, lakini kuzima mita kupima kiwango cha mafuta kinachoingia nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imegusa maeneo yote muhimu ikiwemo elimu, afya, maji, miundombinu na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kipekee Waheshimiwa Mawaziri wanaomsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Abdallah Possi. Ni watu ambao wamekuwa na ushirikiano mkubwa, mimi niko katika Kamati ambayo ipo chini ya Wizara yake; Kamati ya UKIMWI na Masuala ya Madawa ya Kulevya. Wamekuwa karibu sana nasi pale tulipowahitaji na wamekuwa wakitushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kuchangia kwa kuomba mambo machache yaweze kufanyiwa jitihada za makusudi. Suala zima la ajira kwa vijana wetu, lakini na akinamama ambao nchi hii ndiyo inawategemea sana katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sasa tukaelekeza mawazo yetu katika kubadilisha kilimo hiki cha kutegemea mvua; tukatoka hapo tukaanzisha kilimo cha umwagiliaji; kilimo ambacho kama kitatiliwa mkazo, nchi hii tutatoka kule ambako tuko na tutakwenda kule ambako tunatolea mifano nchi za wenzetu; Malaysia, Vietnam na nchi nyingine ambazo tulikuwa nazo *level* sawa ya uchumi. Lazima tuthubutu kidogo, tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu kuna bwawa la Itagata, zuri tu, Serikali imewekeza pesa za kutosha, lakini lile bwawa linavuja. Naomba sasa ifanyike juhudi za makusudi liweze kuzibwa ili wananchi; vijana wa pale wapate ajira, wajiajiri wenyewe kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuajiri vijana wengi, ni lazima pia tufungue miundombinu ya barabara; waweze kujiajiri kwa kununua mazao na kuuza. Pia katika maeneo mengi ni wakulima wazuri, waweze kutoka na kufika haraka katika masoko ambayo yako katika maeneo ya miji likiwemo Soko la Kimataifa la Kibaigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hili suala la elimu bure. Naipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuliona hili. Kuna changamoto kadhaa ambazo naamini zikifanyiwa kazi zitakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika milioni 50 kwa kila kijiji. Kabla ya hizi shilingi milioni 50, kulikuwa na mabilioni ya Mheshimiwa Kikwete katika Serikali iliyopita. Kulikuwa na changamoto kadhaa. Sasa tujifunze kutokana na changamoto zile! Mabilioni yale hayakufika katika vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmojawapo katika Jimbo langu, watu wangu hawakupata kukopeshwa hata kikundi kimoja. Kwa bahati nzuri hili linalenga vijiji na mitaa yetu. Kwa maana sasa utengenezwe utaratibu mzuri wa namna gani na watu gani watakopeshwa na urejeshaji utakuwa katika utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishauri mara nyingi vijana wangu wa maeneo yetu kwamba mabenki siyo rafiki sana hasa kwa vikundi vya vijana kwa sababu riba, mara nyingi ndiyo inakuwa faida ya wale ambao ni wajasiriamali. Kwa hili, naipongeza sana Serikali lakini iangalie tu changamoto ambazo zitajitokeza ili lisijekuwa gumu kama lile ambalo limepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hilo hilo la ajira kwa vijana, napenda sana nizungumzie suala la mbolea. Tumekuwa tukizungumzia ruzuku ya vocha za mbolea katika baadhi ya maeneo. Napendekeza kwamba, ni vizuri sasa tukabadilisha mtazamo, badala ya kutoa vocha ya mbolea, sasa Serikali iwekeze moja kwa moja katika mbolea yoyote ambayo itauzwa nchini iwe imepewa ruzuku. Tutaondoka mahali hapa pa kuweza kusukumana; huyu kaiba, hapa halikutekelezwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nzima ikauza mbolea ya ruzuku, itaondoa gharama hizi za kusafirisha mbolea kwa Sh. 3,000/= kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora. Itaondoa msukumano ambao upo, watu badala ya kufanya kazi nyingine, tunafutilia nani alipewa vocha na hakuifikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko wa mbolea wa kilo 50 au 25, ni sawasawa na mfuko wa *cement*. Mfuko wa *cement* kuutoa Dar es Salaam mpaka Tabora, unapita pale kwangu Itigi, unapelekwa kwa Sh. 500/= tu, lakini ulizia mfuko wa mbolea, utafikiri umebeba tani; mifuko sita ya *cement* inasafirishwa sawa na mfuko mmoja wa mbolea kwenda katika mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na udhaifu wa sera. Naomba tubadilishe, hakuna haja ya kuweka vocha, mbolea yote iwekewe ruzuku, ndiyo mahali ambapo Serikali itawekeza, kila mkulima anayetaka kununua mbolea, akute bei iko pale. Tutaondoka katika hili wazo la kuanza kusukumana na kutafuta nani kala na nani kafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la ulinzi na usalama, Jimbo langu ni Jimbo ambalo lina jiografia ngumu kidogo. Kutoka Makao Makuu ya Jimbo mpaka mwisho pale Rungwa kuna kilomita 190 karibu 200, Kituo cha Polisi kipo Itigi, hakina gari. Naomba sasa, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo ina Serikali, Mawaziri wake wasikie, watuletee gari mpya. Mara nyingi wamekuwa wakiwapa vijana wale magari makuukuu. Njia ni mbaya, barabara mbaya, gari bovu; huwezi kufika mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali yangu hii ni sikivu, naamini wamesikia. Vile vile kuna jambo dogo tu la usikivu wa redio ya Taifa katika maeneo ambapo mimi natoka. *TBC* haisikiki katika masafa ya *FM*. Kuna redio ambayo imeweka busta yake pale; Redio Mwangaza, ni redio ambayo inasikika vizuri sana. Sasa wakati mwingine mtu anahitaji kusikia habari kama hizi za Bunge.

Pale kwangu hawasikilizi, labda itokee mtu ana runinga kwa ule muda ambao umeamuliwa. Naomba sasa Serikali ilifanyie kazi hili la masafa ya Redio ya Taifa. Hizi nyingine tutaachia wawekezaji wenyewe, wataangalia namna gani ambayo watatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mawaziri wote wa Serikali hii ya *Ma-Doctor* na Maprofesa ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri wanayofanya, inapelekea hata rafiki zetu, watani zetu sasa wanafika mahali wanakuwa hawana cha kusema, wananyamaza tu na matokeo yake sasa tunawasemea sisi kuwaombea katika Majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa kulinda muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nitoe mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais (Sera, Bunge, Vijana, Kazi na Walemavu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli; vile vile napongeza

Baraza zima la Mawaziri kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya, lakini pia kuwapongeza kwa juhudi wanazotusaidia kwa kushirikiana na sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kuwapongeza Mawaziri ambao wamekuwa wakija katika Jimbo langu la Segerea kutatua changamoto mbalimbali ambazo zinatukabili; Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Jafo na Waheshimiwa wengine ambao walifika kama Mheshimiwa Angelina Mabula. Nawapongeza sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017, zimezungumziwa *program* mbili. *Program* ya kwanza ni *program* ya kukuza ujuzi wa vijana na *program* ya pili ni kwa ajili ya kuwasaidia vijana ili kuweza kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015/2016 iliandaliwa *program* na Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana ya wakati huo, ambayo ilitenga shilingi bilioni 4.1 ambayo iliweza kuwasaidia vijana waliohitimu mafunzo ya Chuo Kikuu au wahitimu wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizo fedha zilizotolewa hazikuweza kukidhi au kuwasaidia vijana wote ambao waliweza kumaliza; kwa sababu tukiangalia takwimu ya vijana wetu wanaomaliza Chuo Kikuu na pesa inayotengwa, inakuwa ni ndogo sana.

Kwa hiyo, naomba Serikali pamoja na kwamba inatenga hizi fedha kwa ajili ya wahitimu wetu wa Vyuo Vikuu, naomba waangalie hili suala kwa kuangalia mifumo mingine ya taasisi za kifedha ambazo zinaweza zikashirikiana na taasisi za kijamii kuona ni jinsi gani wanaweza wakaungana nao ili kuhakikisha wanawasaidia vijana wetu ambao wanamaliza kwa wingi sana Vyuo Vikuu lakini pesa za kuwasaidia kupata ujuzi au ajira au kujiajiri wenyewe zinakuwa ni ndogo. Kwa hiyo, naomba suala hilo waliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sura ya nne, kipengele cha nne, ukurasa wa 48 - Kazi na Ajira. Katika Mpango wa Maendeleo 2016/2017, zimezungumziwa *program* mbili kama nilivyosema; *program* moja ya ajira ambayo imeweza kutolewa shilingi bilioni moja, lakini *program* nyingine ya kukuza ujuzi ni shilingi bilioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hiki walichokifanya kwa ajili ya vijana wetu, kwa sababu tuna vijana wengi ambao wanahitaji kusaidiwa pamoja na kuandaliwa vizuri. Hizi fedha hazikidhi viwango vya vijana ambao wanamaliza Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuongelea suala la vijana wetu ambao wapo kwenye matabaka ya kati, ambao wamemaliza kidato cha nne au darasa la saba. Vijana wamekuwa wakijiajiri wenyewe. Sasa naomba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, iwaangalie hawa vijana kwa sababu wamekuwa wakijiajiri wenyewe, lakini pia mbali na kujiajiri wenyewe, kuna vijana wengine wana vipaji; lakini hawajawekwa kwenye huu mfumo wa kupata pesa kwa ajili ya kusaidiwa, kwa sababu huu mpango umeelezea kusaidia vijana tu ambao wamehitimu elimu ya juu. Sasa hawa vijana wa kati hatujawatengenezea mpango ni jinsi gani wanaweza wakasaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali ije na mpango maalum kwa ajili ya hawa vijana ambao wengine ni wasanii na wana vipaji. Kama Serikali ikiwatambua inawezekana ikawa ndiyo ajira yao ya kudumu. Pia pamoja na kuwa ajira ya kudumu, hao vijana wataweza kulipa kodi kwenye Serikali yetu. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaangalia watu wote kuanzia wenye elimu ya kati, lakini pia na wenye elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuzungumzia suala la bomoa bomoa katika Jimbo langu la Segerea. Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri ambaye aliweza kusimamisha hiyo bomoa bomoa isiendelee wakati walipokuwa wanabomoa, lakini kwa sasa hivi wananchi hawajui kinachoendelea. Tunajua kwamba kulikuwa kuna kesi sijui imetupiliwa mbali! Kwa hiyo, tunajua wananchi wengi wamejenga sehemu ambazo siyo salama, lakini wakati wanajenga, tuna Serikali ya Mtaa, pia tuna Serikali ya Kata. Hawa watu wamekuwa wakijenga, watu wanaangalia, kuna Watendaji wetu wapo kule wamekuwa wanawaruhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe, wanasiasa, tumekuwa tukifanya mikutano katika hayo maeneo, tukienda kwenye mikutano wanatuomba barabara, sisi tunakuja kwenye Manispaa zetu tunaomba barabara na wale watu wanapelekewa barabara. Pia wamepelekewa huduma nyingi za kijamii za kuwaonyesha kwamba sisi Serikali tunaunga mkono wenyewe waendelee kuishi pale. Sasa hivi tukisema kwamba tunawabomolea au tunawapa siku kadhaa ili waweze kutoka pale itakuwa hatujawatendea wananchi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie, ni kitu gani kitafanyika kuhusu bomoa bomoa? Watu wengi hawana elimu ya kujua kwamba mimi natakiwa nijenge mita 60 kutokea wapi? Kwa hiyo, Sheria ya Mazingira iliyokuja kwa sasa hivi, imekuja tu kuongea wananchi wengi ambao wanakaa sehemu ambazo mimi nipo, hawajui Sheria ya Mazingira. Sasa hivi ndiyo wameanza kuambiwa kwamba unatakiwa ujenge mita 60. Wananchi haelewi.

Kwa hiyo, naomba Serikali kabla hamjawabomolea inabidi kwanza mwende mkawape elimu. Pamoja na kuwapa elimu, hawa wananchi hawana kitu chochote. Kuna wengine walijengewa na watoto wao, watoto wao walishakufa, wamebaki wazee. Sasa hivi unavyokwenda unambomolea nyumba mwananchi kama yule, anakuwa hana sehemu ya kukimbilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa mhusika aende akaangalie ni jinsi gani tunaweza tukawasaidia. Tuna Manispaa tatu Dar es Salaam, tuna viwanja ambavyo vipo waangaliwe wananchi watasaidiwaje kupata viwanja ili tutokane na hili tatizo la bomoa bomoa. Najua Serikali ya Chama cha Mapinduzi siku zote imekuwa mstari wa mbele kuwaangalia wananchi wake na hasa wananchi wa hali ya chini. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ilila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, umemaliza muda wako, naomba ukae.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Edwin Sannda, atafuatia Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa naanza na itifaki ya pongezi kwa Rais wetu, Waziri Mkuu kwa mpango mzuri na timu yake nzima ya Mawaziri na Manaibu Waziri.

Kwa ujumla mpango huu ni mzuri sana, nami nimeupitia, nimeuangalia kwa kina, kwa upana wake na kwa ujumla wake ni mpango mzuri kweli kweli; wanastahili pongezi sana. *However,* kuna marekebisho kadhaa yanahitajika katika maeneo mbalimbali ili mwisho tuweze kuunga mkono hoja kikamilifu. Marekebisho hayo ndiyo yataukamilisha mpango huu uwe bora zaidi ya ulivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie maeneo mawili tu kwa leo; la kwanza ni lile la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Tukienda ukurasa wa 15, wanasema Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuwadhamini wajasiriamali wenye miradi inayokidhi vigezo kwenye taasisi za fedha ili wapate mikopo yenye masharti nafuu.

Haya mafunzo pamoja na mpango ule ambao upo ukurasa wa 16 wa shilingi milioni 50 kila kijiji, nafikiri mpango ni mzuri, utekelezaji wake ndiyo huwa tatizo.

Sasa ili tuweze kusaidia, nasi Wabunge kwanza tushirikishwe katika mpango wa utekelezaji mapema, tuwe nao. Tutakachofanya, kikubwa zaidi tunaenda kuandaa watu wetu, kwa sababu mpaka sasa hivi, wana matumaini makubwa kweli kweli, wanasubiri, wana kiu na kadri wanavyosubiri, tunatoa fursa ya maneno ambayo huenda siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tukiupata mapema kama Wawakilishi wa wale wananchi, tukaenda kule, tukauangalia, tukaanza kuujaribu, tukaanza kuustadi kwa kina, tutaweza kubaini upungufu na kuufanyia marekebisho. Kwa hiyo, kabla ya utekelezaji, tutakuwa tumeweka kila kitu kimekaa sawasawa na hatimaye muda wa utekelezaji unapofika, bajeti inakuwa imekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kushauri na hili lipo kwenye Wizara ya Fedha nafikiri kuna umuhimu sana katika maeneo ya kuboresha, ni kutengeneza *mechanism* ya *monitoring* na *control,* watu watakuwa wameshapata zile fursa, fedha zimetolewa lakini unawezaje kuhakikisha na kutengeneza mfumo wa kwamba tunawakagua hawa watu kadri wanavyokwenda? Vinginevyo hizi fedha zitatoka, mikopo itatolewa, lakini lile lengo tunalotaka lifikiwe mwisho, watu wafanikiwe, wapunguze umaskini, wainue uchumi, tutakuwa tumekwama kama hatutatengeneza mfumo na muundo imara wa *monitoring* na *control.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale wanapokosea, kweli watu wetu sio wote wana ujuzi wa ujasiriamali, wanafundishwa leo, halafu unamkabidhi hela mtu ambaye huenda hajashika kiwango hicho cha hela kwa muda mrefu au labda toka azaliwe, halafu ukategemea atafanikisha kadri tunavyotegemea, inaweza ikawa mtihani mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali, tutengeneze *mechanism* nzuri sana ya kuweza kuwachunguza na kuwasimamia hawa mpaka mwisho tuone matokeo yake. Hapo kweli tutakuwa tumefanikisha zoezi na azma yetu ya kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi ili tuweze kupunguza umaskini. Hili ndilo eneo ambalo tukiwawezesha hawa wananchi wa kawaida tunaosema ni maskini, ile *macro-economy* itakuwa *supported* vizuri sana na wananchi wa kawaida kwa sababu kila mmoja sasa atakuwa kidogo ana nguvu yake na anaweza kuendesha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo moja la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, naomba niachie hapo, nafikiri Waziri wetu wa Fedha na Mipango amelipata na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala zima la elimu. Mpango wa elimu ni mzuri, maeneo yote yameelezewa. Hili lipo kwenye ukurasa wa 49, naomba nisome kidogo mwone jinsi ambavyo inatakiwa iwe. Anasema:

"Hatua zinazochukuliwa zinalenga kuhakikisha kwamba elimu ya Tanzania ni ya viwango vya ubora wa hali ya juu ili kuwawezesha vijana wetu kukabiliana na changamoto za maisha ya kujiajiri wenyewe na kumudu ushindani katika soko la ajira la ndani kikanda na Kimataifa." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kauli ni nzuri sana na imewasilishwa vizuri kweli kweli, lakini lazima tuangalie kwa ujumla wake, ule mfumo, muundo na taratibu za utoaji wetu wa elimu kuanzia awali zinamjenga mtu kwa namna gani. Tunataka *practically* ziweze kutoa matunda au matokeo ya wanafunzi ambao ni *competent,* kwenye soko la ajira tukienda huko, tunaona namna tunavyo-*perform*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukilinganishwa tu na wenzetu wengine wa nchi za jirani na hapa tumezungumzia kikanda na tumezungumzia Kimataifa, *competence* yetu kwa kweli inahitaji kuboreshwa sana. Hili ndilo eneo ambalo kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu, kuna umuhimu sana wa kuliboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ubora tuuteremshe chini *practically,* tuhakikishe mifumo, muundo na utaratibu wetu wa kutoa elimu kuanzia chini, unamjenga kijana awe na uwezo, ajiamini, ajitambue kwenye suala zima la nidhamu ya mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumze jambo moja ambalo kwa kweli linanisikitisha na Naibu Waziri wa Elimu nafikiri yupo hapa. Watu wanaopata *Division IV* wanachukuliwa kwenda kuwa Walimu.

Sasa kipindi chote hiki ambacho tulikuwa na Walimu waliopata *Division IV* ndio wanakwenda kufundisha watu, halafu tunataka kujenga matunda ya watu ambao wana kiwango bora cha elimu, hapa kidogo pana mtihani, lazima tubadilishe hili, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatumia neno *failure,* kwamba *Division IV* ni *failure* ingawa kwa sasa kiwango cha *Division IV* inaonekana ni ufaulu. Sitaki kuamini kama ni ufaulu na ipo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia tubadilishe, ufaulu uishie *Division III*. Unapozungumzia *Division one, two, three,* ndiyo ufaulu. Sasa tunapiga mahesabu mpaka *Division IV* mtu anaaminika kwamba amefaulu halafu ndio hao wanaenda kufundisha, halafu tunategemea watoe *product* ambazo ni nzuri! Siyo rahisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujenge uwezo, tujenge wanafunzi wanaotoka wanajiamini huko nje; akienda anajieleza, anajiamini. Akiambiwa afanye kazi, ana *competence* ya kutosha.

Kwa hiyo, napenda nitumie fursa hii kuwasilisha marekebisho kwenye hii hotuba kwamba, suala zima la elimu, dhana ni nzuri sana, lakini ni lazima tuboreshe mfumo na muundo, utujengee na kutoa *competence* katika elimu yetu kuanzia *elementary* mpaka Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kubwa nataka niwasilishe hili la *Division III* kuendelea kuwa ufaulu, nashauri libadilishwe. Sasa tukishafanya maboresho hayo yote, kimsingi nitakuwa sina shida ya kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Kama hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia na baadaye Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Tunaendelea, kama Mheshimiwa Ghasia hayupo, namwita Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, hotuba yenye mashiko na inayotekeleza. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba sisi vijana tuko nyuma yake kwa ari na nguvu mpya. Usione wengine maumbo madogo, lakini tukiwa kwenye matukio, tunakuwa wakubwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kwa niaba yake naomba radhi kwa hotuba ambayo ameitoa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni. Kwa sababu nilishajitambulisha kuwa nilioa huko; kwa hiyo, aibu yake, aibu yangu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme…

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanaongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu jamani, tumpe nafasi! *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli naomba niwaambie, kama kweli ningekuwepo humu Bungeni asingeweza kutoa ile hotuba na hata mkichunguza mtagundua ile hotuba kama haijaandikiwa mlangoni, basi iliandikiwa humu humu, haraka haraka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Wewe endelea.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Sikilizeni Semina!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nitoe semina kidogo kwa Waheshimiwa Wabunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Goodluck naomba ukae, kuna taarifa. Wacha tusikilize taarifa.

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifungu cha 68(8) kikisomwa pamoja na kifungu cha 64(1)(g), Mbunge asitumie lugha ya kuudhi. Mbunge hawezi kusema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliandikia hotuba mlangoni. Haya ni maneno ya kuudhi. Naomba ayafute.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MBUNGE FULANI:** Endelea, endelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck, naomba uendelee.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na umbo langu dogo, lakini leo naomba nitoe semina kwa Wabunge wa Kambi ya wenzetu wa Upinzani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa!

**MBUNGE FULANI:** Waeleze!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunakuja kuapa aliitwa Mbunge mmoja mmoja pale mbele, hawakuitwa kundi, sawa! Kwa hiyo, naomba tunapofanya vitu, tufanye kwa maslahi ya Taifa, kwa mtu mmoja mmoja.

Nawapa mfano; sisi Wabunge wa CCM hatuna msalie Mtume. Ukituzingua, tunakupiga chini! Yule mnayemsujudu sasa hivi yuko upande wenu wa Upinzani, Mheshimiwa Lowassa; alituzingua, tukampiga chini.

Mheshimiwa Pinda mwaka 2015 alitetereka, tukataka tumtose, akachomokea dirishani. Kwa hiyo, CCM hatuna habari ya kuambiwa. Kwa hiyo, naomba tusifanye vitu kwa kuambiwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea, endelea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Sikilizeni semina.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Goodluck naomba ukae. Naomba ukae! Toa taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(8), ukisoma Kanuni ya 63(1) pamoja na kuzingatia Ibara ya 100 ambayo inatoa uhuru wa kutoa maoni, inasema Mbunge asiseme uongo, lakini ukienda Kanuni ya 64(1)(b) kanuni inaelekeza usitoe jambo ambalo haliko kwenye mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakuna mahali popote ambapo Mheshimiwa Lowassa ametajwa na makandokando yake na huko alikotoka. Kwa hiyo, naomba kwa sababu hayo

maneno yanakatazwa na Kanuni ya 63(5), naomba Mheshimiwa Mbunge anayeendelea kuchangia, ama athibitishe kauli yake au afute kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Sikilizeni semina!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(1) naisoma na 63 kama alivyosema mzungumzaji aliyekaa. Tarehe 22 Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani alisema Kambi ya Upinzani hawatachangia Bungeni kwa kuwa tumekiuka Katiba. Sasa tunawaona wanaendelea kuchangia kukatisha wazungumzaji.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mtu anazungumza taarifa kule, nawe naomba ukae.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuuliza, Kanuni ya 63(1) ni lini Kiongozi wa Kambi Rasmi wa Upinzani ametengua kauli yake?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatakiwi kujibu yeye, anatakiwa ajibu…!

**MBUNGE FULANI:** Kaa wewe!

**MBUNGE FULANI:** Asimame Kiongozi wa Upinzani atengue kwanza kauli yake, halafu ndio waendelee kuchangia. Wamezuiwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ufuate kanuni. Afute kauli kabla ya kuendelea ndiyo kanuni zinavyozungumza hapa.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu jamani, tufuate taratibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna! Athibitishe kauli au afute kauli, ndiyo mujibu wa kanuni inavyosemwa hapa.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MBUNGE FULANI:** Watu wanapewa miongozo halafu unasema aendelee tu kujibu hoja, haiwezekani!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa iko wapi?

**MHE. ALLY MOHAMED KEISSY:** Ally Keissy hapa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**MHE. ALLY MOHAMED KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji aliyezungumza, amemvunjia heshima Waziri Mstaafu Mzee Pinda kusema alitokea dirishani. Afute kauli yake mara moja. Tena namtaka afute kauli yake au athibitishe, Mheshimiwa Pinda lini alitaka kutokea dirishani? Huu ni utovu wa nidhamu, tena unaonekana huna adabu, huna nidhamu! *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu! Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, Mheshimiwa Goodluck, naomba uendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mwambieni ukweli.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu ni kutaka Wabunge wa Upinzani waelewe, nimewaambia kuwa natoa somo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utaratibu wa kusema Mwenyekiti, kasema sisi Chama cha Mapinduzi hatuna.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Jamani, mmoja mmoja!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba amalize.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaharibu! kuhusu utaratibu nakuomba, kuhusu utaratibu wa kanuni.

**MWENYEKITI:** Ameshasikia, anaendelea na utaratibu mzuri. Mheshimiwa Mbunge, endelea.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mwingine… *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo anayesikika Mwenyekiti, amesema, Mwenyekiti amesema; kila mkisimama hapa, Mwenyekiti amesema. Mimi namfahamu huyo Mwenyekiti kwa sababu nilioa huko tangu wakati niko kwenye mpango mkakati wa kumpata binti yao, yeye Mwenyekiti; nimeoa, yeye Mwenyekiti, nimezaa; mtoto wa kwanza, yeye Mwenyekiti; nimezaa mtoto wa pili, yeye Mwenyekiti. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwape taarifa tu, sasa hivi niko kwenye mpango yakinifu kwa ajili kumpata mtoto wa tatu lakini yeye haonyeshi hata utaratibu wa kuachia hicho kiti. Huyo atawaambia Mwenyekiti amesema mpaka lini? Sio kila anayevaa kilemba ni *fashion,* wengine wanaficha mapembe, wengine wananyoa vipara.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba tulielewe hilo. Hivyo vitu mtuachie sisi vijana tuvifanye; mambo ya Mwenyekiti kasema, Mwenyekiti kasema! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, juzi nilisikitika sana kusikia Mbunge amesema anahoji mshahara wa Rais. Cha kusikitisha zaidi huyo aliyehoji mshahara wa Rais

yeye anachangia kwenye Chama kila mwezi shilingi milioni tatu lakini hahoji hizo shilingi milioni tatu zinaenda wapi. Mshahara wa Rais uko kwenye Katiba. Angehoji kwanza, shilingi milioni tatu anazochanga kila mwezi kule zinakwenda wapi? Ni kwa sababu Mwenyekiti amesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi, kwanza naomba niwapongeze Wazanzibari…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchangiaji, naomba ujikite kwenye hoja tafadhali.

**MBUNGE FULANI:** Eeeeh! Kenge huyooo! Kenge haoooo! *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa nane wa hotuba ya Waziri Mkuu umezungumzia masuala ya siasa. Kwa hiyo, nimechagua kuchangia upande wa siasa. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, imenisikitisha zaidi hii Mwenyekiti amesema. Ndugu zangu Wazanzibari mmeingia kwenye mkenge wa Mwenyekiti amesema. Mmeambiwa msusie uchaguzi, mbona wao Uchaguzi wa Meya hawajasusia? *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Uchafuzi, siyo uchaguzi.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar, mmeambiwa msusie uchaguzi; sawa jamani! Mmeambiwa msusie uchaguzi. Zanzibar kuna misemo isemayo hivi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Goodluck, naomba ukae chini. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Aaahahaha! Umewachanganya! *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji wafuatao ni Mheshimiwa Innocent Bilakwate na baadaye atafuatia Mheshimiwa Livingstone Lusinde. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniambia nitaongea!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu! Kuhusu utaratibu!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaongoza Bunge kibabe, hutaki kusikiliza watu.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii kuchangia.

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zinakutaka unisikilize.

**MBUNGE FULANI:** Utasikilizwa baadaye, naomba mwingine aendelee kwanza. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKATWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu. Nakushukuru kunipa nafasi hii kuchangia. Kwanza nampongeza sana Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo ameiwasilisha mahali hapa. Ni hotuba nzuri ambayo inaongelea kila kitu; hakuna mahali ambapo hakugusa. Kabla sijafika huko, kwanza naipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutumbua majipu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inayotumbua majipu. Kwanza majibu yalianza kutumbuliwa pale walipoanza kukata jina la fisadi namba moja. Hili nalisema kwa sababu hao hao ndio waliosema ni fisadi, hatukuanzisha sisi.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Kwa hiyo, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi na nawapongeza Mawaziri, songeni mbele. Tuko nyuma yenu, tutapigana usiku na mchana mpaka kitaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais wetu kwa ujasiri mkubwa kwa kazi nzuri anayoifanya na Serikali nzima kwa ujumla. Niwaambie Waheshimiwa Mawaziri na Waziri wetu Mkuu, msiogope. Siku zote unapokwenda kwenye kituo cha mabasi au cha daladala, kuna watu wanaitwa wapiga debe. Siku zote wapiga debe huwa sio wasafiri. Waacheni wapiga debe wakapige debe, wanaosafiri wanajua wanakoenda. Sisi tunajua tunakoipeleka nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nijikite kwenye michango yangu. Naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inajitahidi kukusanya mapato. Naiomba Serikali yetu, bado Watanzania wanahitaji elimu kuhusu

kutumia hizi mashine za *electronic*. Ukienda maeneo mengi ya vijijini, hizi mashine hakuna. Tunapoteza mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa muda mfupi huu tuliotoka kwenye shilingi bilioni mia nane na kitu, kwenda kwenye shilingi trilioni 1.3 tunaweza kuvuka hata tukaelekea kwenye trilioni mbili.

Naomba tuongeze juhudi za kuwaelimisha Watanzania, kila tunachokinunua tupate risiti. Naiomba sana Serikali hasa katika suala la umeme, kuna maeneo mengine ambayo hawataweza kutumia mashine hizi; hakuna mitandao, hakuna umeme. Kwa mfano, kama kule kwetu Kyerwa, kuna maeneo mengi hakuna mitandao na hizi mashine hazitafika. Naomba Serikali ipeleke mitandao mahali ambapo hakuna mitandao ili tuweze kukusanya mapato mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nijikite kuipongeza Serikali; inasema tunaenda kwenye nchi ya viwanda; ili tuweze kufika kwenye nchi ya viwanda, kuna vitu ambavyo tunahitaji kwanza tuviangalie.

Kwanza, tuongeze nguvu kwenye umeme. Tunataka huu umeme wetu unaokwenda vijijini uweze kuwasaidia vijana wetu. Tunayo makundi mbalimbali, uzalishaji mkubwa uko vijijini; kilimo, kila kitu kinapatikana huko vijijini. Tukiweka umeme wa kutosha, tutaweza kufungua viwanda vidogo vidogo na vijana wetu ambao ndio nguvukazi wataweza kupata ajira. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali izingatie hayo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu. Tunayo mitambo mikubwa, tuna viwanda vikubwa, hivi viwanda vinahitaji kutumia umeme. Serikali ijikite kuongeza nguvu kwenye kuzalisha umeme, tunataka mitambo inayochimba madini iunganishwe kwenye *grid* ya Taifa. Itakapounganishwa kwenye *grid* ya Taifa, mapato yetu yataongezeka kwa sababu uzalishaji ambao wanatumia sasa hivi *generator* utapungua na mapato yataongezeka. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, tunao uwezo wa kuongeza umeme kwa sababu tayari tunayo gesi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, tunaposema tunaenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda, ni lazima tuboreshe miundombinu yetu iwe mizuri. Huwezi ukasema utajenga viwanda wakati miundombinu haiko vizuri. Kwa mfano, kama kule kwetu Kyerwa tunazalisha kila kitu lakini barabara ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, hili mliangalie. Kuna barabara inayotoka Murushaka kwenda Nkwenda mpaka Mulongo mpakani na Uganda. Hii barabara imesuswa kwa muda mrefu,

lakini unapoongelea uchumi wa Kyerwa ni pamoja na barabara hii. Hii ndiyo namba moja Kyerwa. Naiomba sana Serikali iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, kuna hao wananchi ambao wanazalisha, kwa mfano, kama kule kwetu, kuna masoko ambayo yameanza kujengwa pale Nkwenda na Mulongo; haya masoko yamesahaulika. Serikali iliyajenga, yamefikia nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, haya masoko yaendelezwe ili wananchi wawe na soko la uhakika. Siyo wanalima halafu wakishalima mazao yanaozea mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ijitahidi sana kuboresha miundombinu ili mazao haya yaweze kuuzwa mahali panapohusika. Mwananchi anapolima ajue nina uhakika wa kupeleka mazao yangu sokoni na kupata pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia maiomba Serikali hii ihakikishe inawakumbuka vijana wetu wa bodaboda. Hawa ni vijana wanaojiajiri, lakini hawa vijana wamekuwa kwenye mazingira ambayo siyo mazuri; vijana hawa wakati mwingine wanapata mateso mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti naiomba sana Serikali, kuwapa elimu hawa vijana na sisi wanasiasa ambao tuko humu Bungeni, tuwape elimu hawa vijana waweze kuwa na Bima ya Afya wapate matibabu. Vijana wengi wanapata ajali, wengine wanakatika miguu na mikono lakini hakuna Bima ya Afya. Mwingine hana pa kutibiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukaanzisha Mfuko hawa vijana wakawa na kitu kidogo ambacho wanaweka ili hata inapotokea, wanapopata ajali, anakuwa na pesa sehemu fulani ameiweka; siyo wanatumia tu. Wanahitaji elimu na nawaomba Wanasiasa wenzangu tuhakikishe hawa vijana wetu tunawapa elimu ili wajue ile ni ajira kama sisi wengine ambavyo tunajiwekea akiba na hawa vijana waweze kujiwekea akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilizungumzie, ili tuweze kufanikiwa haya yote ambayo tunayasema, tunahitaji kuboresha maslahi ya Watumishi wetu. Kuna watumishi wengine wanafanya kazi kwenye mazingira magumu. Mazingira yanakatisha tamaa. *(Makofi)*

Kwa mfano, kama kule kwetu Kyerwa kwenye Halmashauri, kuna gari moja tu. Hiyo gari ya Mkurugenzi, mara wanakwenda kwenye miradi; hawawezi wakafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, naomba tuboreshe mazingira yawe mazuri waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ili tuweze kwenda kwenye uchumi mzuri na maisha yawe mazuri, lazima Watanzania wapate maji safi na salama. Katika maeneo mengi hakuna maji. Tunaposema tunataka uchumi wa Mtanzania upande, ni pamoja na kuondoa hivi vitu ambavyo mnamfanya Mtanzania; kwa mfano, kuna mahali pengine mtu anakwenda kuchota maji masaa matano. Huyu mtu atafanyaje shughuli za maendeleo aweze kujipatia kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya tuyaangalie. Naiomba sana Serikali, tunapofanya haya, tusiangalie sehemu moja tu, hawa ni Watanzania, wote wafaidi kile kidogo tunachokipata. Unakuta miradi inaelekezwa eneo moja tu. Tuelekeze maeneo yote, tugawane kidogo, mwisho wa siku wote tufanikiwe maana wote ni Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali, suala la afya ni muhimu. Namwomba Waziri Afya, Kyerwa hatuna Hospitali ya Wilaya, lakini hata vile Vituo vya Afya vilivyopo havina madawa, naamini hii ni Serikali sikivu; na majipu haya ambayo wenzetu wa upande wa pili waliyapandikiza, tumewagundua, tunayatumbua kila siku; yanaondoka. Tunaamini wao ndio wanayapandikiza kwa sababu tunapoanza kuyatumbua, tunaona wanalalamika, maana wale ni wenzao. Kwa hiyo, tutaendelea kuyatumbua na Serikali imejipanga vizuri tutapata Watumishi waaminifu ambao hawakupandikizwa. Serikai hii itapaa sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naishukuru Serikali yangu na naamini ni sikivu. Kwa hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bilakwate. Sasa tunamalizia na mchangiaji wa mwisho kabla hatujaanza na wachangiaji Mawaziri na Manaibu Waziri; na sasa namkaribisha Mheshimiwa Lusinde

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo! Uliniambia nisubiri.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida yangu, nataka nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia zawadi ya uhai, kunipa afya bora ili niweze tena kusimama kwenye Bunge lako na niweze kutoa mchango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweke sawa kumbukumbu, katika Bunge hili kuna Wizara tatu zinachangiwa kwa mfumo wa aina yoyote mchangiaji anayotaka. Wizara ya kwanza ni Ofisi ya Waziri Mkuu, unachangia kwa hoja zozote unazojisikia Mbunge. Wizara ya pili ni TAMISEMI, unapiga kokote Mbunge unakotaka kupiga; na ya tatu ni *Finance Bill*, kwa hiyo, kama mtu huelewi, Mbunge ukisimama Wizara hizo, usiache kitu! Kula moto, tema madini, watu watakusikiliza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, amefanya kazi kubwa tangu ameteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Tuna uhakika kwamba Rais hajakosea kukupa kiti hicho Mheshimiwa Majaliwa na wala sisi Wabunge hatujakosea kukuidhinisha. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Majimbo ya Waheshimiwa Wabunge wengi hapa Tanzania likiwepo la Mtera, kuna baadhi ya miradi imekuwa ya muda mrefu, imekuwa miradi sugu. Tufanye utaratibu wa kila Mbunge akuandikie ni mradi gani umechukua muda mrefu haujatekelezwa, tukuletee ili kuwe na bajeti maalum ya kuondoa viporo vya miradi iliyopita. Tukifanya hivyo, tutakufanya uanze sasa kutekeleza miradi mipya wakati umekamilisha ile miradi ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilisema kwenye Bunge hili kwamba, ndugu zangu hawa wamechanganya mayai yote kwenye kapu moja, tupige. Nilizungumza nikiwa mahali hapa! Leo tumepiga, si mnaona biashara imekwisha?

Kwa hiyo, niwaambie tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, kuna wengine wanasema anatafuta umaarufu; hivi ukimshinda mtu anayesema mafuriko hayazuiwi kwa mikono, wewe ukayazuia, unataka umaarufu gani tena? Mheshimiwa Dkt. Magufuli anatafuta umaarufu upi kama amekuwa binadamu wa kwanza duniani kuzuia mafuriko kwa mikono? Anatafuta umaarufu upi? Tuliwaeleza hawa na leo nataka niwathibitishie, nataka niseme na nchi, nataka niwaambie Watanzania kwamba hawa jamaa mliowapigia kelele, leo hii wameonesha wamefeli, hawana uwezo wowote hata ndani ya Bunge hawa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Rais. Leo wanasimama hapa, watu wa Dar es Salaam mnisikilize. Anasimama hapa Kiongozi wa Upinzani anasema, Rais anafanya makosa kuamrisha pesa zilizokuwa ziende kwenye sherehe zijenge barabara ya Morocco. Wapinzani wanasema ni makosa. Hivi watu wa Dar es Salaam mnawapendea nini hawa? Hawa watu hawataki maendeleo! Wanataka domo! Mnawaona, wanataka waonekane kwenye *TV* wanasema bajeti ile na hela za kutengenezea barabara ya Mwanza, wanataka tukupe Mheshimiwa Nape halafu urushe *live TBC* ili waonekane hawa. Kutengeneza barabara na kuonekana kwenye *TV* lipi bora jamani?

**MBUNGE FULANI:** Kuonekana kwenye *TV*!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hapa na nazungumzia hapa kwenye ukurasa wa 11, 17 kipengele kinachohusu demokrasia. Someni hapo! Mheshimiwa Waziri Mkuu huwezi kukuza demokrasia kama una Wapinzani wa jinsi hii. Haiwezekani! Utakuzaje demokrasia katika nchi kama Wapinzani ulionao ni wa aina hii?

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mwenyekiti! Mwenyekiti taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde kaa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Ibara ya 68 kipengele cha (8). Ninachosema tu, naomba mzungumzaji aende kwenye mada, lakini mambo ya kunyambaliana na maneno, kusimangana, kutoleana ujeuri; humu ndani kila mtu anaweza kusema. Tumenyamaza waende kwenye hoja za msingi siyo kuambiana ujeuri. Kama ni ujeuri kila mtu ana ujeuri alikotoka nao.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini wewe! Nini sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, naomba uendelee.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kumwonya mzungumzaji anayezungumza. Mimi ni Mbunge *senior* na mwenye jina kubwa kuliko wewe. Unaposema kwenye Bunge hili, unamtolea mtu taarifa; wewe kama unaweza kusema umeambiwa, sema; kama hujafukuzwa Chama! Simama useme humu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kukua kwa demokrasia. Mimi hapa nataka leo nitoboe ndiyo maana nimesema leo najitoa muhanga. Katika maisha yangu nimewahi kuwa Kiongozi; Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la CHADEMA. Kule ndani kulikuwa na siri kubwa! Tulikuwa tumepanga siri wakati huo, niliyoikataa mimi, mpaka nikahama Chama hiki ya kuua Vyama vingine. CHADEMA wamefanikiwa kuua Vyama vyote hapa Tanzania.

Kwa hiyo, tunapozungumzia kukuza demokrasia tujue kwamba NCCR-Mageuzi ilikuwa na Wabunge watano na sasa ina Mbunge mmoja tu. Sijui ni maendeleo gani hayo? Wanaviua Vyama! Hawa wako kwa ajili ya kuua Vyama vingine! *CUF* walikuwa na Wabunge chungu nzima, sasa hivi Zanzibar sifuri. Hawa! Hawa wanaua Vyama vingine. Wanataka kubaki peke yao. *(Kicheko/Makofi/Vigelegele)*

Kwa hiyo, nakuomba Msajili wa Vyama vya Siasa, endelea kusajili Vyama, ukifanya mchezo nchi hii demokrasia itakufa kwasababu kuna Chama kinataka kuhodhi Vyama vingine vyote viwe ndani yake. Hawa wanataka kufanya hivyo! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM huko nyuma tulikuwa na zidumu fikra za Mwenyekiti. Tumetoka, hawa wameingia huko. Hawa sasa hivi zidumu fikra za Mwenyekiti, ndiyo maana unaona kila wakiambiwa kitu, wanafanya. Jambo la aibu sana! Unasimama kwenye Bunge hili, unasema Serikali imevunja Katiba, haiko Kikatiba, Serikali hii imekosea, kwa hiyo, hatutasema, lakini posho wanachukua, hawa! Yaani kama ni Waislamu; kama una Muislamu anasema hali nguruwe, anakula maini tu, ndiyo hawa! Wanasema Serikali hii imekosea, haiko Kikatiba, lakini mishahara na posho wanachukua hawa. Hawako tayari kusema! *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa nimegundua siyo tu tuna wafanyakazi hewa, tuna Wabunge hewa; hawa! Bunge hili lina Wabunge hewa! Nataka nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Nape. Wizara yako Mheshimiwa Nape ilikuwa haijawahi kuchangia maendeleo yoyote vijijini zaidi ya habari, tunasikia michezo lakini kwa mara ya kwanza, pesa ulizozizuia ambazo mmeshauri, sasa zinaelekea kuchimba visima vya maji. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka maji, hawataki kumwona Mbunge kwenye *TV*. Tunafahamu wamepata *political mileage* sana kwa sababu ya kusema mambo ya hovyo, watu wanayasikia, lakini kwa sasa watatakiwa kwenda kufanya kazi na kutoka jasho ili wananchi wawakubali. Ofisi ya Waziri Mkuu inashughulika na *TASAF*. Kwenye *TASAF* kuna malipo hewa. Wako watu wamekufa, lakini wanaendelea kupokea zile hela kama ambavyo tuna Wabunge wamekufa, hawazungumzi Bungeni, lakini wanapokea hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi hewa wako wengi sana kwenye nchi hii, tuwashughulikie. Kuna watu hapo wanazungumza habari ya kumponda Rais kwamba anakurupuka kuchukua maamuzi. Rais, watu wote anaowafukuza na wanaosimamishwa ni kweli majipu. Kwa mfano, mchukulie ndugu yangu Kabwe. Mbunge wa Upinzani alisimama hapa, Mheshimiwa Wenje akasema Kabwe ni jipu hafai atolewe na hawa wakampigia makofi. Leo kasimamishwa, hawa wanasema anaonewa. Huwezi kuwaelewa hawa! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wana-CCM pamoja na Waheshimiwa Mawaziri, kwa Baraza hili alililoliunda Mheshimiwa Rais, kule Mheshimiwa Majaliwa, pembeni Mheshimiwa Nape, kule kuna Mzee *Handsome*

*boy*, hapa Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Jenista Mhagama; hawa hawachomoki, ndiyo maana mnaona wanapiga kelele! Mnawaona wanapiga kelele hawa, anazungumza habari ya shule wakati CHADEMA ilimsimamisha Rajabu Jumbe kugombea Umakamu wa Rais akiwa darasa la saba, wewe umesahau? Sasa kama ninyi mlitaka kuleta Makamu wa Rais darasa la saba, itakuwa Mbunge! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali. Nataka niwaambieni, katika siasa duniani, mimi ni Mwanafalsafa, nikija kufa ndiyo mtaelewa kwamba yule mtu alikuwa wa namna gani. Katika watu ambao wanajua siasa na wamefanya, nawaambieni Tanzania hatuwezi kusonga mbele. Wana-CCM tujigawe; wawepo Wabunge wa Upinzani kutoka CCM, tuisaidie Serikali. Hawa tuachane nao! Hakuna kitu wanachokifanya hawa! Tukiendelea kuwaamini hawa, tutapoteza *point* nyingi sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote, Chama cha Upinzani kinakuwa na hoja moja tu. *ANC* wameshinda uchaguzi pale, hoja yao ilikuwa Ubaguzi; lakini hawa umeme, barabara, maji nini, hawa Wapinzani wa wapi? Hakuna Wapinzani wa namna hiyo! Mpinzani anakuwa na hoja moja tu. Anaijenga na anaaminika kwa watu. Hawa hawaaminiki, wanazungumza kila kitu! *(Kicheko/Makofi)*

Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, maendeleo katika nchi yetu kuna mikoa imechelewa kupata maendeleo kwa sababu *resources* zetu kuwa ndogo, igeukieni hiyo, acheni mikoa ambayo wananchi wameshiba, wanachagua Mbunge kuja kunyamaza tu Bungeni, achaneni nayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wa kutekeleza hoja hii, fanyeni kazi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia shida zao; hawa walionyamaza achaneni nao, hawana shida hawa. Mbunge anatoka nyumbani anakuja kukaa hivi, hasemi shida yoyote halafu baadaye wanakuja kwenye viti vya Mawaziri kunong'ona; Waziri mtu mzuri. Unafiki wa namna hiyo haukubaliki! Tunataka waseme wazi. Wakisimama hapa, wanakashifu Mawaziri, wanawatukaneni, halafu wanakuja kwenye kiti, naomba umeme. Tunataka maombi wanayoyaleta mezani kwenu, wayaseme wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunakufahamu, wewe ni mtaalam; umekuwa Bwana Mpango, umeongoza maeneo mengi. Tunataka safari hii, Serikali ya Awamu ya Tano, mipango yenu yote mliyoipanga na mkatupa asilimia 41 ya pesa, zishuke kwa wananchi ili maendeleo yapatikane, tuwakate mdomo hawa. Sasa hivi tutafanya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, tutatengeneza umoja wa kutembea Jimbo kwa Jimbo kuwaambia hawa wasichaguliwe tena 2020. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumzie barabara. Ukitoka hapa kwenda Iringa, kuna kipande cha barabara ambacho Mheshimiwa Rais ameshakiahidi kutoka barabara ya lami inayokwenda Iringa ipite barabara ya lami mpaka Hospitlai Teule ya Mvumi. Naomba kipande hicho mkikamilishe ili mimi niwe Mbunge wa maisha wa Jimbo lile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, katika wanasiasa wanaoniuma; nazungumzia demokrasia, lazima niwe mkweli; ananiuma sana kaka yangu Mheshimiwa James Mbatia. Mheshimiwa Mbatia ni mwanasiasa wa siku nyingi kuliko Mheshimiwa Mbowe. Sijui kalishwa nini, siku hizi anaambiwa na Mheshimiwa Mbowe, nyamaza! Naye ananyamaza kweli! Ananyamaza! Yaani sielewi kilichotokea! *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ilila kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mbatia ni Mwanasiasa wa siku nyingi, Chama chake kilikuwa na Wabunge watano. Akanambia yeye amesoma, mimi sijasoma, sasa anakwenda mbele. Kutoka watano kuja mmoja! *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde inatosha kwa leo, muda wako umemalizika!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Kweli hata mimi ambaye sijasoma siwezi kufanya ujinga kama huo! Hata mimi ambaye sijaenda shule, siwezi kufanya kitu cha namna hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Hawa tunawamudu, hamna kitu na tutahakikisha tunawafagia. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyo alikuwa mchangiaji wa mwisho kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge na sasa tunaanza na Waheshimiwa Mawaziri. Ataanza Waziri wa Fedha na Mipango…

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

**MWENYEKITI:** Baadaye atafuatia Waziri wa Mawasiliano, Mheshimiwa Nape, atafuatia Mwanasheria Mkuu na baadaye Naibu Waziri, Dkt. Abdallah Possi na mwisho atamalizia Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Mavunde.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

**MBUNGE FULANI:** Huruhusiwi kuchangia bwana!

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Kuna wengine unawaruhusu!

**MWENYEKITI:** Nikuwa nimeshaanza. Nilisema utaratibu wako nitausikiliza baadaye na kwa mujibu wa kanuni ya 68 mwisho inasema kwamba Mwenyekiti ndio mwenye maamuzi ya mwisho kuhusu utaratibu. Kwa hiyo, naomba utaratibu wako unisikilize baada ya kumaliza shughuli za leo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unafanya *double standard,* kuna mtu umempa hapa! Kwa hiyo, unafanya *double standard.*

**MBUNGE FULANI:** Eeh.

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unafanya *double standard.*

**MWENYEKITI:** Uliomba utaratibu ama ni taarifa?

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Naomba mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mwongozo nilishaanza kuzungumza; hukuomba mwongozo, uliomba utaratibu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Ukamkatalia!

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Niliomba utaratibu ukanikatalia.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti akisimama, unakaa.

**MWENYEKITI:** Uliomba utaratibu, hukuomba Mwongozo. Naomba ukae.

**MHE. JOHN H. WEGESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Naomba ukae. Tafadhali naomba ukae.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja. Sababu ya kuunga mkono hoja ni kutokana na mipango mizuri ya Serikali kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la uwajibikaji na maadili ndani ya Serikali, naipongeza Serikali kwa jinsi inavyorejesha nidhamu ya utumishi wa umma. Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu wameonesha kipaumbele chao cha kupambana na mafisadi kwa kuwatoa kazini na kufanyiwa uchunguzi ambao umewezesha wengine kufikishwa Mahakamani, naipongeza sana hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ukuzaji wa uchumi kupitia mpango wa kufanya mapinduzi ya viwanda, naiomba Serikali pamoja na kuanzisha viwanda vipya, tuangalie na viwanda vyetu vilivyokuwepo zamani, viwanda vifuatavyo tuviangalie kwa umuhimu wake katika Jiji la Dar es Salaam:-

(i) Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Mbagala - *TANITA*
(ii) Bora Shoes
*(iii) UFI*
*(iv) Tanzania Cables*
*(v) Aluminium Africa*
*(vi) Metal Box*
*(vii) Metal Product*
(viii) Urafiki *Textile*
(ix) Banda la Ngozi na viwanda vingine vingi ambavyo kwa sasa hakuna uzalishaji unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za afya, naiomba Serikali iondoe dhana ya wagonjwa au majeruhi wanaopata ajali kupitia katika Hospitali ya Mkoa badala ya kupelekwa moja kwa moja Muhimbili. Nasema hivyo kutokana na ukosefu wa vifaatiba katika Hospitali za Temeke, Amana na Mwananyamala. Wagonjwa wanaopata ajali mara zote wanapoteza fahamu katika Hospitali za Mikoa na wanafika Muhimbili wakiwa mahututi au wamekufa kabisa. Naiomba Serikali yangu sikivu ibadili utaratibu huu usiwe wa lazima sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira wezeshi; nashukuru Serikali kwa kuwaandalia vijana na akinamama, naipongeza Serikali kwa kuweka bajeti ya shilingi milioni 50 kwa kila Mtaa na Kijiji. Naiomba Serikali iweke mkazo wa kupeleka fedha maeneo yenye ujasiriamali. Maeneo yenye wingi wa vijana na wanawake ni pamoja na Mbagala, Mtoni, Tandika, Gongo la Mboto, Buguruni, Kariakoo, Ilala, Manzese, Mwenge, Kijitonyama, Tegeta, Ubungo, Bunju na Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo yana wingi wa wananchi ambao wanahitaji kupata mitaji, naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuangalia maeneo hayo kwa jicho la upekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kazi na hifadhi ya jamii, napongeza Wizara na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa jinsi alivyoendesha zoezi la kuwatoa wageni walioajiriwa nchini bila vibali, jambo alilolifanya ni kubwa na limesaidia sana. Naomba zoezi hili liwe endelevu kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Namtumbo tunashukuru sana kwa kupewa heshima kwa mwakilishi wao kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Imani hiyo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakika itazaa imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *MIVARAF* unaihusu sana Wilaya ya Namtumbo ambayo wakazi wake ni wakulima kwa zaidi ya asilimia tisini. Ujenzi wa miundombinu ya barabara za kuwezesha mazao ya wakulima kuyafikia masoko pamoja na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi mazao ni muhimu. Shughuli zinazofanyika katika mradi wa *MIVARAF* ni muhimu sana kwa wakulima wa Namtumbo. Nitashukuru kujulishwa mradi huo unaanza kutekelezwa lini Wilayani Namtumbo na una bajeti ya kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja ya bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCIA U. M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni uwezeshaji wananchi kiuchumi:-

(i) Serikali itoe mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vya wanawake wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Makambako,Wanging'ombe, Lupembe, Makete na Ludewa. Mafunzo hayo yalenge namna ya kuanzisha na kuendesha biashara ndogo na namna ya kutunza mitaji.

(ii) Serikali ianzishe Benki za Wanawake katika mikoa yote na hasa kwa Mkoa wa Njombe kwenye Wilaya zake zote.

(iii) Wajasiriamali wadogo wa Njombe hasa Wamachinga na wauza matunda hawana maeneo maalum kwa ajili ya biashara zao, naomba Serikali iwasaidie kuwatafutia maeneo mazuri ya kufanyia biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu vijana; naomba Serikali iwafikirie vijana wa Mkoa wa Njombe kwa kuhakikisha wanapata mikopo kupitia vikundi vya vijana, fedha ambazo ziko kwenye Halmashauri. Pia wapewe mafunzo ya namna ya kuanzisha na kuendesha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo; Serikali ianzishe Benki za Kilimo katika Mkoa wa Njombe kila Wilaya, yaani Makete, Wangingo'mbe, Makambako, Lupembe, Ludewa na Njombe Mjini, pia wakulima wapewe mikopo kupitia Benki hiyo ya Wakulima kwa riba nafuu

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni suala la miundombinu; barabara zote za Mkoa wa Njombe, Njombe - Ludewa, Njombe - Makete, Njombe - Lupembe, zina hali mbaya. Naomba Serikali itenge bajeti mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kutengeneza barabara hizo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni suala la maji; katika Mkoa wa Njombe ni kubwa. Naomba Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya Mradi wa Maji katika Vijiji vya Lugenge, Halmashauri ya Mji wa Njombe na Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kuhusu mazingira; Halmashauri ya Mji wa Njombe ina tatizo kubwa la mlundikano wa taka kwenye vizimba na gari ni moja. Naomba Serikali itenge bajeti kwa ajili ya kuongeza magari ya takataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri walio katika Wizara yake kwa kutuletea bajeti ili tuweze kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imegusa kila eneo lakini yapo baadhi ya mambo ambayo nataka nipatiwe ufafanuzi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watu wenye ulemavu; niipongeze Serikali katika ukurasa wa 21 inasema inathamini mchango mkubwa wa watu wenye ulemavu katika maendeleo na kwamba wana haki sawa ya kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Hata hivyo, bado watu wengi wenye ulemavu wanapata mateso sababu Serikali haijaweza kutunga sheria kuhakikisha watu wanaomiliki vyombo vya usafiri wanahakikisha miundombinu inakuwa rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walemavu wengi wamekuwa wakipata mateso makubwa sana hasa wale wenye baiskeli kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine wanapokuwa wanasafiri umbali mrefu. Bado majengo mengi sana hayajaweza kuwa na miundombinu rafiki ya kumfanya mtu mwenye ulemavu aweze kuyatumia kama vile shule, hospitali, vituo vya afya hata ofisi zetu za Serikali, mtu mwenye ulemavu anapotaka huduma katika majengo hayo imekuwa ni mateso kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni lini Serikali itaweka sheria kuhakikisha zinalinda haki ya mtu mwenye ulemavu. Pia bado wetu wenye ulemavu wengi na hasa wale wasio na uwezo wa kupata baiskeli wapo nyumbani hawapati hata haki ya kusoma. Nashauri Serikali ihakikishe kila mwenye ulemavu anapatiwa baiskeli bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianzisha *program* ya kuwasaidia watu wenye ulemavu katika mkoa wangu, niliamua kuwathamini, kuwajali na kuwasaidia pale walipo, naelewa changamoto nyingi sana ambazo Serikali yetu inatakiwa kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya bure; niendelee kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kutoa elimu bila malipo nchini, imesisitiza kila mzazi kupeleka mtoto shule na asiyepeleka mtoto hatua kali itachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imeweka mkakati gani kuhakikisha hawa watoto wa mitaani au watoto wanaojulikana kama ombaomba nao wanapata hiyo haki ya kusoma? Ni nani anayewajibika ili watoto hawa wasome? Swali hili huwa najiuliza kila siku lakini huwa nakosa jibu, ningependa kujua mkakati wa Serikali kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri au pendekezo langu kwa Serikali, kwa kuwa kuna shule za watu binafsi na shule nyingi zimekuwa zikitoza fedha nyingi lakini nazo zimekuwa zikitozwa kodi na Serikali, kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwapeleka hawa watoto katika shule hizo ili zile shule zinazokubali kuwachukua na kuwasomesha hawa watoto wa mtaani shule hizo zipunguziwe kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya wazabuni, wazabuni wa nchi hii bado wana mateso makubwa sana pamoja na kuwa walijitahidi kutoa huduma kwa Serikali yetu, kuna baadhi ya wazabuni ambao toka awamu

zilizopita wamekuwa wakifuatilia malipo yao bila mafanikio. Serikali itambue kwamba wazabuni hawa wengi wao ni wale waliochukua mikopo benki na kuna wazabuni ambao wamesababishiwa kutaka kuuziwa dhamana zao walizoweka rehani ili wapatiwe mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itambue kuwa wazabuni hawa pia wanadaiwa na kodi ya mapato, kwa sababu sheria inasema ukishatoa *invoice* kwa mzabuni wako unatakiwa ulipe kodi, sasa wanalipa kutoka wapi wakati bado hawajalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuhakiki madeni ya wazabuni bado hatma ya malipo haijajulikana. Ningependa kujua Serikali hii ya Awamu ya Tano imejipanga vipi kuhakikisha wazabuni wanalipwa kwa wakati ili kumwondolea adha ambayo mzabuni amekuwa akiipata na imesababisha wazabuni wengi kufilisika na kufunga biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali wa kutoa milioni hamsini kila kijiji; naendelea kutoa pongezi zangu kwa Serikali na Rais wa Awamu hii ya Tano kwa kuwa na mpango wa kupeleka milioni 50 kila kijiji. Sasa napenda kujua, Serikali imejipangaje kutoa elimu ya kuwatayarisha walengwa ili kuhakikisha pesa hizi zitakapoanza kutolewa zinawafikia walengwa na zinawasaidia, pia kuweza kurudishwa ili ziweze kuwa na mzunguko, kwa kuwa ukimpatia mlengwa akazirudisha zitasaidia walengwa wengi kufikiwa. Tuna rundo kubwa sana la akinamama ambao wameweza kuwa na uthubutu wa kufanya biashara, lakini hawana mitaji, sasa hili jambo litakuwa ndiyo suluhisho ya mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira zisizo rasmi; napenda kujua ni lini Serikali itarasimisha ajira zisizo rasmi? Kwa mfano, Mkoa wetu wa Iringa ni Mkoa ambao vijana wengi wamekuwa wakipata ajira ya kufanya kazi za ndani *(house girl au house boy),* pia tumekuwa na mkataba wa Kimataifa na nchi yetu kuridhia, bado ajira hii haijarasimishwa imekuwa ikisababisha vijana wengi kufanyiwa vitendo vya kikatili, kunyanyaswa, kubakwa, kupata mimba zisizotarajiwa na kuambukizwa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni lini ajira hii itarasimishwa ili vijana wetu waweze kutendewa haki na hata kujiunga katika Mifuko ya Jamii, kuwekewa bima ya afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji ya vikongwe; haya mauaji ya vikongwe hasa Mikoa ya Kanda ya Ziwa yamekuwa ni tishio na mauaji haya yamedumu kwa muda mrefu sana. Ningependa kujua Serikali imejipanga vipi kukomesha ukatili huu wanaofanyiwa vikongwe kwa kushirikishwa na imani za kishirikiana? Je, toka mauaji haya yameanza kufanyika ni vikongwe wangapi wameuawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kumaliza miradi ya zamani. Ningependa kujua mpango wa Serikali kuhakikisha inamaliza miradi iliyochukua muda mrefu kukamilika. Kwa mfano, katika Halmashauri yetu upo mradi wa machinjio, mradi huu umechukua muda mrefu sana kukamilika. Ni imani yangu kuwa mradi huu ukikamilika Manispaa yetu itakuwa na chanzo kizuri sana cha mapato na pia Halmashauri itaongeza ajira kwa vijana wetu, hivyo ningeshauri Serikali ifanye tathmini ya vile vyanzo ambavyo vinaweza kutuongezea mapato na miradi yake ipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji; niendelee kuipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza *Program* ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji safi, salama na ya kutosha. Imani yangu ni kuwa, kama *program* hiyo itakamilika, nia ya Serikali kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani itatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Iringa hauna tatizo la maji, bali tatizo kubwa ni usambazaji wa maji. Kwa mfano, Wilaya ya Kilolo ina mito mingi, Serikali inashindwaje kutoa maji kutoka kwenye Mto Lukosi, Ruaha na Mtitu? Nina imani kabisa kama Serikali ingesambaza maji kupitia vyanzo vya mito hii, ingeweza kutumia gharama nafuu sana ya uhakika kuliko kuchimba visima visivyokuwa na tafiti za kutosha na kusababisha pesa nyingi kutumika katika tafiti badala ya kutumia vyanzo vya mito, kwa sababu maji yanapokosekana ni mwanamke ndiye anayeteseka. Tunaomba ile ahadi ya kumtua mama ndoo kichwani ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma muhimu katika Wilaya mpya; kuna Wilaya ambazo zimeanzishwa muda mrefu sana, lakini bado hazijapatiwa huduma muhimu. Kwa mfano, Wilaya ya Kilolo ilipata hadhi ya kuwa Wilaya toka mwaka 2002, mpaka leo hii Serikali haijaweza kujenga Hospitali ya Wilaya, Makao Makuu ya Polisi, Mahakama ya Wilaya, pia barabara inayounganisha Makao Makuu na Wilaya mpaka leo hakuna lami pamoja na Halmashauri kuweka jitihada ya kutenga maeneo kwa ajili ya huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi hata hizi ahadi za Serikali za kujenga Wilaya mpya kama zitatekelezeka, ningependa kujua mpango wa Serikali wa kuhakikisha hizi Wilaya zilizoanzishwa muda mrefu utekelezaji wake upo vipi, ukamilishaji wa hizo huduma katika Makao Makuu ya Wilaya, kwa sababu wananchi wamekuwa wakipata shida sana kuzifuata hizo huduma na hasa kutokana na changamoto za miundombinu ya barabara zetu za vijiji zilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri. Pia, nawapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu, viongozi na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa utendaji mzuri na maandalizi mazuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kushukuru mema mengi tunayofanyiwa na Serikali yetu, Jimbo langu la Bagamoyo linakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinahitaji ufumbuzi:-

(i) Kuhusu kuwalipa fidia wananchi wa Zinga, Kerege na Kiromo wanaopisha mradi wa *EPZ*. Mazingira wezeshi ya uwekezaji ni pamoja na kuwalipa wananchi fidia ya ardhi na mali zao kupisha wawekezaji. Ni miaka tisa sasa wananchi hao bado wanasubiri kulipwa fidia zao. Serikali yetu Tukufu iwalipe fidia wananchi hawa mapema iwezekanavyo.

(ii) Ukosefu wa ajira kwa vijana wengi Jimboni Bagamoyo. Naiomba Serikali kujielekeza zaidi katika kuongeza fursa za mikopo na elimu ya ufundi na ujasiriamali kwa vijana katika JImbo la Bagamoyo. Serikali iharakishe mchakato wa ujenzi wa Chuo cha *VETA*, Wilaya ya Bagamoyo. Kwa mustakabali wa Taifa, naunga mkono uamuzi wa kukabidhi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa Wizara ya Elimu kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ufundi.

(iii) Azma ya Serikali kupanua na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji ni jambo jema sana. Naiomba Serikali yetu Tukufu itutengee Bagamoyo fedha za kutosha kutuwezesha kupanua miradi ya umwagiliaji hususan kujenga miundombinu katika miradi ya umwagiliaji ya *JICA - Bagamoyo* na Chauru na Kidogozero kule Chalinze. Serikali itutengee pia ruzuku kwa ajili ya pembejeo, msimu huu wa kilimo pembejeo zimekuwa tatizo sana.

(iv) Mtandao wa barabara zinazopitika vijijini ni nyenzo kubwa kwa ajili ya maendeleo ya uchumi na afya kwa wananchi wetu. Kasi ya ujenzi na ukarabati barabara za Bagamoyo Vijijini ni ndogo sana.

Barabara nyingi za Bagamoyo Vijijini ni mbovu na zinawagharimu wananchi kiuchumi na maisha yao. Barabara katika Kata za Fukayosi, Yombo, Kiromo, Zinga na Mapinga na barabara ya Mjini Bagamoyo ni mbovu sana. Serikali iongeze mafungu katika barabara na iangalie uwezekano wa kuunda Wakala wa Barabara Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii una fursa kubwa ya kuchangia pato la Taifa letu na utalii wa Tanzania ni wa namna mbalimbali ikiwemo utalii wa fukwe za bahari, utalii wa wanyamapori, utalii wa utamaduni, kihistoria na malikale. Bagamoyo ina fursa kubwa ya utalii wa kihistoria na malikale. Serikali ituwezeshe

kuhifadhi magofu ambayo yanazidi kumalizika mwaka hadi mwaka. Serikali itenge mafungu kwa ajili ya kazi hii. Pia, Wilaya iwezeshwe kufundisha vijana katika fani za kumhudumia mtalii mfano, kuongoza watalii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi kwako na Waheshimiwa wote kwa kuchaguliwa kuingia kwenye Bunge la Kumi na Moja. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaliwa kuwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa nami nampongeza sana. Nimeisoma hotuba yake nzuri na nimekubaliana naye, lakini naomba ufafanuzi kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 14 na 15, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi imeelezwa vizuri sana, naomba kunukuu:-

"Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuwadhamini wajasiriamali wenye miradi inayokidhi vigezo kwenye taasisi za fedha ili wapate mikopo yenye masharti nafuu"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba ufafanuzi wa kina kwani Tanzania ni kubwa na wajasiriamali ni wengi sana na hivyo si rahisi kama maandiko yalivyokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi kusema kuliko kutenda, hivi Waziri Mkuu anavyosema Serikali itaendelea kuwadhamini wajasiriamali anaweza kuwaeleza Watanzania ni lini dhamana hiyo ilitolewa na ni akina nani walifaidika? Endapo anazungumzia mabilioni ya JK, naomba kutofautiana naye kabisa kwani fedha zile zimetoweka na mzunguko sasa umekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia nzuri ya Serikali, naomba wananchi wapatiwe miradi zaidi ya fedha. Katika Awamu ya Kwanza, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwawezesha wajasiriamali na wakulima wa Kilimanjaro mradi wa kopa ng'ombe ambao uliweza kuwapatia lishe bora, nyumba za kisasa, ada za watoto shuleni na hatimaye maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aya ya 23 inasema, nanukuu:-

"Serikali imehamasisha uanzishaji na usajili wa vikundi vya kiuchumi kama vile Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na Benki za Jamii Vijijini (*VICOBA)*.

Serikali pia imesimamia uanzishwaji wa Taasisi mwamvuli ya kusimamia *VICOBA* inayoitwa *VICOBA FETA*. Takwimu zilizotolewa Februari, 2016 na Taasisi hiyo zinaonesha kuwa, kuna vikundi 100,000 vya *VICOBA* vyenye wanachama milioni 2.2 na mtaji wa shilingi trilioni 1.2. Ni jambo la kujivunia kwamba asilimia 79 ya wanachama wa *VICOBA* ni wanawake”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa njema alizotupa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu ushirika wa *SACCOS* na *VICOBA,* naomba atufafanulie ni jinsi gani wanawake hao watapatiwa mafunzo ya ushirika. Mpaka ninavyozungumza, jukumu kubwa limekuwa kwa Wabunge. Naomba nichukue nafasi hii nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atufafanulie jinsi ya kuwapatia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule ukurasa wa 16, aya ya 24, hotuba imeonesha wazi hali ya Vyama vya Ushirika, *SACCOS* zinazokidhi vigezo vya usajili nchini imepungua kutoka 5,559 mwaka 2013 hadi 3,856 mwaka 2015. Huu ni upungufu wa asilimia 30.6 sawasawa na 31%. Huu ni upungufu mkubwa na tatizo ni kwamba, Serikali haitoi kipaumbele kwa ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba kufafanua, Novemba 2006, Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Magufuli alitangaza Baraza la Mawaziri na ndipo umma wa Tanzania ulipozisikia Wizara zilizopo. Wengi mpaka sasa wanajiuliza hivi Wizara ya Ushirika iko wapi? Endapo ni idara, je, iko kwenye Wizara gani? Pendekezo ni kwamba, ipelekwe kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwenye Awamu ya Nne, Wizara hiyo ilikuwa kwenye Kilimo na ilijulikana kama Wizara ya Kilimo na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. J. P. Magufuli kwa kuonesha nia na uwezo mkubwa wa kuiongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake wote. Naomba waongeze juhudi na misimamo yao katika kuongoza Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesisitiza umuhimu wa wananchi kujiunga na matumizi ya soko la Marekani bila ya ushuru chini ya mpango wa *AGOA*. Hata hivyo, Serikali haikueleza namna itakavyochukua hatua za kuwaelimisha wananchi kujiunga na mpango huo. Ni vyema Serikali ikawaelekeza na kuwatayarisha wananchi ili kuwapa ujuzi na uelewa wa soko hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MAKAME MASHAKA FOUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na kuwa Rais wa Tanzania. Pia namshukuru Mungu na wananchi wa Jimbo la Kijini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo wa wananchi wa Tanzania. Serikali ikipe kipaumbele zaidi kwani zaidi ya 60% ya Watanzania wamejiajiri katika kilimo. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, naishauri Serikali kuweka kipaumbele kwenye kilimo cha umwagiliaji pia kutenga maeneo maalum hasa yenye ukosefu mkubwa wa mvua ili vijana wa maeneo hayo wapate kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ni nguvu kazi kubwa ya Taifa. Wako vijana wengi waliomaliza kusoma hawana kazi. Naishauri Serikali iweke utaratibu au mkakati wa kuhakikisha vijana wote wenye uwezo wa kufanya kazi wanafanya kazi na mkakati uanze vijijini hadi Taifa. Hali hii itasaidia vijana wengi kutokuhamia mjini na kuzurura hovyo mitaani. Naishauri Serikali iweke utaratibu maalum kwa kuwapatia taaluma nzuri ya uvuvi wa kisasa vijana wetu wanaoishi Ukanda wa Pwani ili wavue uvuvi wenye tija. Kwani uvuvi wa kizamani hauna tija kubwa kwa hivi sasa, mfano uvuvi wa madawa, kuchokoa kwa miguu umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati sasa kuchukua hatua kali kwa wafanyabiashara wa madawa ya kulevya kwani vijana wengi hivi sasa wanaathirika kiakili, wanakuwa wezi, wabakaji kutokana na kutumia madawa haya ya kulevya. Hivyo, naiomba Serikali isiwe na muhali kwa wasafirishaji na wasambazaji, wote wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuanzia Serikali ya Mitaa hadi Taifa ifanyie kazi kauli mbiu ya Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli isemayo Hapa Kazi Tu inayoenda sambamba na kutumbua majipu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni hifadhi ya jamii. Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliazimia kuanza kuwalipa pensheni wazee wote waliofikia umri mkubwa bila kujali walikuwa waajiriwa au laa, je, ni lini hasa ahadi hii ya kulipa pensheni kwa wazee hawa ambao wanaisubiri sana itatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni kwa lini Sera ya Hifadhi ya Jamii itaanza kutekelezwa kwa wananchi wote yaani wakulima, wafanyakazi, wafanyabiashara ili kila mwananchi afaidi mafao ya hifadhi ya jamii? Pia kuna mkakati gani wa kupunguza malalamiko ya wananchi ambao husumbuliwa sana na Mifuko ya Jamii kama *NSSF* na *PPF*? Je, hatua za kuboresha mifumo hii zimechukuliwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sekta binafsi. Hivi sasa sekta binafsi ndiyo mhimili mkuu wa kukuza uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wengi zaidi. Hata hivyo, waajiri wengi wa sekta hii hususani kilimo, ulinzi, huduma za hotelini, biashara na viwanda wamekuwa hawatoi mikataba na barua za ajira na wakati mwingine masharti ya kazi ni magumu sana na ya kinyonyaji, mazingira yanatisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baadhi ya waajiri hulipa mishahara duni ambayo haiendani na uzalishaji na haina tija. Lazima Serikali ihakikishe kwamba waajiri wote wanakuwa na mikataba na barua za ajira zinatolewa kwa wafanyakazi wote. Hili liende sambamba na kuimarisha Idara ya Kaguzi za Kazi ili ifanye kazi ya ukaguzi mara kwa mara na kutangaza hadharani waajiri ambao wanakiuka sheria za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali kuboresha kilimo. Ni lazima Serikali ije na makakati mpya wa kuinua kilimo ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa ruzuku, usambazaji wa pembejeo, masoko, chakula, kama vile kahawa, mahindi, maharage na kadhalika. Je, Serikali imefanya uchambuzi ili kuimarisha kilimo kwenye maeneo yenye tija na kujenga mazingira wezeshi ili kuongeza thamani ya mazao? Nashauri pale ambapo wananchi wanaweza kuuza nje mazao yao waruhusiwe kwani itasaidia kuongeza fedha za kigeni. Pia mkakati wa kuanzisha kilimo kikubwa ili kutoa ajira kwa vijana wetu umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni mkakati wa kuanza kutengeneza magari na vipuli. Serikali lazima ifanye maamuzi magumu ya kimkakati ili kuanzisha kiwanda cha kutengeneza magari na vipuli vyake. Kiwanda hiki kitasaidia kuchukua vijana wetu wengi ambao wana ufundi mkubwa. Kuna mafundi wazuri katika mikoa yetu. Ni muhimu kuanza kutengeneza magari ambayo yatatumia gesi na mafuta. Pia itasaidia kufanya utafiti na kuziangalia *projects* za wanafunzi wa vyuo vya ufundi ambazo ni nzuri sana. Maamuzi haya ni muhimu

sana ili kutoa ajira na kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kununulia magari na vipuli.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii katika maeneo matatu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uundwaji wa vikundi vya kijamii *(SACCOS)*. Mpaka sasa ni vikundi vichache vimeweza kusajiliwa kutokana na uelewa mdogo na kutotembelewa na wahusika kwa maana ya viongozi wa ushirika kutoka katika Halmashauri zetu. Mpango huu wa kusaidia vijiji shilingi milioni 50 binafsi najua kuna vikundi havitakuwa na sifa kutokana na ugumu huo wa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni habari. Kama nchi tume-*sign* mikataba mbalimbali ya haki ya kupata na kutoa habari kwa wananchi. Masikitiko yangu ni kwamba, Serikali imezuia vyombo binafsi kuonyesha, kuandika shughuli za Bunge zinazoendelea kwa kigezo cha kuwa na Bunge *TV* ambayo kimsingi haionyeshi na kama inaonyesha, inaonyesha kwa upendeleo. Isitoshe kuna magazeti yamefungiwa na kama Bunge halijajua makosa yao ili vyombo vingine vijifunze. Nashukuru kuleta Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari, labda utaleta uhuru katika habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni mawasiliano. Tumekuwa na vyombo au Makampuni mengi ya Simu, lakini wasiwasi wangu ni gharama zinazotozwa kwa wananchi. Gharama zinaongezeka katika ununuaji wa vocha na wananchi wengi hawana ujuzi wa kitaalam na kupelekea mwananchi wa kawaida kulipia gharama kubwa sana bila uangalizi wa wataalam watetezi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni uingizwaji wa simu feki unaofanywa na wafanyabiashara wachache na kujinufaisha na kuacha wananchi wanaathirika kwa ubovu wa simu hizo na hata hasara ya kuharibika baada ya muda mfupi. Nashauri *TBS* na wadau wanaolinda haki ya mlaji wafanye kazi yao kwa faida ya mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni masoko. Tumeingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, sijaona kama tumeandaa wananchi wetu hasa wanawake kuingia katika ushindani wa soko. Pia wananchi hawana elimu ya kibiashara hasa ya utalii ukilinganisha na jirani zetu ambao ni washindani wetu.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo ameanza na anaendelea kuifanya. Vile vile pongezi kwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake kwa kumsaidia

Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake. Naomba kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utalii; nimefurahishwa na kupata moyo kwa hatua ambazo Serikali itachukua kuimarisha utalli. Utalii ni sekta ambayo ina *potential* kubwa sana kwa uingizaji wa fedha za kigeni. Kwa upande wa Zanzibar, Sekta hii ni *leading sector* kwa mchango kwenye pato la Taifa. *However*, watalii wamekuwa wakilipia katika nchi zao na hivyo kukosesha pato kwa upande wa nchi. Uelewa mdogo wa changamoto hii kwa upande wa Kampuni za Kitalii kwa hapa nyumbani, umesababisha tabia hii kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati ambao utaandaliwa uhakikishe kwa kiwango kikubwa unashirikisha Makampuni ya Kitalii ya hapa nyumbani kuzungumzia changamoto hii na utatuzi wake. Vile vile kwa kuwa Zanzibar inategemea sana utalii, mkakati ushirikishe wadau wa Zanzibar kwa kiwango kikubwa cha majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI; wakati tukiwa kwenye Kamati, imeonekana bajeti nyingi zimeweka eneo la mkakati wa kudhibiti UKIMWI, kama ni eneo ambalo linasubiri fedha kutoka kwa wafadhili. Hii ni hatari, afya za wananchi na matibabu yake, hayawezi kuwekwa katika mikono ya wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kwenye *activities* zetu ambazo tunazifadhili kwa fedha yetu ya ndani, *issues* za *HIV/AIDS*, *Women, Climate change and environment,* ziwe *mainstreamed* humo. Tusisubiri hadi fedha za wafadhili zifike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa Mapato; eneo hili ni gumu na lina changamoto nyingi, hata hivyo pongezi kwa Serikali kwa kulipa mtazamo maalum suala la ukusanyaji wa mapato. Matumizi ya mashine ya *electronics (EFDs)* ziambatane na mafunzo ya watu wetu katika matumizi hayo, hususan kwenye Halmashauri zetu. Eneo hili la ukusanyaji wa mapato ni eneo gumu sana, lakini ni muhimu kuliko yote. Maendeleo yetu bila ya mapato yatokanayo na vyanzo vyetu vya ndani yatakuwa ni magumu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *approach* ya utoaji wa elimu ibadilike *now*, ijielekeze sana kwa wananchi ili waelewe umuhimu wa ulipaji kodi kwa Serikali kwa kudai risiti wanaponunua bidhaa mbalimbali. Changamoto hii ikitatuliwa tunaweza kufika mbali zaidi. Vyombo vya habari vya Serikali na binafsi vione umuhimu wa jambo hili. Aidha, katika bidhaa za mafuta tuangalie jinsi gani tunaweza kupata fedha kwa kuongeza angalau shilingi mia ili tupate fedha ziingie katika Mifuko ya Maji na *REA* kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Viwanda; dhamira hii ni nzuri katika ujenzi wa Taifa na kiuchumi. Hata hivyo, viwanda vitakavyojengwa vitumie rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini ikiwemo rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,karafuu ya Zanzibar ingepata viwanda vinavyohitaji, tuna hakika Zanzibar ingepata tija kubwa kuliko inavyopata hivi sasa. Liangaliwe hili kwa mapana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,naipongeza Serikali kuja na Mpango wa Pili mzuri wa Maendeleo, ambao utagusa maeneo mengi, ikiwemo Ilani ya uchaguzi tulioinadi mwaka jana 2015. Pia napongeza Hotuba ya Waziri Mkuu ambayo inaonesha *commitment* ya Serikali kwa wananchi wake. Hatua hii na hatua nyingine mbalimbali ambazo Serikali imeendelea kuchukua, imesaidia kuwapa Watanzania mtazamo mpya wa kufanya mabadiliko kuanzia kwenye ngazi ya familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,rasilimali watu, naomba na kuishauri Serikali iangalie kuboresha maslahi ya watumishi ili waweze kushiriki kikamilifu katika kuchangia ukuaji wa uchumi. Na-*declare interest* mimi ni mhasibu, mkulima na mfanyabiashara pia.

Naishauri Serikali iwatazame kwa jicho kuu watumishi wa Idara ya Takwimu, kwani ikiboreshewa vifaa na huduma wataisaidia Serikali kupata taarifa muhimu zinazohusu hali ya uchumi, changamoto, pamoja na namna ya ufafanuzi wa changamoto kwa wakati. Pia kada ya uhasibu itazamwe, itumike kuisaidia Serikali, kada hii inatumika zaidi kwa sasa kuandaa taarifa tu na hawatumiki kwenye maamuzi, kwani hawaonekani kama viongozi kwenye idara na *agency* za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti,huduma za jamii katika Jimbo la Ushetu; maeneo ya Majimbo, Halmashauri za Wilaya zilizopo nje ya Makao Makuu ya Wilaya zimesahaulika na Serikali kuendelea kuamini huduma zikifika Makao Makuu ya Wilaya mwonekano unakuwa huduma imewafikia wananchi wengi, hivyo naomba yafuatayo Ofisi ya Waziri Mkuu iyazingatie:-

(a) Kwanza, afya, tunahitaji tupatiwe hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, katika Kituo cha Afya cha Mbika, Kata ya Ushetu. Kituo hiki hivi sasa kinahudumia Jimbo la Ushetu na Majimbo jirani ya Ulyankulu na Urambo. Hospitali ya Wilaya ya Kahama pekee imezidiwa kwani inahudumia Wilaya za Mbogwe, Bukombe, yaani wagonjwa wa nje na ndani ni 600 kwa siku.

(b) Huduma ya utawala; tunaomba kupewa Wilaya ya Ushetu ili usimamizi na uratibu wa shughuli za huduma na maendeleo zisimamiwe vizuri. Tuliahidiwa kupewa Wilaya baada ya kupewa Halmashauri ya Wilaya na Jimbo, jambo ambalo limekamilika (rejea hotuba wa Waziri Mkuu ya 2010/2011).

(c) Ujenzi wa barabara kutoka Mpanda- Ulyankulu- Ushetu - Kahama kwa kiwango cha lami; kama ilivyo kwenye Mpango wa Maendeleo na Ilani ya Uchaguzi, barabara hii itajengwa. Hata hivyo, inaonesha usimamizi wa barabara hii itakayohusu mikoa mitatu, yaani Katavi, Tabora na Shinyanga, inaonesha usimamizi unasimamiwa na Meneja *TANROAD* Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nashauri ifuatavyo:-

(i) Usimamizi ufanywe na mameneja wote, kila mmoja eneo la mkoa wake na kuwe na *project* tatu ili usimamizi na uwajibikaji upimwe kimkoa.

(ii) Ujenzi uanze kwenye kila Mkoa husika ili huduma kwa wananchi iende kwa uwiano.

(d) Ushirika; suala la ushirika litazamwe, tuwe na ushirika kwenye sekta zote, wafugaji hawana ushirika madhubuti, hivyo wasaidiwe kikamilifu.

(e) Maji; maji yaliyotoka Ziwa Victoria yamefikishwa Wilayani Kahama, kwa nini yasisambazwe kwa wananchi wa Jimbo la Ushetu.

Mwisho, naunga mkono hoja. Taarifa yangu iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na fursa ya kuwepo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kasim Majaliwa pamoja na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Abdallah Possi na Mheshimiwa Anthony Mavunde, wote kwa pamoja kwa kuunda timu ya uhakika ya kuleta maendeleo. Niipongeze pia timu ya wataalam wa ofisi zote chini ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nipongeze hotuba nzuri ambayo ilisomwa na Waziri Mkuu ambayo imegusa nyanja zote. Niipongeze Serikali kwa kuja na mpango wa kuelekea kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwanza kabisa naomba niishauri Serikali na wataalam, ijipange kuangalia suala zima la sera na sheria pamoja na kanuni mbalimbali ili tufanikiwe katika mipango yetu ya kuwa na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naona kutakuwa na tatizo katika mfumo wetu wa gharama za juu kwenye uzalishaji. Viwanda vingi nchini vimeshindwa kupata mafanikio kwa sababu ya sera yetu ya kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa na Taasisi za Udhibiti *(Regulatory Bodies),* ndiyo maana hata baada ya kuongeza kodi ya kusafirisha nje malighafi, mfano ngozi au korosho ghafi, lakini bado zinasafirishwa ghafi kutokana na gharama mbalimbali za tozo na kodi zinazotozwa katika usindikaji ndani ya nchi kuwa kubwa kuliko hiyo *export levy*.

Pia bidhaa nyingi huingizwa nchini bila kodi yoyote, kama mbegu, madawa ya kilimo (viuatilifu) na mifugo (dawa za chanjo na zinazozalishwa nchini kutozwa kodi na tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali iangalie namna ya kuondoa tozo hizo zinazotolewa na wadau kwa ajili ya huduma zao na badala yake Serikali igharamie gharama za uendeshaji wa taasisi hizo. Leo hii zimebaki kufanya kazi ya kukusanya tozo zaidi badala ya huduma. Baadhi ya tozo hizo ziondolewe kabisa kwa sababu zinaleta ushindani usio wa haki *(no fair trade practice);* waliosajiliwa hutoza zaidi kuliko wasiosajiliwa. Taasisi nyingine hufanya kazi zinazofanana. Pia Serikali iangalie namna ya kuondoa urasimu na kupunguza muda wa kutoa maamuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ni kuongeza bajeti ya utafiti. Utafiti ndani ya nchi unatakiwa kuboreshwa sana. Njia pekee ni kuwekeza katika rasilimali watu, vifaa na kutoa taarifa za utafiti huo *(dissemination of information)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba tuishauri Serikali kama Bunge, itangaze bila kukosa mafanikio yote yaliyofanywa na Serikali. Serikali haitangazi yote yaliyofanywa kutoka miaka mingi iliyopita. Hii inatoa fursa kwa Wapinzani wa Serikali yetu kutusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya makadirio ya mapato ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri, naomba Jimbo la Mufindi Kusini tuliahidiwa kujengewa barabara kwa kiwango cha lami, barabara ya Nyololo hadi Mtwango, Mafinga hadi Mgololo, barabara hii ni muhimu sana kwa

uchumi wa Taifa, pia imepita kwenye maeneo ya Viwanda vya Chai, Karatasi, Mgololo na Mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme; naomba Serikali ipeleke umeme Kata ya Mtambula, Idunda, Itandula, Kiyowela, Idete, Makungu na katika maeneo ya vituo vya afya na maeneo ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji; naomba kutengenezewa miundombinu ya maji. Kuna matanki ya maji 12 hayafanyi kazi sababu miundombinu ya maji imeharibika, ilijengwa 1970, naomba Serikali iitengeneze miundombinu hii ili kuondoa adha kwa wananchi wa Kata ya Igowole, Nyololo, Idunda, Itanduka na Kibao ambao wanapata shida kubwa ya kukosa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Afya; naomba Serikali imalizie kujenga vituo vya afya katika Kata ya Mtwango, Mninga na Makungu. Wananchi wamejenga kuta bado kumalizia tu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuipongeza kwa dhati kabisa hotuba nzuri sana ambayo ni mwongozo kwa nchi yetu iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na niseme mwanzo kabisa kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili, siyo mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee hoja chache, nyingine tutaziwasilisha kwa maandishi. Hoja ya kwanza ambayo nitapenda kuisemea ni hoja dhaifu ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani akidai kwamba pamekuwepo na uvunjwaji wa Katiba na sheria za nchi kuhusiana na Bajeti ambao unafanywa na Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Naomba Mheshimiwa Mbowe…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mbowe ajifunze kwanza kusoma sheria za nchi…

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba ukae tusikilize taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Hajavaa tai, huyo!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nasimama kwa Ibara ya 68(8) na Mheshimiwa Waziri ni msomi na ni msomi kweli kweli, ananizidi mimi. Mimi nina *degree* moja, yeye ni *Doctor*. Anasema asilimia mia mbili. Hili ni neno la uongo ndani ya Bunge, naye hata mki-*record* mkaonesha saa 10.00 usiku, vijana wa Kitanzania watafikiri kwamba kumbe asilimia imehama kutoka 100 imekwenda 200. Naomba Mheshimiwa kwa kanuni ya 63(5) afute hiyo kauli, siyo nzuri sana, Mheshimiwa Waziri namheshimu sana, mpigakura wangu wa kule *home*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge naomba ukae chini. Jamani Waheshimiwa Wabunge, wakati wa *wind-up* hakuna taarifa. Naomba tuendelee na Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jambo la kwanza niweke bayana kwamba wale wanaochangia, wasome kwanza mafungu maana yake nini. Mheshimiwa Mbowe alichanganya kati ya Fungu 62 na Fungu Na. 98. Fungu 62 ni Uchukuzi ambalo ni fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Bunge hili liliidhinisha shilingi bilioni 143.5 na hadi tarehe 31Machi, fedha ambazo zilikuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 56.69. Fungu Na. 98 ni Ujenzi. Fedha za ndani ambazo Bunge hili liliidhinisha ni shilingi bilioni 798.26 na kati ya hizo, shilingi bilioni 606.64 zilikuwa ni kwa ajili ya Mfuko wa Barabara. Shilingi bilioni 191.62 ni kwa ajili ya miradi ya ujenzi, miradi mbalimbali, vivuko, madaraja na nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hadi kufikia tarehe 31 mwezi Machi, fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi, zilikuwa shilingi bilioni 931.3. Kati ya hizo, shilingi bilioni 323.95 zilikuwa ni za Mfuko wa Barabara. Shilingi bilioni 607.35 zilikuwa ndiyo za ujenzi wa nyumba, vivuko na kulipia madeni ya Wakandarasi. Sasa ukichukua fedha zilizoidhinishwa ukatoa zile ambazo zimekwisha tolewa mpaka sasa, zilizozidi ni shilingi bilioni 133.04 ambazo ni sawa na 0.6% ya bajeti yote ya mwaka ambayo ni shilingi trilioni 22.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema hivi, kwanza kwenye kanuni za sheria za bajeti kanuni ya 28(1) inasema, nanukuu: "*All reallocations between Votes shall require the approval of the Minister.*" Kwa hiyo, sheria imenipa mamlaka. *(Makofi)*

La pili, 28(2) inasema hivi, "*reallocations between Votes shall not exceed 5% of the total Government Budget.*"

Nimeshawapigieni hesabu hapa, zilizozidi ni 0.6%. Hakuna mahali popote ambapo sheria ya nchi au sheria ya bajeti imevunjwa. Ndiyo maana nasema huo ni uongo ulio dhahiri na kwa kiongozi kama yeye kutoa takwimu ambazo hazina ukweli ni upotoshaji wa Bunge, ni upotoshaji wa wananchi wa Tanzania. Serikali ya Awamu ya Tano ni makini, inasoma kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya nchi na sheria zote zinazoongoza utekelezaji wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee hoja nyingine moja ambayo ilitolewa, ambapo ilishauriwa kwamba fedha zote za Mifuko ambayo iliundwa na Sheria za Bunge zipelekwe kama zilivyopitishwa na Bunge na ziende kwa wakati. Tunakubaliana kabisa na hiyo hoja na Serikali imeanza kuchukua hatua. Tumefungua *account* maalum kwa kila Mfuko ambao umeanzishwa ili kuhakikisha kwamba fedha hizi za Mifuko hiyo zinalindwa. Kwa hiyo, tahadhari tu hapa ni kwamba utoaji wa fedha hizi utategemea hali ya mapato katika kipindi husika, lakini Serikali imechukua hatua hii, tunaupokea ushauri, tutaendelea kuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea ni ushauri ambao tulipokea kwamba tozo kwenye mafuta ziwekwe kwenye Mfuko wa Maji na iongezwe kutoka Sh. 50/= hadi Sh. 100/= kwa lita ili kuondoa tatizo la maji. Hii ni hoja ya msingi na kwa upande wa Serikali tunasema, kwa sasa hivi, tunafanya uchambuzi wa mapendekezo ya wadau mbalimbali ili tuweze kurekebisha Sheria za Kodi na tozo ikiwa ni pamoja na haya mapendekezo ambayo Waheshimiwa waliyatoa. Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia tu kwamba tutakapokuja mwezi wa Sita kuleta bajeti, ushauri mbalimbali ambao tumepokea, unafanyiwa uchambuzi na mapendekezo yanayotakiwa tutayaleta mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kulikuwa na hoja inafanana na hiyo ambayo ilielekezwa. Kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Jitu ambayo alishauri kama hivyo kwamba tuweke tozo kwenye mafuta na fedha hizo tupeleke kwenye Mfuko wa Mazingira.

Ushauri kama nilivyosema, umepokelewa. Mheshimiwa Jitu Soni ndiye alitoa ushauri huu. Kama nilivyosema, tumeshafungua Akaunti Maalum na tutahakikisha kwamba hizo fedha tunazi-*ring fence,* lakini ushauri tumeupokea, tunaendelea kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee hoja ya mwisho. Tulipokea ushauri kwamba ukuaji wa uchumi unatakiwa uende sambamba na kuongezeka kwa huduma za maji, umeme na miundombinu. Utekelezaji wa mipango na sera

mbalimbali za Serikali, lengo lake ni kuhakikisha kwanza uchumi wa nchi unakua. Kama keki haikui, maana yake hicho tunachogawana ni kidogo mno. Kwa hiyo, ushauri wake ni mzuri kabisa kwamba tukuze kwanza ile keki na hapo ndiyo itatuwezesha kugawana vizuri na kupeleka huduma bora zaidi za jamii za umeme maji na miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja na ushauri mzuri kwamba Serikali iangalie namna ya kuongeza bajeti ya Mfuko wa Pembejeo ili kuboresha Sekta ya Kilimo. Serikali inapokea ushauri huo na tunaendelea kuufanyia kazi kwa sababu nchi hii bila kilimo, nchi ya viwanda haitawezekana. Kwa hiyo, ni hoja ya msingi, tunaipokea na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, naomba kwa mara nyingine tena kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia mbili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri Fedha. Tunamkaribisha sasa hivi Waziri wa Mawasiliano, Mheshimiwa Nape Nnauye.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (HUSM). Ahsante sana kwa nafasi hii uliyonipa. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusa kila kona, bahati mbaya imekuwa dozi kubwa imewafanya wenzetu wapate kiwewe na kukimbia humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na michango ya Waheshimiwa Wabunge kuna hoja zimeguswa. Baadhi ya hoja tutazishughulikia kwenye bajeti ya Wizara tutakapoileta, lakini nimesimama nishughulike na hoja moja ambayo kwa kweli inapotoshwa sana. Ni vizuri tukaweka kumbukumbu na rekodi sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kurusha Bunge moja kwa moja; la kwanza, yanazungumzwa mengi lakini kuna mambo hayasemwi. Jambo la kwanza, mpango wa kuanzisha *Studio* ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulipitishwa na Bunge hili na pesa zake zikatengwa. Hili jambo wenzetu hawataki kuwaambia Watanzania! Wanasema ni mpango ambao umebuniwa, unapitishwa kinyemela kwa lengo la kutaka kuwanyima Watanzania kuona Bunge lao. Huu ni uongo, tena uongo wa mchana peupe, kwa sababu mpango huo ulipitishwa hapa, Mheshimiwa Freeman Mbowe na wenzake walikuwepo na mpango huu waliupitisha. Hili la kwanza, ni vizuri tukaweka rekodi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, la pili, kunasemwa hapa kama vile Bunge hili limezuiwa lisionekane kabisa, kwamba pana *total blackout* ya kuoneshwa Bunge hili. Nadhani *either* ni kutoelewa, uelewa mdogo au wanafanya makusudi baada ya kukosa hoja za msingi za kuja kuzijadili hapa, sasa wanaanza vioja ili ionekane liko tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika, pengine nitafute lugha rahisi wenzetu watuelewe; utaratibu umebadilishwa wa kulionesha Bunge letu, kama ambavyo utaratibu mwingine wowote unaweza ukabadilishwa. Dar es Salaam pale, barabara ya Samora ilikuwa ni barabara inapitisha gari kwenda na kurudi. Kwa sababu ya tatizo la foleni, ule utaratibu ukabadilishwa. Sasa utaratibu ukibadilishwa, anakuja mtu anazira kwenda barabarani kwa sababu utaratibu umebadilishwa kupunguza foleni. Nadhani hapa pana shida ya kuelewa au pana makusudi au pana kushindwa kazi kwa sababu ya kasi ya Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitisha mpango wa kuanzisha *Studio* ya Bunge utaratibu wa kurusha Bunge hili ukabadilishwa na umebadilishwa kwa makusudi yafuatayo:-

Moja; Bunge hili wakati linarushwa mchana, wananchi waliokuwa wanapata fursa ya kuliona Bunge letu, idadi yake ukilinganisha na idadi ya watakaoliona Bunge usiku, kwa takwimu, siyo kwa maneno ya kelele, kwa takwimu, idadi yake inaongezeka. Maana yake ni nini? Maana yake tunatoa fursa kwa Watanzania wengi zaidi kuliona Bunge, kushuhudia kazi za Bunge kuliko ilivyokuwa inatokea mwanzo. Kwa watu ambao wamezoea kupiga kelele, wala hili siyo tatizo, jambo jema, Watanzania wametuelewa na tunasonga mbele bila matatizo. *(Makofi/ Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ambalo hawasemi, Waziri wa Habari, tena Waziri wako, hawasemi na hii ni tabia yao; nami naomba Watanzania wawasamehe na wala sina mashaka, Jumatano watarudi hapa tutaendelea na mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nalo ni kubwa Watanzania hawaambiwi, utaratibu wa kuweka *Studio* hapa Bungeni unarahisisha urushaji wa matangazo ya Bunge bila kulazimisha Vituo vya Habari vya Utangazaji kuja Dodoma na kuleta mitambo yao na gharama za Watumishi kuwaleta Dodoma. Kazi hiyo inafanywa na *Studio* ya Bunge. Uelewa mdogo!

Kazi hiyo inafanywa na *Studio* za Bunge, inapelekwa kwenye *satellite*, chombo chochote kila uwezo wa ku-*link* na kuchukua matangazo haya na kuyarusha kwa gharama nafuu na hivyo inaongeza idadi ya watazamaji, inapunguza gharama na inafanya kazi ya Bunge hapa ionekane zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uongo wa kusema utaratibu huu…

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, naomba mtulizane, tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uongo wa kusema kwamba utaratibu huu unawanyima haki wananchi, pengine tukubaliane, wenzetu wanaposema tafsiri ya mwananchi wanamaanisha mwananchi yupi? Huyu mama ntilie! Huyu mpiga debe! Huyu Machinga! Au wanamzungumza mwananchi yupi?

**WABUNGE FULANI:** Wote!

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Sisi tunamzungumza mwananchi ambaye anaamka asubuhi, anakwenda kufanya kazi zake, jioni anarudi nyumbani kwenda kupumzika, anapata muda wa kutosha wa kuliangalia Bunge na kushuhudia kinachoendelea hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua wenzetu wana *agenda* nyuma ya hili, lakini Watanzania wametuelewa, dhana ya Hapa Kazi Tu imeiweka Serikali hii madarakani, tuendelee bila kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie pia Watanzania hili, jambo ambalo hawaambiwi; inaonekana kama vile utaratibu huu ni wa ajabu sana, lakini Tanzania siyo nchi ya kwanza kwa Bunge lake kuwa na *Studio* yake na kufanya kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabunge yote ya Jumuiya ya Madola yameweka *Studio* za Bunge, yanafanya utaratibu huu tunaoufanya, tena sisi tumeenda mbali tumetoa uhuru kuliko ule uliotolewa na Mabunge mengine. Vile vile Serikali na Bunge tumezungumza na Wanahabari na kuwahakikishia kwamba utaratibu huu kwa Bunge letu ni mpya. Kama mpya, unaweza ukawa na upungufu wake katika utekelezaji wake. Serikali na Bunge tuko tayari kukaa na Wanahabari tukaangalia upungufu uliopo katika utekelezaji wa mpango huu, tukauboresha, tukautekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, tunaomba watuunge mkono. Wameendelea kutuunga mkono na tutaendelea kufanya hivi; Watanzania wanatuelewa, dunia inatuelewa na wasiotuelewa leo watatuelewa kesho, wala siyo mara ya kwanza wao kutoelewa kwa mara ya kwanza. Tutaendelea namna hiyo, tutafanya na tutasonga mbele. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuwapongeza na kuwashukuru sana, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa uzalendo wao na kuamua kubaki hapa kujadili na kutimiza wajibu wao wa Kikatiba, tofauti na wenzetu ambao wanalalamika Katiba inavunjwa, lakini wao wanatoka na kuivunja zaidi Katiba hii wanayodhani wanaitetea. Naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wa CCM na nimalizie kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Habari. Sasa namkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nachukua fursa hii ninapopata nafasi hii ya kuchangia, kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa rehema zake anatuwezesha kushiriki kwa ufanisi mkubwa katika vikao hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imesheheni taarifa katika nyanja zote, kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Taifa hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza, unaweza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata fursa ya kuchangia kuboresha hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao wameitumia haki yao ya Kikatiba kwa ufanisi ipasavyo. Niseme kwamba Katiba katika Ibara ya 63 inatoa haki kwa Bunge na mojawapo ya haki ya Bunge na majukumu yake ni kuisimamia Serikali inapokuwa inatekeleza majukumu yake ya Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya yametajwa, ni pamoja na kuuliza maswali yoyote; swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake, kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti, kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu na wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango huo. Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kutunga sheria na kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Haya ni mamlaka ya Bunge ambayo yamewekwa Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ambavyo Serikali imeleta bajeti yake katika Bunge hili, Serikali kwa namna yeyote haijapoka mamlaka ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba. La sivyo, isingeleta hapa hii bajeti, lakini inajua kabisa kwamba bajeti ni

lazima iende iidhinishwe na Bunge. Kwa hiyo, hoja au madai kwamba Serikali imepoka madaraka ya Bunge, siyo sahihi, ni hoja ambayo haipaswi kuzingatiwa na Waheshimiwa Wabunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba Bunge hili limepewa uhuru na haki ya kujadili, haki ambayo haiwezi hata kupingwa au kuhojiwa katika Mahakama yoyote. Hivi ndivyo Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyosema. Haki hii pia imewekwa katika Sheria ya Mamlaka na Kinga na Haki za Wabunge kwenye kifungu cha (3) na kwenye Kanuni, Kanuni ambazo zinatungwa chini ya Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki hii haipaswi kuzuiliwa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, kifungu cha 29 cha Sheria ya Mamlaka, Kinga na Haki za Wabunge, inafanya kosa la jinai mtu yeyote kumzuia Mbunge asichangie, asitekeleze haki yake ya msingi ya kusimamia Serikali. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo napenda kushauri au kulitolea ufafanuzi ni suala la *instrument* inayotolewa na Mheshimiwa Rais baada ya kuunda Baraza lake la Mawaziri. Hati hiyo inatungwa chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mawaziri au kwa Kiingereza inaitwa *The Ministers (Discharge of Ministerial Functions Act).* Hii ni sheria ambayo inaeleza majukumu ambayo Rais anabaki nayo na hayo mengine anaamua kuwagawia Mawaziri wengine.

Baada ya Mheshimiwa Rais kuunda Baraza lake la Mawaziri, Mawaziri wameendelea kutekeleza wajibu wao, bila hata migongano kwa sababu zile Wizara jinsi zilivyotajwa, kwa mfano Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo, Waziri anatekeleza hayo hayo. Cha msingi tofauti na ambavyo imezungumzwa; na hili ni jambo ambalo siyo zuri sana kwa Waheshimiwa Wabunge; Kifungu kile cha (5) ambacho kimetajwa, hakimlazimishi Mheshimiwa Rais kutoa hiyo hati, kwa sababu kile kifungu kinatumia neno "*may*" na tafsiri za sheria kwenye Kifungu cha 43 imeeleza vizuri kwamba neno "*may*" ni hiari *(discretion)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwa mujibu wa sheria hiyo, kama kuna jambo lolote Kifungu cha 5(2) mtu anataka kujua kwamba hivi suala hili liko mamlaka ya Wizara ipi? Kule Mahakamini ataambiwa nenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Atakapoenda kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakachokisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba suala hili liko chini ya dhamana ya Wizara fulani, ndiyo mwisho wa hilo suala. *(Makofi)*

Kwa hiyo, moja, kitu chenyewe siyo cha lazima, hata kama hapa ameandika "*shall,*" kilichosemwa kwenye sheria ni "*may.*" Cha pili Mheshimiwa Rais hakupewa *timeline,* hakupewa masharti ndani ya muda fulani awe

ameitangaza; na cha tatu, Serikali tofauti na kilichozungumzwa hapa kwamba Serikali inafanya kazi bila mwongozo, hapana. Serikali inafanya kazi kwanza kwa kuzingatia Katiba na Sheria, kwanza Katiba, Sheria na Sera za Chama ambacho kimeunda hiyo Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu ni hiari, tumwachie Rais. Kwa sababu Sheria yenyewe inasema *from time to time*; inawezekana sisi tukawa tunazungumza hapa, huko ameshatoa, sisi hata hatujui. Kama ameshatoa, *well and good* kama hajatoa, tumwachie wakati wowote atakapoona inafaa kutoa atatoa. *Afterall,* hajavunja sheria yoyote kwa sababu sheria yenyewe hiyo, hiyo *instrument* anaitoa yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, hili suala ambalo amelisema Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha kuhusu madai ya kuvunjwa kwa Katiba, amelifafanua vizuri ila naomba kuongeza Waheshimiwa Wabunge kwamba kifungu kilichotajwa cha 41 cha Sheria ya Bajeti, hicho kifungu hakina yale maneno yaliyowekwa pale. Muisome ile sheria, hayapo hayo maneno Waheshimiwa Wabunge, isomeni hiyo sheria. Hayo maneno yaliyosemwa, hayapo na kifungu hiki cha 68 cha sheria hii ndicho kinasema sheria hii ya bajeti yenyewe ina mamlaka ya utawala dhidi ya sheria nyingine zote zinazohusu masuala ya bajeti.

Kwa hiyo, tunatambua kwamba masuala ya matumizi ya fedha pia yanaongozwa na kutawaliwa na Katiba, Sheria ya *Public Finance*, *Appropriation Act* na *Budget Act* na imeweka masharti. Pale ambapo ni lazima kwa masharti yale ya kutekelezwa, Serikali italeta Bungeni, lakini kwa namna ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema mpaka sasa. Mambo yenyewe haya Waheshimiwa Wabunge, ni ya ndani mno ya kiutendaji. Kwa Mbunge asingeweza akayajua haya. Mkitaka kuyajua haya, mtumieni *Controller and Auditor General* ambaye anafanya ile kazi, anasema hapa Serikali imefanya hivi. Sisi wenyewe hatuwezi kujifanya tunao watu wa ndani kuyajua yale mambo. Kama mna watu wanawajulisha yale mambo, basi wanawa-*mislead*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba kusema suala la uhuru wa vyombo vya habari. Hivi vinazungumzwa juu ya Kifungu cha 18 cha hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Naomba nishauri hivi, labda nikisome kifungu hiki: "(a) kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; (b) anayo haki ya kutafuta kupokea na kutoa habari bila kujali mipaka ya nchi; (c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutokuingiliwa katika mawasiliano yake; (d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii."

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, unapoyasoma haya, niwarejeshe kwenye haki zenu za majukumu yenu kwenye Ibara ya 63 kama nilivyosema. Sasa (d) kwanza ibara hii inachosema ni haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali. Haki ya kupewa taarifa, siyo haki ya kutangazwa wakati wote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana huwezi ukaenda Mahakamani popote ukaanza kusema mimi sijatangazwa. Ndiyo maana pia kuna Waandishi wa Habari na sisi tunasoma magazeti kila siku, hata juzi waliniandika *Citizen* na Mwananchi. Taarifa hiyo ni mambo ambayo yameshafanyika na ndiyo maana kuna taarifa za habari katika *Television* na katika Redio na ndiyo vipindi ambavyo vinapendwa sana duniani. Hapa kungekuwa na tatizo, kama Waandishi wa Habari wangekuwa wanazuiliwa hata kuandika chochote kinachoendelea humu ndani, naona Waandishi wa Habari wako pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku Mheshimiwa Waziri Mkuu alipowasilisha hoja yake, Mwandishi wa *Citizen* aliniandikia ki-*note* hapa, akasema Mheshimiwa *AG* tunaomba maoni yako kuhusiana na maoni ya Kambi ya Upinzani. Nikamwambia kwamba subiri majibu ya Serikali tutakapokuwa tunahitimisha na akaandika hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa hakuna haki ya msingi na niseme tu; moja, itakuwa siyo vyema sana ni matumizi mabaya ya haki zetu sisi Wabunge kuacha kuchangia kutetea Jimbo lako, eti kwa sababu haki iliyoko hapa siyo haki ya mwonekano; haki iliyopo kwenye Bunge ni haki ya kujadiliana na kufanya maamuzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya Bunge hayafanywi kwa mwonekano, yanafanywa kwa kujadiliana, kwa kuzungumza au kuandika au kwa kupiga makofi kama unaunga mkono hoja. *That is how decision are made*. Kwa hiyo, itakuwa siyo jambo jema, nami nimewatetea sana kwenye kesi zinazowakabili kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na kesi 52 za uchaguzi, tayari kesi 29 tumeshashinda, unatetea Wabunge waje wawakilishe wananchi wao hapa, halafu wana-*abdicate* majukumu yao, *that is not fair. (Makofi)*

Wananchi wanachotaka ni *what is there* kwenye Jimbo; ni kitu gani? Ni aibu sana kwa Waheshimiwa Wabunge. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge wote, tutumie vizuri Bunge la Bajeti kwa sababu ndilo Bunge ambalo tunasimama kutetea kipato cha Taifa kwa ajili ya maslahi ya watu wetu kule Majimboni. Ni aibu kuacha kuchangia eti unadai kwamba unataka uonekane kwenye *television and that is not very fair. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwa mara nyingine kwamba, naunga mkono hoja hii.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wa kisheria. Sasa tunaendelea na Naibu Waziri, Dkt. Abdallah Possi.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya ambayo ndiyo nyenzo muhimu katika ufanyaji kazi wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa imani yake aliyoonesha kwangu kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na watu wenye Ulemavu. Nasema ni heshima kubwa sababu nafahamu changamoto iliyoko miongoni mwa jamii ya watu wenye ulemavu. Namwahidi sitomwangusha, nitafanya kazi kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti. Namshukuru pia kwa miongozo yake ya kila siku, ambayo siyo tu kwamba imetupa ari lakini imetujenga katika uongozi na naamini ni Waziri Mkuu imara na Wanaruangwa wamepata mwakilishi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Antony Mavunde. Kutoka kwa hawa wawili nimejifunza kwamba umoja ni nyenzo muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali na nafahamu kwamba Wanaperamiho na Wanadodoma Mjini wamepata Wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe na kukushukuru pia kwa ushirikiano wako uliotupa siku zote tulizokuwa hapa Bungeni. Nawapongeza Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote. Sasa kwa mujibu wa kanuni 99(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016 nijibu baadhi ya mambo mbalimbali yaliyoongelewa kuhusu watu wenye ulemavu. Nitayajibu kwa ujumla wao kwa sababu baadhi ya mambo yamerudiwa rudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja kuhusu elimu katika mambo mbalimbali. Niseme tu, tayari Serikali inatambua umuhimu wa elimu kwa watu wenye ulemavu, jitihada zimekuwa zikifanywa. Binafsi nimefanya ziara katika maeneo mbalimbali, nimeona kuna dalili njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi yangu itazidi kuwasiliana na Wizara ya elimu ili kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata elimu sawa na watu wengine, katika suala hilo hilo la elimu limezungumziwa jambo linalohusu Vyuo vya Elimu ya Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu. Ni dhima ya Serikali kuboresha elimu katika Vyuo hivi hasa kupitia Program ya Kukuza Ujuzi inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Niseme tu, haya hayataishia hapa. Vyuo vingine vyovyote vinavyotoa Elimu ya Ufundi, vina jukumu pia la kuhakikisha elimu yao ni shirikishi na tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu ili Vyuo vya *VETA* pia viweze kutoa elimu shirikishi kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa pia suala la ajira. Niseme tu Sheria Na. 9 ya mwaka 2010, lakini pia na Sheria ya Ajira ya *Employment and Labour Relations Act* vinazungumzia kuhusu ajira kwa watu wenye ulemavu. Niseme tu na nikumbushe kwamba ni marufuku kwa mujibu wa sheria zote hizi mbili, mtu kuachishwa tu kazi eti kwa sababu ya ulemavu. Ukweli ni kwamba waajri wana jukumu la kuweka miundombinu na kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyakazi wenye ulemavu, yaani kwa Kiingereza ni *reasonable accommodation*. Kwa hiyo, natoe tu wito kwa watu wenye ulemavu kulizingatia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa pia suala kuhusu majengo ya umma *(accessibility)*. Ofisi yangu imeshaanza kuwasiliana na itaendelea kuwasiliana hasa na TAMISEMI lakini pamoja na Idara na Taasisi nyingine za Serikali ili kuhakikisha kwamba majengo ya umma yanafikika kirahisi kwa watu wenye ulemavu. Hili ni suala la kisera lakini pia ni suala la kisheria lipo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatekelezwa na Serikali iliyoko madarakani kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumziwa pia masuala yanayohusu mauaji wa watu wenye Ualbino, niseme tu hili ni suala ambalo lilianza toka miaka ya 2006. Nashukuru Mungu kwa sasa limepungua, lakini nafahamu suluhisho thabiti la mauaji haya ni watu kuondokana na imani potofu. Watu mara nyingi wanaangalia hili suala kwa uchache wanafikiri ni ushirikina, lakini tunakwenda mbali zaidi, tatizo kubwa ni binadamu kufikiria kwamba mtu mwenye Ualbino ni mtu tofauti. *Once* imani hiyo inapotoka, basi usalama sahihi ndiyo utapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali na itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuwa na mpango madhubuti wa kuondoa unyanyapaa na tayari tuko katika *stage* za awali za kuandaa mpango huo ambao *once* ukifanikiwa baada ya miaka mitano tuna uhakika hali itakuwa nzuri ili wale wanaoishi katika vituo maalum, sasa waweze pia kujumuika na wenzao kwa sababu tunafahamu ni kinyume cha sheria, ni

kinyume cha haki za binadamu kwa watu kuwekwa kwenye makambi pasipo sababu maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limezungumziwa suala la kodi na *incentives* mbalimbali kwa watu wenye ulemavu. Hili ni wazo zuri na teknolojia inapoendelea, inarahisha mambo mengi. Haijaandikwa popote kwamba chombo cha usafiri cha mtu mwenye ulemavu kiwe ni bajaji peke yake. Kwa hiyo, pale ambapo ataweza kuendesha gari, basi Ofisi ya Waziri Mkuu itawasiliana na Wizara ya Fedha ili kutengeneza utaratibu maalum kwamba yale magari ambayo yatakuwa ni nyenzo nzuri ya kujongea kwa watu wenye ulemavu, basi *incentives* zipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia utaratibu kwa sababu nafahamu *experience* ya nchi nyingine, utaratibu huu ulikuwa *abused* kwa mara ya kwanza, lakini walijitahidi wakaweka sawa. Kwa hiyo, ni wazo zuri na tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hapa ambalo kidogo itabidi nilielezee kwa kirefu ni kuhusu makazi ya Watu Wenye Ulemavu. Hoja zilizotolewa, yaliitwa makambi, sidhani kama ni lugha nzuri sana, ni Makazi ya Watu Wenye Ulemavu. Haya yana historia ndefu; yalikuwa ni makazi ya wazee na wasiojiweza na watu wenye ulemavu na ukiangalia historia yake hasa, yalianza kuwatunza waathirika wa ugonjwa wa ukoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba dhamira ya Serikali hasa ukizingatia sheria na mikataba mbalimbali ya haki za binadanu na hasa Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wa mwaka 2006 ni kuhakikisha kwamba mtu mwenye ulemavu anashiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii na siyo kuwekwa kwenye makambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu pia kutokana na changamoto mbalimbali, wapo watu wachache kwa namna moja au nyingine watahitaji msaada fulani. Kwa hiyo, niseme tu kwa wale wanaoishi katika makambi haya kwa sasa Serikali itajitahidi kuyaboresha makambi haya, tayari tulishaanza mawasiliano na Wizara ya Ardhi ili kuzuia uvamizi katika baadhi ya haya maeneo na huduma nyingine zimendeelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, dhima kuu ni kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanaishi katika jamii shirikishi. Kwa hiyo, nikumbushe tena, Halmashauri zina wajibu wa kuwasaidia watu wenye ulemavu ambao hawana msaada lakini jamii pamoja na familia kisheria vyote hivi vina jukumu la kuwasaidia na kuwatunza watu wenye ulemavu ambao watahitaji msaada. Ila kwa hali halisi ni kwamba suala la ulemavu ni suala mtambuka na watu wenye ulemavu wana haki ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limeongelewa suala la kuwezesha watu wenye ulemavu kiuchumi. Niseme tu kwamba kuna baadhi ya mambo kwa kweli yanahitaji tu kubadilisha namna ya kufikiri.

Kwa mfano, tunapozungumzia asilimia kumi ya bajeti ya maendeleo ambayo inakwenda kwa vijana na akinamama katika Halmashauri mbalimbali, hakuna kikwazo chochote cha sheria kwa Mtendaji wa Serikali kutoa kipaumbele maalum kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweke msisitizo tu na niseme kwamba kwa sababu watu wenye ulemavu ni watu ambao waliachwa nyuma kwa muda mrefu na kwa sababu *affirmative action* (kipaumbele maalum) kimekuwa ni jambo la kawaida cha kuwakwamua watu walioachwa nyuma kwa muda mrefu, imefanywa hapa katika jinsia lakini hata katika zile nchi ambazo zili-*suffer* ubaguzi wa rangi, yalifanywa hivyo kwa makundi maalum yaliyobaguliwa kutokana na hali zao. Hivyo basi, kutokana na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu na Katiba ya Nchi na Mikataba mbalimbali na sera nitoe maagizo tu kwa Watendaji wote wa Serikali, sasa kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu siyo *option* kwa sababu ni suala la lazima ili kuhakikisha kwamba usawa halisi kwa watu wenye ulemavu unapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, naunga mkono hoja na niwatakie heri Mawaziri wote na Viongozi wote wa Serikali katika kuchapa kazi, waendelee kufanya kazi vizuri. Nitoe ushauri tu kwa wenzangu wa upande wa pili, wapo watu wanaosema kwamba utakuwa una busara sana *if you try to hide a bit of your stupidity. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Possi. Sasa namkaribisha Naibu Waziri, Mheshimiwa Anthony Mavunde!

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kwa sababu, ni mara yangu ya kwanza kuchangia na kusimama kutetea hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuniteuwa na kunipa dhamana ya kuhudumu katika nafasi ya Naibu Waziri Kazi, Vijana na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kwa ushirikiano mkubwa na miongozo mbalimbali ambayo amekuwa akitupa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Abdallah Possi, kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakinipa katika utekelezaji wa majukumu yetu, lakini pia na Mawaziri wengine wote wanaounda Baraza la Mawaziri kwa miongozo yenu na ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia, kipekee kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao kwa kura nyingi sana. Nataka niwaahidi tu kwamba, kwa yale ambayo waliyatazamia kutoka kwangu nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu niweze kuwatumikia vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba sasa uniruhusu nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo ziliwasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge walichangia, moja ya mambo yaliyojitokeza wakati wa uchangiaji, lilijitokeza suala la ukaguzi wa Sera ya Uwekezaji katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* pamoja na Benki Kuu ya Tanzania ilitoa Mwongozo wa Uwekezaji wa mwaka 2015 ambao kwa mujibu wa mwongozo huo *SSRA* na *BOT* imekuwa ikifanya *special inspection* kwenye miradi yote ya uwekezaji ambayo inahusisha Mifuko ya Hifadhi ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, lengo kubwa sana la kaguzi hizi ni kuhakikisha kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inawekeza katika miradi ambayo itakuwa ina tija na manufaa kwa Watanzania. Pia, kupitia *SSRA* zimekuwa zikifanyika kaguzi za mara mbili kwa mwaka ambapo lengo lake kubwa ni kuweza kuangalia miradi hii ambayo inawekezwa na kuona namna ambavyo inaweza kuleta tija hasa katika maeneo ambayo yanawagusa Watanzania moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ilijitokeza hoja ya kuhusu Mikataba ya Wafanyakazi na vilevile wageni wasiokuwa na vibali vya kazi. Serikali imeendelea kufanya kaguzi mbalimbali kwa kutumia Maafisa Kazi waliopo nchini ili kuweza kubaini Waajiri wote ambao hawatoi mikataba kwa Wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie tu fursa hii kutoa agizo kwa waajiri wote nchi nzima kuhakikisha kwamba wanatoa mikataba kwa wafanyakazi wao na Serikali haitasita kuendelea kuchukua hatua itakapobainika kwamba Waajiri hawatoi mikataba kwa Waajiriwa wao, jambo ambalo kwa mujibu wa Sheria zetu tutawachukulia hatua ili kuona ni namna gani sasa wata-*comply* na masharti ya Sheria zetu za Kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la vibali vya ajira kwa wageni, tumeendelea kufanya kaguzi mbalimbali katika maeneo ya kazi kuweza kuwabaini wale wageni wanaofanya kazi pasipokuwa na vibali au ambao wanakiuka vibali vya kazi na hatua stahiki zimekuwa zikichukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mashahidi, mmeona ziara mbalimbali ambazo zilifanywa na Mheshimiwa Waziri pamoja na mimi Naibu wake, kupitia katika maeneo tofauti tofauti ya kazi na tumekuwa tukichukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba wale wageni wote waliokuja kufanya kazi nchini, kwa mujibu wa Sheria Na. 1 ya Mwaka 2015, wanafuata masharti ya Sheria na tunahakikisha kwamba vibali vya kazi walivyopewa wanavifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu ambazo wameziomba. Kwa hiyo, ikibainika tofauti, tumekuwa hatusiti kuchukua hatua na wako wageni wengi ambao tumewafutia vibali na wengine kusafirishwa nje ya nchi kwa kukiuka masharti ya Sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilijitokeza pia, hoja nyingine ya kuwajengea uwezo Maafisa wa Vijana katika Halmashauri na Viongozi wa *SACCOS*. Hoja hii ilijitokeza kama ushauri na kwa niaba tu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, niseme kwamba ushauri huu tumeupokea, tutaufanyia kazi kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini. Hata hivyo, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imeshaanza kuwajengea uwezo Viongozi wa *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya vijana na kufikia Machi mwaka huu, tayari vikundi 2,552 vilikwishakupatiwa Semina mbalimbali kuhusiana na masuala ya ujasiriamali, kilimo na masuala ya uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja nyingine iliyojitokeza wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia, ilijitokeza hoja ya kuwa na idadi ndogo ya Watanzania wanaoajiriwa katika Sekta ya Viwanda. Katika hoja hii pia, ilizungumzwa kwamba asilimia kubwa ya watu wengi ambao ni wageni ambao wanafanya kazi katika maeneo haya, wamekuwa wakichukua kazi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi kama Serikali, kama nilivyosema pale awali, tumeendelea kuisimamia na kuitekeleza Sheria Na. 1 ya mwaka 2015 ambayo imeweka utaratibu wa kuwaajiri wageni ndani ya nchi yetu, hasa katika maeneo ambayo yana upungufu wa wataalam. Ili kuhakikisha kwamba idadi

kubwa ya vijana wanaajiriwa katika viwanda vyetu, tumeendelea kufanya kaguzi mbalimbali na lengo lake ni kuweza kubaini wale wafanyakazi wageni ambao hawakidhi masharti ya Sheria Na.1 ya mwaka 2015 kwa kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimwondolee hofu Mheshimiwa Mbunge, mama yangu Mheshimiwa Mama Vullu, ambaye katika hoja yake alisisitiza pia, kwamba ikiwezekana, basi tuongozane naye katika eneo lile la Mkuranga ambako kumekuwa kuna changamoto kubwa kwamba viwanda vingi ambavyo viko pale, wanaofanya kazi, wengi ni wageni ambao hawana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwahidi tu Mheshimiwa Vullu kwamba kwa sababu tumedhamiria kuwatumikia Watanzania, niko tayari muda wowote kushirikiana naye kwenda kuhakikisha kwamba tunafanya kaguzi ili kuwabaini wale wote ambao ni wageni wanaofanya kazi pasipokuwa na vibali vya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, ilizungumzwa hoja kuhusu masuala ya afya na usalama mahali pa kazi. Ni kweli nataka nikiri kwamba kumekuwepo na changamoto kubwa sana, lakini Serikali imeendelea kufuatilia kupitia *OSHA* na imesajili na kukagua maeneo takriban 39 katika eneo la Mkuranga na hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kwanza ambazo zimekuwa zikichukuliwa tunapokwenda kufanya kaguzi na kukuta kwamba katika baadhi ya maeneo Sheria haijafuatwa kwa maana ya masuala ya afya na usalama mahali pa kazi, hatua ya kwanza imekuwa ni kutoa hati ya kumtaka Mwajiri afanye marekebisho, lakini pale inapoonekana kwamba hali hairidhishi na bado hakujafanyika hatua zozote za marekebisho, basi tumekuwa tukichukua sheria za kuwatoza *fine* na kuwapeleka Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumzwa pia hoja ya utengaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli za vijana na hii ilitokana na kuwa kumekuwepo na tafrani hasa baada ya Mheshimiwa Rais kuzungumza, kuwataka vijana waache kucheza *pool* na kwenda kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulizingatia hilo, Serikali kupitia Wakuu wa Mikoa yote Tanzania imeelekeza Halmashauri za Wilaya na Serikali za Mikoa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya, lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba vijana wanapata maeneo ya kufanya shughuli za uzalishaji mali. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kuendelea kuwasisitiza viongozi wote wa Halmashauri za Wilaya na viongozi wa Mikoa kuendelea kutenga maeneo maalum kwa ajili

ya vijana ili wapate shughuli za kufanya; kilimo na shughuli za ujasiriamali kama ambavyo imekuwa maagizo yakitolewa mara kwa mara na Mheshimiwa Rais alivyoagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilizungumzwa hoja ya fedha za mikopo ya asilimia 10 kwa ajili ya makundi ya akinamama na vijana. Ushauri huu umepokelewa na Ofisi ya Waziri Mkuu imeweka mkakati kuhakikisha kwamba fedha hizi zinawafikia walengwa kuhakikisha kwamba mapato ya ndani ya Halmashauri, zile 5% kwa makundi ya vijana na akinamama zinayafikia makundi haya. Pia, tumeweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba Halmashauri zinatoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo la Mheshimiwa Rais kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kutoa rai kwa vijana nchi nzima kuhakikisha kwamba wanaendelea kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali ili waweze kupata fursa ya kuweza kuwezeshwa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, kwa kutambua kwamba tuna changamoto kubwa sana ya ukosefu wa ajira kwa vijana, tumekuwa tuna mipango mbalimbali ya kuhakikisha kwamba vijana hawa kwanza kabisa tunawatambua; pili, tunawarasimisha na hatua ya tatu tuone namna gani tunaweza tukawawezesha kiuchumi ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachukua tu fursa hii kuwaomba vijana wote nchi nzima waendelee kukaa katika vikundi vya uzalishaji mali ili sisi kama Serikali sasa, tuwe katika sehemu ya kuweza kuwasaidia katika kuwawezesha kiuchumi ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nichukue fursa hii kipekee kabisa kuwahimiza vijana wote nchi nzima kuendelea kufanya kazi kwa bidii hasa tukizingatia kwamba vijana ndiyo nguvukazi ya nchi hii. Nasi kama Serikali tutaendelea kuandaa mazingira wezeshi ya kuwafanya vijana washiriki katika uchumi wao na watumie muda wao mwingi katika kuujenga uchumi wa nchi yetu, badala ya kufanya shughuli ambazo hazina tija na zisizokuwa za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili, nataka tu nisisitize ya kwamba takwimu zimeonesha nguvu kubwa hii ya vijana imekuwa ikitumia muda mwingi kufanya shughuli ambazo hazizalishi na zisizokuwa na tija kutokana na tafiti mbalimbali ambazo zimeelekeza. Kwa hiyo, ni vema sasa vijana wetu na sisi tukabadilisha mtazamo katika nchi yetu hii tukajielekeza katika kushiriki moja kwa moja kwenye shughuli za kiuchumi ili na sisi kama nguvu kazi ya Taifa tuwe sehemu ya ujenzi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe vijana wote nchi nzima kuchukulia agizo la Mheshimiwa Rais la kufanya kazi kama ni sehemu ya kutekeleza wajibu wetu kama wananchi wema katika nchi yetu, lakini na sisi tuoneshe mchango wetu katika kuhakikisha kwamba tunatoa mchango katika nchi yetu katika kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie tu kwa kufanya nukuu kutoka Kitabu cha Virgil's Georgecs katika mashairi haya, mstari namba 146; yalisomeka pale maneno ya Kilatini ambayo yanasema, "*Labor omnia vincit*" ambayo tafsiri yake ni kwamba, *Work conquers all,* ambayo inashabihiana kabisa na falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Hapa Kazi Tu, ikituhimiza kwamba kila mmoja kwa nafasi yetu hasa vijana, tuhakikishe kwamba tunatenga muda wetu kwa ajili ya kufanya shughuli za kuzalisha, tusaidie kujenga uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujibu hoja hizo ambazo Waheshimiwa Wabunge, walizizungumza nichukue tu fursa hii kipekee kabisa nami niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia, lakini ambao wametushauri katika namna bora ya utekelezaji wa majukumu yetu ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nasi kama Wizara tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunatatua kero, changamoto na matatizo mbalimbali ambayo yanawakabili kundi kubwa hili la vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, kwanza nawashukuru wote kwa mchango wenu, Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri. Sasa natoa kwanza fursa kwa Mheshimiwa Heche na utaratibu wake! Hayupo! Haya, basi sasa…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Haya, sasa nitatoa Miongozo. Nani na nani wanataka Miongozo?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Waitara!

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Sware Semesi!

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Immaculate!

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa ajili ya Mwongozo, nasimama na Kanuni ya 68(7), niki-*quote* Kanuni ya 64(d), (f) na (g), nikiomba Mwongozo kuhusu Mheshimiwa Dkt. Possi, wakati anahitimisha *statement* yake alisema kuwa, itakuwa jambo la busara kwa upande wetu huu wa UKAWA sana, *if we try to hide a bit of our stupidity.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona hiyo Kanuni ya 64, kama nilivyo-*quote* (b), (f) na (g) vimekiukwa. Ahsante. Naomba afute hiyo kauli!

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa mwingine!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7), natumia Kanuni ya 63 na 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kanuni ya 63(1), pamoja na kuzingatia Ibara ya 100 ya Uhuru wa Kutoa Mawazo katika Bunge, inakataza kusema uwongo. Vile vile imesisitiziwa katika Kanuni ya 61(1)(a), kusema uwongo na (b) kwenye mambo ambayo hayako kwenye mjadala. Pia (f) inasema kumsema vibaya Mbunge au mtu mwingine yeyote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Malembeka anazungumza humu Bungeni, alisema, mimi Mbunge wa Ukonga nimekatazwa kuzungumza humu ndani na CHADEMA, kitu ambacho siyo kweli!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyooo! *(Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Pili, wakati Mheshimiwa Goodluck anazungumza, akasema Kiongozi wa Upinzani Hotuba yake ameandikia pale mlangoni, jambo ambalo siyo kweli. Vile vile Mheshimiwa Dkt. Possi wakati anachangia anasema tujaribu kuficha ujinga wetu au upumbavu wetu! Ni maneno ya kuudhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Mheshimiwa Dkt. Mpango amerudia, niliomba Taarifa, akarudia akasema anaunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili. Hili ni Bunge, ni chombo halali cha Kikatiba cha Kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa kutumia Kanuni ya 63(5), hawa niliowataja ama wafute kauli zao au wathibitishe hayo maneno waliyozungumza kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa mwisho, kama yupo mtu mwingine!

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Taarifa!

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa!

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kutumia Kanuni hizo hizo alizozungumza Mheshimiwa Waitara, naomba afute kauli yake ya lugha ya kuudhi aliposema Mheshimiwa Malembeka yeye sio Mbunge wa Ukonga, haruhusiwi kuzungumzia masuala ya Ukonga. Kama yeye, naye sio Mbunge Ukonga! Hii nchi yetu haibagui. Mtu yeyote anaruhusiwa kwenda kugombea kokote, ana uhuru na ana haki ya kuongea lolote lile. Kama anataka kusema hivyo, basi naomba afute kauli yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella! Huo ni Mwongozo wa mwisho! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Mwongozo kwa mujibu wa Kifungu Namba 68(7). Mwongozo wangu unahusu dhamira ya kuwa na matumizi bora ya muda katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, tuko Wabunge wengi na tunahitaji kuchangia michango muhimu sana ili kuwasemea wananchi wetu na kufanya yale ambayo yanatakiwa katika Majimbo yetu, lakini kumekuwa na matumizi mabaya ya muda kwa sababu ya miongozo ya kukatizakatiza watu wanapozungumza, hasa wanapozungumza Wabunge wenye hoja za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. Tutakwenda kwa mtindo huu au tutaendelea kusikia watu ambao wameamua kutokuchangia na kuwakatisha watu wanapopata mtiririko wa kuchangia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa. Miongozo yote nimeipokea na itatafutiwa muda muafaka na itajibiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tutahitimisha…

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi! Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kessy, tumemaliza Miongozo au unataka Mwongozo tena!

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumjulisha Mheshimiwa kuhusu 200% au 500%. Naona yeye *degree* yake kidogo imecheza! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia unaweza ukasema hata 200% au 300%, kutokana na uchumi wako. Kwa mfano, nimenunua kitenge Sh. 10/= nimeuza kwa Sh. 200/=, inakuwa nimeuza kitenge nimepata faida 300% ama 400%. Haelewi, *degree* yake asome upya huyo! *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Keissy.

Waheshimiwa Wabunge, kwa leo tumemalizia wachangiaji wetu kwa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja hii itahitimishwa siku ya tarehe 27 mwezi wa Nne na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista Mhagama na Waziri Mkuu mwenyewe, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo moja hapa, mnaombwa au mnakumbushwa kupitia kwenye *pigeon box* zenu kuchukua vitabu vya Bajeti vya Hazina.

Waheshimiwa Wabunge kwa vile kesho ni Sikukuu ya Kitaifa, siku adhimu ya Muungano wetu, nichukue fursa hii kuwatakia kila la heri Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Watanzania kwa ujumla.

Baada ya kusema hayo, sasa naliahirisha Bunge hili hadi siku ya Jumatano, tarehe 27 Aprili, 2016 saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Jioni, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 27 Aprili, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*